

KRISTO NI SIRI YA

MUNGU ILIYOFUNULIWA



Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Endeleeni tu kusimama kidogo tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

² Baba wa Mbinguni mwenye neema, tunakukaribia Wewe tena asubuhi ya leo kwa ajili ya rehema na kwa ajili ya mwongozo wa Roho Mtakatifu leo, kama ilivyotufunukia, ya kwamba inatupasa kukutana pamoja asubuhi ya leo na kufundisha Neno Lako, na ili tujue jinsi ya kuishi katika siku hii ya sasa, na ni wakati gani wa siku tunaoishi. Tungeomba mwongozo wako mtakatifu kwa mawazo yetu, mioyo yetu leo, kwamba ungetuelekeza kwenye kila Neno ambalo ni muhimu kwetu kujua; kwamba ungefungua vinywa vyetu wazi, na mioyo yetu, pia, kupokea, na yale ambayo ungesema nasi, na ungefungua vinywa vyetu kwa mambo ambayo si sawa, tukijua ya kwamba ni Wewe tu unayeweza kulifunua Neno la Mungu.

³ Na sasa kwa kuwa inanibidi kuliacha hili kanisa dogo mara moja kwenda sehemu zingine za ulimwengu, ninawakabidhi Kwako, Bwana. Ambao, wao ni moyo, kitovu cha moyo wangu, tuseme. Wao ndio—ndio wamezaliwa Kwako, kwa Roho na kwa Neno la Kweli. Nami naomba ya kwamba utawabariki, Bwana, na kuwaweka wameunganishwa pamoja kwa karibu na vifungo vya upendo wa Kristo.

⁴ Mbariki mchungaji wetu mpendwa, mchungu kondoo. Tunaomba ya kwamba utamtia mafuta kwa Roho Mtakatifu, wa Neno Lako, na kuwafunulia na kulilisha kundi.

⁵ Na mara moja, muda mfupi tu uliopita, ulipoonyesha lile ono, hii maskani ndogo hapa, karibu kuweka Chakula akiba, kwamba utakuja wakati ambapo haya yote yangehitajika. Tulipomwona Ndugu Sothmann na Ndugu Wood wakiwa tayari kuvuka kuingia nchi nyingine, kwenda . . . Lakini Wewe ulisema, “Weka Chakula hiki akiba hapa kwa ajili ya huu wakati.” Bwana, kwa heshima nimejaribu kufanya hivyo.

⁶ Na sasa, asubuhi ya leo, katika somo hili ambalo tumewazia, ninaomba ya kwamba utalifikisha lote kilele chake, Bwana, kuonyesha ya kwamba Wewe ni Mungu, na hili ni Neno Lako na Kweli Yako. Lijalie, Bwana, watu wapate kula humo na kunenepa, tuseme, katika neema ya Mungu, ili waweze kuona kwamba ni rehema kuu ya Mungu kwetu katika siku hii. Wabariki wote waliopo na wale ambao wangependa kuwepo,

Baba. Na ujitwalie Mwenyewe utukufu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Bwana ambariki kila mmoja wenu sasa.

⁷ Nami naamini, kabla tu hatujaanza, tuna mtoto mchanga hapa, wa Collins. Nilikutana na baba yake muda mfupi tu uliopita, na—naye alikuwa na mtoto mchanga aliyetaka awekwe wakfu. Nasi tunataka kufanya hivyo sasa, endapo Ndugu ama Dada Collins, mmojawapo, atamleta huyo mtoto mdogo mbele tupate kuwa na ibada ya kuwekwa wakfu kwa mtoto huyu.

⁸ Kuondoka, mnajua, mbona, husababisha . . . kwa kuwa hawa ni washiriki waaminifu, ni, wa Mwili wa Kristo. Mnaona, kamwe sikusema “wa maskani hii.” “Wa miili ya Kristo,” ule . . . mwili huu hapa, sehemu ya Mwili Wake.

⁹ Nao wana jamaa mdogo hapa wanayetaka awekwe wakfu. Na—na hii daima ni kazi nadhani mke wa—wangu ananionea wivu, kuwashika watoto. Uh-huh. Basi Ndugu Neville, kama utakuja mbele, tafadhali.

¹⁰ Jina lako la kwanza ni nani, ndugu? [Baba anasema, “Clyde.”—Mh.] Huyu ni Ndugu na Dada Clyde Collins, ni ndugu ya ndugu yetu mpendwa hapa, Kasisi Collins, Willard. Nao wamepata nyongeza kwenye idadi ya akina Collins hapa, naona, na jamaa mdogo mzuri sana.

¹¹ Ana umri gani, Dada Collins? [Mama anasema, “Karibu miezi minne.”—Mh.] Karibu miezi minne. Na jina lake ni nani? [“Mark David.”] Mark David. Hilo ni jina zuri sana. Anaonekana kama mvulana mzuri sana. Aisee, kidogo ni mvulana mkubwa, pia.

¹² Sasa najua akina mama hapa wanaweza kumthamini jamaa huyu mdogo hapa. Huyu si ni kipenzi?

Vema, tunapoinamisha vichwa vyetu sasa.

¹³ Baba wa Mbinguni, wakati baba na mama huyu wachanga wanapokuja na donge hili dogo la thamani la mwili wa mwanadamu ambalo limetolewa kwa ndoa yao, likawekwa mikononi mwao lipate kuhifadhiwa kwa ajili ya Bwana Mungu. Kwa uchaji wanamleta mtoto huyu Mark David hapa kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa Mwenyezi, Yeye aliyeweka maskini mvulana huyu wa thamani, afya njema na mvulana mzuri, chini ya uangalizi wao, akalelewe kwa utukufu wa Mungu.

¹⁴ Bwana, wabariki baba na mama. Jalia pipa kamwe lisiwe tupu, nyumbani, wala chupa isiishe kamwe. Baba na awe mzima na mwenye uwezo, Bwana, kufanya kazi na kupata chakula kwa ajili ya huyu jamaa mdogo; jalia mama awe mzima na aweze kukitayarisha; na mioyo yao iwe tayari, Bwana, kumfundisha maskini huyu jamaa, kumlea katika maonyo ya Mungu. Lijalie, Bwana.

¹⁵ Sasa kutoka mikononi mwao, hadi kwa yangu, anakuja mtoto huyu wa kupendeza, maskini Mark David. Nami ninamkabidhi, pamoja na mzee wa kanisa hapa, Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, kwa maisha ya utumishi. Tujalie, Bwana. Pata utukufu kutoka kwa maisha yake. Jalia aishi maisha marefu, hata kufikia Kuja huku kwa Bwana Yesu, kama hilo linakupendeza. Na, ikiwa ni hivyo, jalia aje aubebe Ujumbe wa Bwana Mungu, katika wakati ujao. Lijalie. Mdumishe mwenye afya njema, mwenye furaha, na moyo wake uwekwe daima kufanya mambo yaliyo sahihi, mbele za Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo, tunamtoa huyu mtoto Kwako, katika kuwekwa wakfu. Amina.

¹⁶ Mungu akubariki. Mungu akubariki, Dada Collins, na mvulana huyu mzuri, nawe Ndugu Collins. Mungu awe pamoja nawe.

Waleteni, sisi sote pamoja:

Waleteni, waleteni,
Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
Waleteni, waleteni,
Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

¹⁷ Naupenda huo. Mnaona, waleteni kwa Kristo kabla ibilisi hata hajapata nafasi. Tayari wamewasilishwa Kwake basi kwa maisha ya utumishi.

¹⁸ Je, kuna mtu yeyote anayejua kama familia ya Dauch, yeyote wao, ameshuka kuja huku leo, ama la, Dada Dauch? Ndugu Brown, uko hapa, Ndugu Brown? Naam, nimefurahi. Na nani. . . Ndugu Dauch bado yuko pamoja nasi? Ajabu! [Ndugu Tom Brown anatoa taarifa kuhusu hali ya Ndugu William Dauch—Mh.] Ndugu Dauch karibu atuache. Mnaona, hatuwezi kusema mengi mno wala kuuliza mengi mno, tayari amepitisha miaka ishirini na mmoja ya wakati ambao Mungu alimwambia aishi. Huo ni wakati wa kawaida wa maisha, kupita wakati ambao Mungu alimwambia angeweza kuishi.

¹⁹ Lakini tulipigiwa simu hivi majuzi asubuhi, kwamba alikuwa—alikuwa yuafa, nasi tukakimbilia kule. Naye Bwana Mungu kweli alikuwa mwema kwake, amemwepusha na mauti. Ninii tu, nadhani yu—yuko tayari na anangojea tu Kuja kwa Bwana. Lakini, mnajua, sote hushikana mmoja kwa mwingine. Tunaninii tu. . . Huyo jamaa mzee ni kama—ni kama baba kwangu huku.

²⁰ Ninamkumbuka akiwa ameketi papa hapa chini kwenye maskani ya kale, ile sehemu ya kale, wakati yeye. . . Nuru ile ilipomulika huku, kwenye ubatizo huo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, papo hapo akaja. Na mwenye umri wa miaka themanini na saba au themanini na minane hivi, akiwa na fimbo, akaja papa hapa juu na kusema, “Ninataka kuingia moja kwa moja mle ndani na kubatizwa.” Mtu fulani akaenda na kumletea

nguo. Asingeweza kungojea hadi wakati mwingine; ilimbidi aje papo hapo, papo hapo. Kwa hiyo na—napenda hilo.

²¹ Akasema, hivi majuzi, nilikuwa nikizungumza naye; akasema, “Unafikiri niko sawa sasa, Ndugu Branham?”

²² Nikasema, “Je, uliwahi kwenda kwa daktari kwa uchunguzi wa mwili?”

Akasema, “Naam, bwana.”

²³ Nilisema, “Daktari ataweka stethoskopu masikioni mwake, na kuiweka penye moyo wako, aone kama moyo wako unapiga vizuri; na kadiografu ya umeme, na halafu shinikizo la damu, uchunguzi wa mkojo, na kadhalika, vyombo, apate kujua hali ya mwili wako. Sasa, jinsi anavyofanya hivyo, anaangalia nyuma kwe—kwenye kitabu hapa, ambapo wataalamu wa masuala haya mbalimbali huandika, ‘Kama *hili* likitendeka, tatizo ndilo hili.’”

²⁴ Nami nikasema, “Sasa, stethoskopu pekee niliyo nayo ni Biblia, unaona, kwa ajili ya nafsi.” Nami nikasema, “Nitakupima.” Nikasema, “Yohana Mtakatifu 5:24, alisema, ‘Yeye ayasikiaye Maneno Yangu.’” Nikasema, “Huko si kuketi tu na kulisikiliza. Huko ni kulipokea, unaona, kulipokea; unaliadini Hilo. Kitu ndani yako kinakwambia Hilo ni sawa. Umelikubali, unaliadini, ni lako. ‘Yeye ayasikiaye,’ Hilo tayari ni lako, ‘Maneno Yangu, na kumwadini Yeye aliyenituma.’ Unaadini jambo hilo?”

Akasema, “Ninaadini.”

²⁵ Nikasema, “Basi nitakwambia kile Daktari Mkuu alisema, ‘Amepita toka mautini kuingia Uzimani, wala hataingia tena hukumuni wala kuhukumiwa.’” Nikasema, “Nijuavyo mimi, kulingana na vile Vitabu, umepita mtihani.”

²⁶ Mzee huyo, wa karibu umri wa miaka mia moja, sio mfuasi wa kanisa hata kidogo; lakini mara ya kwanza tu Nuru hiyo ilipomulika njiani mwake, aliipokea. Mnaona hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu zamani ikilala hapo? Uh-huh. Naam, bwana. Unaona, mara tu Nuru inapoipiga, inapata Uzima upesi sana.

²⁷ Sasa, najua kuna joto leo, nami, inaonekana kama ni vigumu kwangu kuwaita ninyi watu pamoja kwa ajili ya ibada ambamo mnasongamana ndani namna hii. Lakini hata hivyo ni—niliwazia, kwa neema ya Mungu, ya kwamba ningekuwa na ibada nyingine kabla sijawaacha ninyi nyote; kwa msimu mfupi, natumaini.

²⁸ Nami sina budi kwenda sasa kesho usiku, huko Chicago, kuanzia Jumatano. Nilifikiri ningefika huko mapema kidogo, ikiwezekana, na kupumzika kidogo kabla ya kuanza mfululizo wa ibada. Nami ninaadini wamelipata... Hapa, nilikuwa nikilitazama papa hapa. Li—limetangazwa huko juu. Unaitwa Marengo... [Mtu anasema, “Marigold.”—Mh.]... eneo, naam,

Marigold, Marigold, naam, eneo, uwanja wa michezo. Uwanja wa Michezo wa Marigold ndipo itafanyika, kuanzia Jumatano usiku, hadi Jumapili. Nao Wafanyabiashara wa Full Gospel wana kiamshakinywa, pia, Ju—Jumamosi asubuhi. Wala sijui ni wapi hasa walipotangazia hilo, kwamba ni wapi. La. Kisha Jumamosi jioni ni huko Lane Tech. Naona hapa i—imetangazwa.

²⁹ Sasa, ikiwa uko karibu na eneo hilo, au huko juu, itakuwa ya kawaida, ibada ya kawaida tu ya uinjilisti kama tulivyo nayo wakati wowote. Karibu Jumbe zote zitakuwa hasa juu ya kitu ambacho kimefundishwa hapa, maana hapa ndipo tunapozitengenezea kanda zetu, mnaona. Huko nje wanaweza kupozana. Lakini wakipata kanda zilizorekodiwa hapa, hiyo ni juu yao kama wanataka kusikiliza kanda yoyote. Inatoka papa hapa. Hii ni mimbara yetu wenyewe.

³⁰ Kwa hivyo huko nje, kwa kawaida mimi hujaribu kuchagua kitu kisicho na kilindi sana, kwa sababu wengi wao wana ujuzi mdogo na kile kinachoingia. Lakini hapa ninahisi nina haki ya kusema chochote ambacho Mungu anaweka moyoni mwangu, kukisema kutoka papa hapa. Kwa hivyo kanda zetu zote zinatengenezwa kutoka hapa. Mnaona? Nao wako moja kwa moja chumbani mle sasa, mnaweza kuona vichwa vyao juu ya kioo chenye mawingu mle ndani, ambamo wameketi na vinasauti vyao.

³¹ Sasa, na kama unataka kuja mkutanoni, tutafurahi sana kuwa pamoja nawe. Ninii tu, ukifika pale, usijue pa kwenda kamwe, mbona, wasiliana tu na yeyote wa Full Gospel, ama—ama Ndugu Carlson, naye ata—atakwambia hiyo ni... Anaweza kukushauri, ama Kanisa la Filadelfia, ama yeyote wao, wanaweza kukuelezea vizuri jinsi ya kufika mahali hapo.

³² Kisha nitarudi Jumatatu ijayo jioni, wakati fulani, alasiri au jioni. Na Jumanne tunarudi Arizona kwa—kwa kuwapeleka watoto shuleni, na kadhalika. Na halafu sijui ni lini hasa nitarudi tena, kwa sababu, Bwana, nataka Yeye aniongoze kuhusu jambo la kufanya.

³³ Jambo la ajabu sana lilitokea. Afadhali... Najua huu unarekodiwa, na ninaweza hata kuliweka hapa. Basi wakati tu maono na miongozo ya Roho Mtakatifu inapotenda kazi, napenda kugusa hasa wakati anapotenda kazi. Hiyo ni... Sasa, katika mwaka jana umekuwa mmoja, moja kwa moja pamoja na mmoja wa wakati mkuu sana wa maono niliyowahi kupata, katika huduma yangu yote, imekuwa ni mwaka huu uliopita, juu ya mambo ambayo yamefanyika, ambapo ninyi watu mnajua ya kwamba lilitabiriwa kabla halijatukia, na lilitukia jinsi tu li—lilivyosema.

³⁴ Sasa, tunarudi hapa, na—na kuzuru. Hali ya hewa mahali hapa, hakika siipendi, kwa sababu ninaninii... hunidhoofisha mara tu ninapofika hapa. Ndipo ninaninii tu... Ninaweza

kuvuka sehemu ya juu ya kilima huko juu na kushuka kwenye bonde hili, nami niko hapa kama dakika kumi na nina mabaka ngozini, ninachefukwa. Hali ya hewa, kuona kizunguzungu, kila kitu kinaonekana mzuka, giza, ndi—ndipo inanilazimu kutoka kwake. Mnaona? Basi hivi majuzi nilikuwa nikizungumza na mke wangu. . .

³⁵ Lakini kinachonileta humu, kwanza, kinachonileta hapa, ni ninyi watu, mnaona, kanisa hili. Ninawaambia, kati ya sehemu zote nilizowahi kwenda maishani mwangu, hapa ndipo mahali ninapopenda zaidi kuja kuhubiri Injili. Na inaonekana kwamba tunaweza kutengeneza kanda kutoka hapa ambayo ni bora mara kumi kuliko mahali pengine popote. Mnaona? Mnaona, hiyo ndiyo sababu ninasema, “Mahali ambapo Mungu anafanya jambo fulani, basi dumu na hayo moja kwa moja.” Lakini nafikiri, ambapo jambo kuu lilipo, hilo lilikuwa ni mimi nikishindwa kutoka mara ya kwanza aliponiita, na kwa hiyo kidogo analifanya gumu kwangu ninapoingia. Kutii ni bora kuliko kafara.

³⁶ Na ndipo nitakuwa nikija na kurudi, wakati wote, nikihubiri maskanini. Nanyi watu mnaotoka nje ya mji, mtaarifiwa. Billy Paul atakuwa hapa, papa hapa ofisini, na—na inaweza kufikiwa wakati wowote, kupitia kwake. Nasi tutarudi hapa, tufanye. . . Na ndipo zile Baragumu Saba zinakuja mara moja, Bwana akipenda, Mapigo Saba ya Mwisho, na vile Vitasa, na kadhalika, tuwezavyo tu, tukipata hali ya hewa ya baridi kidogo, labda, ama chochote kile, vyovyote Bwana aongozavyo.

³⁷ Na sasa, hivi majuzi, nikiingia, kulikuwa na swali lililoletwa kuhusu jambo fulani, kuhusu mtu fulani aliyekuwa amenipa hu—hundi, nayo ilisema “binafsi,” haswa kwangu tu, na mimi pekee, “ushuru umelipwa, bure,” chochote kile. Vema, tukaenda, naye Billy alijua ya kwamba kwa namna fulani nilihitaji hiyo hundi, sasa.

³⁸ Akaenda na kuwauliza mawakili kama tungeweza kutoa pesa. Akasema, “Mbona, yeye ni raia wa Marekani. Kwa nini asiweze kuzitoa hizo pesa? Mnaona, inasema, ‘ushuru umelipwa,’ na mengine yote, ‘bure.’ Raia yeyote anaweza kufanya hivyo.”

³⁹ Kwa hiyo basi asingeweza kuridhika na hilo, Billy, kwa hiyo anamwendea mhasibu wa umma. Akasema, “Mbona, bila shaka, anaweza kutoa pesa hizo.” Kasema, “Yeye ni raia wa Marekani.”

⁴⁰ Kwa hivyo, vema, asingeweza kuwazia mema juu ya hilo, kwa hivyo akamwita Merle Miller, huyo ndiye mkuu wa shi—shirika la ushuru huko—huko Indianapolis, walikuwa mawakili wetu, na kwa hiyo Ice na Miller. Kwa hiyo, “Hakika, ni sawa. Mnaona? Hakika, anaweza kuwa na hiyo hundi. I—i—imeandikiwa yeye, ‘mwidhinishwa pekee.’” Ninaweza, ndimi pekee ninayeweza kuiidhinisha, kadhalika, wala isingeweza kupigwa stampu kwa ninii yetu. . .

⁴¹ Mnaona, sitoi pesa kwa hundi. Hilo ndilo walilonishtakia wakati ule mwingine. Mtu analeta lundo la hundi, na kusema, “Haya, Ndugu Branham,” mkutanoni. Ningesema, “William Branham, William Branham...” Vema, serikali ilikuwa ikishughulikia hayo yote, wakati wote. Nami nilikuwa nikizisaini mwenyewe na nilikuwa nikilipa madeni huko nje, lakini walisema ninadaiwa deni ya kodi kwa hizo zote, hata hivyo, dola laki tatu. Hivyo—hivyo basi hapo ndipo mzozo ulipotokea.

⁴² Kwa hiyo basi mara tu nilipoweka hundi hii, masalale, huyu hapa yule ajenti anarudi moja kwa moja, akasema, “Tutamfungulia mashtaka tena sasa.” Kwa hiyo kidogo lilitatiza.

⁴³ Naye Ndugu Lee Vayle anayeketi hapa, nadhani ni sawa kulisema, tulinii tu... Alikuwa ameshuka, naye Mbaptisti huyu mzuri msomi hapa alikuwa... Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, hapa kwenye dimbwi hivi majuzi, Ndugu Lee Vayle. Na kwa hiyo yeye ni mtu mzuri sana, ndugu katika Kristo. Ametuhubiria hapa awali, na ni mwenye elimu ya juu sana kiakili, na, zaidi ya hayo, mtu anayeongozwa na Roho. Nuru ilipommulika, alisema alijaribu kuondoka, lakini asingeweza kamwe, kwa hiyo nilimbatiza papa hapa hivi majuzi asubuhi. Asingeweza kuvumilia tena, kwa hiyo tulishuka tu hapa na kuvaa nguo zetu na kuingia ndani, naye akabatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

⁴⁴ Vema, niliwazia, kwa kuwa alikuwa amekula chakula hicho kizuri cha kiroho, labda kusudi tuingee kidogo tungekula chakula asili. Kwa hiyo tukaenda kwenye Blue Boar, tukaketi, tulikuwa tukiongea, ndipo hiyo hoja ikatokea, “Unawaachaje watu waongee juu yako hivyo?”

⁴⁵ Sasa, Ndugu Vayle ni mmoja wa watu wazuri sana niliopata kujua, lakini yeye “ni mwenye pupa sana,” sikuzote nilimwambia, mwajua. Na kwa hiyo, yeye, kwa hiyo mimi nikasema... Natumaini hilo ni sawa, Ndugu Vayle. Kwa hiyo yeye... Nikasema, “Usirukie mambo mara moja. Tulia. Mungu Ndiye anayelifanya.”

⁴⁶ Akasema, “Ah, inaweza kuwa sawa kwako,” akasema—akasema. Lakini, vema, yeye—yeye... Naamini yeye—yeye ni mwerevu sana hata hao ndio wamekuwa wakimkabili, hao watu werevu wenye akili; kwa hiyo anajua tu jinsi ya kuimimina hiyo hapo ndani, nao hawana mahali pa kusimamia. Hivyo tu.

⁴⁷ Kwa hiyo nikasema, “Angalia, Ndugu Vayle.” Tulikuwa tumeketi katika Blue Boar. Nikasema, “Daudi, siku moja, baada ya kuondolewa mamlakani na mwanawe mwenyewe, alitoroka akakiacha kiti cha enzi, maasi, Israeli ikagawanyika, naye Daudi akaondolewa mamlakani na mwanawe mwenyewe, basi alikuwa akitoka nje ya mji, akilia. Ndipo jamaa ambaye hakupenda ujumbe wake wa siku za mwisho, mwajua; hakumjali; maskini

jamaa mdogo, kidogo ni kiwete, akienda zake pale, akimdhihakiki, naye akamtemea mate Daudi. Ndipo yule mlinzi akauchomoa upanga ule, akasema, ‘Ati nikiache kichwa cha mbwa huyo kikae juu yake, ambaye amemtemea mate mfalme wangu?’ Daudi akasema, ‘Mwacheni. Bwana alimwambia afanye hivyo.’ Unaona? Kumtemea mate, kumdhihakiki, kisha kumtemea mate. Kasema, ‘Bwana alimwambia afanye hivyo.’ Vema, tunajua hiyo hadithi, jinsi ilivyoishia. Ndugu Vayle aliwazia hilo lilichukua neema nyingi sana kufanya hivyo.

⁴⁸ Basi mara tu aliporudi na kuingia ofisini, mhasibu wa umma alimpigia Billy Paul simu na kumwambia kuhusu hili. Kwa hiyo Ndugu Vayle akapanda nyumbani pamoja nami. Nilipoingia, nilimwambia mke wangu. . . Yapata wakati fulani mwendo wa alasiri. Tuliingia chumbani. Nikasema, “Nina jambo la kukwambia, Mpenzi.”

⁴⁹ Tulikuwa tukiongea tu kabla sijaondoka. Akasema, “Bill, najua ya kwamba Mungu alikutuma huko nje; sote tunajua hilo, lakini kamwe hakukwambia urudi. Alisema. . . Sasa, hapo ndipo pananitia wasiwasi.”

⁵⁰ Nikasema, “Naam, nadhani ni kwa ajili yako na watoto. Haijalishi kwangu. Nitamtumikia, Bwana akipenda, popote niendapo.” Na kwa hiyo nikarudi, nami nikamwambia jambo hilo namna hiyo. Kwa hiyo nikageuka tu, nikaiweka kofia yangu juu.

⁵¹ Ndipo mtu fulani akasema kitu, kuhusu, “Loo, huyu mtoza ushuru! Tunapaswa kutoka nje. . .” Kwa namna fulani akashambulia kitu kama hicho.

⁵² Bila kufikiria yale niliyokuwa nimemwambia Ndugu Vayle, nikasema, “Achaneni na yeye. Labda Bwana alimwagiza afanye hivyo.”

⁵³ Kabla sijamaliza kusema hivyo, Nuru ikamulika ukutani na kuandika pale, Ndugu Vayle na mke wangu wameketi pale, “Rudi Arizona.” Huku herufi zimeandikwa ukutani, “Rudi Arizona.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo mimi hapa naenda, amina, kurudi Arizona.

⁵⁴ Sasa, juma hili limekuwa juma la baraka kuu. Tulikuwa na mahojiano ya faragha wiki hii, ya watu waliokuwa wakingoja tangu ile *Mihuri Saba*. Nami sina shaka ila baadhi yao, bila shaka, waliitwa kutoka nje ya mji, kote nchini. Lakini ile asubuhi kabla ya hayo mahojiano kuanza, nikiwa nimeketi chumbani, Roho Mtakatifu alinjalia kuandika kila kitu walichojua, kila kitu walichotaka kuuliza, nikayapindua hayo maswali jinsi walivyotaka, na kuwambia ndoto zao na fasiri zao kabla hawajaniambia.

⁵⁵ Sasa, watu wako chumbani humu, kule. Na ningeendelea na kuwaacha waongee. Wangesema, “Vema, Ndugu Branham, ninatoka *ninii*.”

56 Nikasema, “Sasa, kumbukeni, tumekusanyika hapa si kwa ajili ya ushirika. Hatujaja hapa kushirikiana sisi kwa sisi. Kuna swali akilini mwako, moyoni mwako, ambalo—ambalo umejikwaa nalo wala hujui ni nini. Na labda nitaweza, kwa msaada wa Mungu, kufanya jambo hilo.”

57 Nikasema, “Kumbukeni, malkia wa Kusini alikuwa na maswali, pia, alipomjia Sulemani. Nayo Biblia ilisema hapakuwa na jambo lolote lililofunuliwa au lililofichwa ambalo Sulemani hangeweza kujibu.” Nami nikasema, “Aliye mkuu kuliko Sulemani yuko hapa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Bwana Yesu aliahidi, ‘Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, hapo Mimi nipo katikati yao. Na chochote wanachoweza kufikiria, au kutamani, na—nao wataomba, watapewa.’ Na sasa swali lako ni jambo usilolijua, kitu ambacho hujui jinsi ya kukikaribia, kitu ambacho hujui cha kufanya kukihusu.”

58 Nami nikasema, “Tena, Maandiko yalisema hivi, ya kwamba, ‘Malaika wa Mungu hufanya kituo wakiwazungukia wale wamchao,’ hivyo katika ulimwengu mwingine ambapo zile hisia tano hazitangazi.”

59 Zile hisia tano huwasiliana tu na ulimwengu huu. Kama hukuwa na hisia, hungeweza kuhisi chochote. Hisia haingekuwa kitu kwako; huo ungekuwa ni ulimwengu mwingine. Kama hukuwa na macho, unachotazama kingekuwa ulimwengu mwingine, usiufahamu kabisa. Kwa hiyo hisi hizi tano ndicho kitu pekee ambacho Mungu alituachia.

60 Sasa kuna nyingine inayoitwa imani. Lakini kwa imani unapanda ngazi, na hatimaye unaweza kupanda juu sana mpaka ukaingia katika ulimwengu mwingine, ambao ni maono. Huko unaweza kuona.

61 Kama vile endapo hukujua ni kitu gani hiki ulichokuwa unahisi kwa hisi yako ya kugusa, hukuwahi kukiona; ndipo macho yako yakafunguka, ungeweza kukiona. Yote yangukuwa ni fumbo kwa mtu huyo ambaye asingeweza kuona. Ingekuwa ni siri kwake, lakini hata hivyo hicho ndicho.

62 Na hapo ndani, Bwana . . . Kabla hatujafika hapa, kwa watu kutoka kote nchini, kila mahali, kutoka kaskazini, kusini, magharibi, waliokuja kwa ajili ya mahojiano haya. Basi mara tu wangemaliza kuzungumza, maswali hasa ambayo wangeuliza, jambo ambalo wangeulizia, ningesema, “Tazama hapa,” nikiinua juu, na palikuwapo na kipande cha karatasi pamoja na kila swali, na kukizungusha jinsi hasa walivyoliulizia, walivyokuwa wanaenda kuliuliza, jibu lao hapa chini kwa swali lao, jinsi tu lilivyojibiwa. Bwana ni mkuu. Anajua mambo yote. Lakini, hata hivyo, inichukue kama siku tatu kutoka kwenye alasiri hiyo, jambo ni kwamba, ilinichosha sana. Na sasa nilifikiria kulipata, hata hivyo, kabla hatujaondoka.

⁶³ Na kuna njia sahihi, njia halisi ya, kwa watu binafsi. Sasa, kuna mambo yanayoweza kusemwa.

⁶⁴ Na iwapo hao watu wako hapa, wanaojua kwamba siri za mioyo zilizofunuliwa, ambazo kabisa zingeninii. . . Linge kuwa jambo la kutisha sana; lingesababisha uhalifu, lingesababisha mtu kumpiga risasi mwenzake, ama chochote kile, kama hayo yangefunuliwa papa hapa jukwaani namna hii, hadharani, humu mbele ya hadhara. Ingesababisha hatia za kifungo, na kadhalika, ambazo zingeninii. . .

⁶⁵ Lakini mnapoketi pamoja namna hiyo, Roho Mtakatifu, ninyi wawili peke yenu pamoja. Lakini tunaelewa hili, kwamba wanachoniuliza ni cha faraghani. Sisemi lolote kukihusu. Na yale ninayowaambia, ni juu yao ikiwa wanataka kuyasema au la. Mnaona? Lakini yanapaswa kujulikana kati yetu, kwenye mahojiano. Hiyo ni kumchukua mtu huyo, mmoja kwa wakati mmoja, na kuketi pale mpaka kila kitu kimetatuliwa kabisa, mnaona, Roho Mtakatifu.

⁶⁶ Na kisha kuwazia juu ya neema, Roho Mtakatifu akiniambia yote kuyahusu, kwa kila mmoja, mlolongo mzima wa hao, kabla hata hawajafika hapa; kote nchini, wakija, watu ambao sijawahi kuwaona maishani. Na kuyaandika wapate kujua, utaratibu tu kulingana na maswali jinsi wangeninii, kuyajibu.

⁶⁷ Ndugu mmoja alikuwa na maswali juu ya uzao wa nyoka, ambayo sikuweza kuyajibu vizuri kabisa, maana maskini nusu saa yao ilikuwa imeisha. Natumaini ya kwamba alilipata vema, majibu yake, kwenye karatasi. Mimi. . . Alikuwa ameliandika, wala hakupata majibu yake yote, kwa hivyo nilimpa tu hayo maandishi tena, majibu kwenye karatasi. Kama hajaipata, Billy Paul anayo. Najua huyo mtu ameketi hapa; nilimwona muda mfupi tu uliopita. Kwa hiyo kama yeye—kama anataka kupata hayo, yameandikwa kwenye kipande cha karatasi, majibu yako ya swali lako.

⁶⁸ Sasa, loo, jinsi Bwana alivyo mwema! Natumaini kila mtu anajisikia vizuri. Uh-huh.

⁶⁹ Na sasa hebu na tukumbuke, na sasa ninapoombea lesi hizi, kumkumbuka Ndugu Dauch. Yeye ni ndugu wa thamani, nasi tunataka kumkumbuka katika maombi.

⁷⁰ Nami na—namwona Ndugu Ungren, bali si—siwezi kumuona Dada Ungren popote, iwapo yuko sawa sasa. Naam, ameketi papo hapo karibu naye. Hakika. Naam. Nina furaha. Maana tuliitwa hivi majuzi usiku, katika. . . wito tu wa dharura wake yeye na binti yake, Dada. . . mimi. . . Downing, Downing. Wakaondoka barabarani, na ni neema tu ya Mungu, la sivyo wote wawili wangevunjwa vipande-vipande papo hapo. Nao hawa hapa wanakuja moja kwa moja kanisani, wakapanda garimoshi wakaja.

⁷¹ Kamwe sitawasahau ninyi nyote. Nawapenda. Mungu anajua hilo. Na—nawapenda. Jinsi, kote nchini, kupitia hali telezi ya hewa!

⁷² Ninapomwangalia ndugu fulani hapa kutoka Georgia, na Alabama, na sehemu mbalimbali, na Tennessee, na kote, ambapo wanaendesha gari lao barabarani, ambapo barafu, kuteleza, na kwenda huku na huku namna hiyo, wapate kuja hapa kwa ajili ya ibada moja.

⁷³ Nilipopata simu hiyo ya dharura kwa Ndugu Dauch hivi majuzi, sikutambua kwamba Lima, Ohio, ilikuwa mbali sana. Ninii... nilifikiri hiyo ilikuwa ni kuchupa kidogo, kupiga hatua na kuruka. Lakini, jamani, niliondoka hapa mapema sana asubuhi hiyo, sikufika huko hadi saa saba alasiri hiyo, nikiendesha cho—chochote kikomo rasmi cha spidi kingeruhusu, na kwenye barabara kuu yenye njia mbili. Nami nawazia jinsi hiyo ilivyo karibu, na huko mbali sana Kusini ambako hawa watu wengine wanatoka, huko mbali Kaskazini na Magharibi, ambako wanatoka.

⁷⁴ Ninawapenda, na hiyo ndiyo sababu ninajaribu kuwa mwaminifu kabisa hapa.

⁷⁵ Na wazee wa zamani! Ninamwona Ndugu Creech na hao wengine wameketi huko nyuma sasa, na wale ambao wamekuwa pamoja nami miaka hii yote na kadhalika, na jinsi tumetembea pamoja. Nilikuwa nikiitazama picha ya Mary Jo, naamini ilikuwa siku kadhaa zilizopita usiku. Maskini mtu mdogo tu tulipokutana mara ya kwanza, na sasa ameolewa, nadhani, naye ana watoto. Ndugu Creech na Dada Creech, vijana, wenye nywele nyeusi, nami pamoja na Meda, na sisi hapa wenye mvi na tumeinama. Mnaona, kuna jambo fulani kuhusu watu kama hao, li—linalokushika imara. Unaona, u—u—unataka kukaa pamoja nao. Unaona? Kuna jambo moja ama lingine ambalo—ambalo sikuzote hufanya akili yako kurudi nyuma. Ninawatoa tu kama mifano kwa wengine waliopo hapa. Vijana kwa wazee, tunakutazamia Kuja kwa Bwana.

⁷⁶ Kwa hivyo asubuhi ya leo nimeliweka... Mungu, naamini, aliliweka moyoni mwangu kufundisha somo la shule ya Jumapili hapa asubuhi ya leo, Mungu akipenda, kwa muda mrefu. Mimi... Na sasa, hii ikiwa ndiyo ibada yangu ya mwisho kwa kitambo kidogo, kadiri nijuavyo, ninii...

⁷⁷ Nami ninawatakeni mkumbuke ya kwamba Ndugu Neville hapa, ameachwa kanisani, kuisimamia maskani hii, chini ya Roho Mtakatifu, kwamba ameachwa hapa, naye anaamini Ujumbe huu na—na kuufundisha sawasawa na mimi. Kweli. Na wakati wowote unapotaka, unapoweza kuona inafaa kuja kumsikiliza Ndugu Neville, hakika atakutendea mema, nina hakika. Yeye ni mtumishi mkuu wa Yesu Kristo.

⁷⁸ Nimemjua Orman Neville tangu nilipokuwa mvulana mdogo, naye hajabadilika hata chembe moja, ila amemkaribia Mungu zaidi. Nakumbuka nilipomwona kwa mara ya kwanza kwenye ninii. . . Nilialikwa kwenye jukwaa lake la Methodisti. Ndipo niliporudi hapa maskanini, nilisema, “Siku moja, nitambatiza katika Jina la Yesu Kristo.” Naye huyu hapa pamoja na Ujumbe sasa, akiendelea, mtumishi hodari kweli.

⁷⁹ Naye Ndugu Neville anapitia matatizo mengi na machungu, ambayo hayaonyeshi hapa maskanini. Lakini kwa kuwa Bwana hunijalia kuangalia kidogo katika maisha ya watu, najua anayopitia; mengi sana, mnaona. Naye bila shaka anapitia kwenye kazi nyingi na uchovu wa akili, na kadhalika. Na nyinyi, nyinyi watu hapa, mshikilieni kama Yoshua na Kalebu walivyoiinua mikono ya Musa, anapolileta Neno.

⁸⁰ Pendaneni, zaidi ya yote. Pendaneni. Msininii. . . Haidhuru ibilisi anajaribu kusema nini! Sasa ninyi nyote ni kundi moja kubwa tamu sasa, lakini kumbukeni onyo langu, mnaona, Shetani hataliacha hilo lidumu hivyo. Hapana, bwana. Atawarushia kila kitu, ikimbidi kuleta mtu fulani ili kupata lengo lake. Atamleta mkosoaji au asiyeamini, na kumketisha chini, na kumfanya ashirikiane nanyi chini ya utulivu na kadhalika, halafu basi atamtia jamaa huyo namna fulani ya sumu, naye ataisambaza kote kanisani. Msichukue upande nayo. Kamwe msijihusishe na kitu chochote kingine. Dumuni moja kwa moja mkipendana na utamu na wema ninyi kwa ninyi. Mwombeeni mwanamume huyo, kwamba ataokoka pia, ama mwanamke huyo, ama yeyote yule, waombeeni tu. Na mshikamane.

⁸¹ Na mkae na mchungaji wenu. Mnaona, yeye ndiye mchungaji, basi mpeni heshima. Atawaongoza vizuri, na, kwa kuwa ameteuliwa na Mungu kufanya hivyo.

⁸² Sasa mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Adui atakuja. Basi ajapo, shikamaneni tu hivyo kwa karibu zaidi. Ndipo yule ambaye ibilisi anamtumia kama adui ama atatoka au aingie na kuwa mmoja wenu. Hivyo tu.

⁸³ Kamwe msiingize matabaka miongoni mweni. . . au—au maongezi, kujigawa kitabaka. Sisi ni kitu kimoja. Nisingeweza kusema, “Mkono wa kushoto, u—umeniudhi mno, nitakuondosha kwa maana wewe si mkono wa kulia.” Yeye ni mkono wangu wa kushoto. Namtaka akae hapo. Hata ncha ndogo ya kidole changu, nataka ikae papo hapo, kila sehemu ndogo ya mwili wangu ikae papo hapo. Naye Mungu anatutaka sisi, kama mwili wa waaminio, kukaa kabisa mmoja na mwenzake, mmoja na mwenzake hasa.

⁸⁴ Na sasa mna kanda kuhusu hilo. Mna kanda za yale tunayoamini. Mna kanda juu ya nidhamu kanisani, jinsi tunavyojiendesha katika kanisa la Mungu, jinsi inavyotupasa

kuja hapa pamoja na kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni. Usikae nyumbani. Ikiwa Mungu yuko moyoni mwako, ni vigumu kwako kungojea milango hiyo ifunguliwe huko nje, kuingia humu ukashirikiane na ndugu zako. Kama hu—hujisikii hivyo, basi nakwambia, ni wakati unapaswa kuomba.

⁸⁵ Maana, tuko katika siku za mwisho, ambapo Biblia ilituina, ama, ilituhimiza ili—ili, “Kwa kadiri tuonavyo siku ile ikikaribia,” kupendana kwa upendo wa Kikristo na upendo wa Kiungu, “kukusanyika pamoja mahali pa Mbinguni na—na—na Kristo Yesu,” na kupendana. “Hivi watu wote watatambua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.” Hiyo ni kweli. Kaeni moja kwa moja pamoja.

⁸⁶ Kama huyo ndugu, ukifikiri amekosea kidogo, ama huyo dada, sema, “Bwana, usiniache kamwe nipate kuchipukiwa na shina la uchungu, kwa sababu lita—litamwathiri, na litamtoa Kristo moja kwa moja kutoka maishani mwangu.” Hiyo asidi ya sumu ya chuki, na wivu, na kinyongo, hiyo itamwondoa tu Roho Mtakatifu kutoka kwako. Itamwondosha hapa maskanini. Itamwua Roho wa Mungu, ama kumfukuza kutoka hapa, imdhuru mchungaji wenu. Itafanya kila kitu. Mnaona? Msifanye hivyo.

⁸⁷ Ninyi shikamaneni tu pamoja kwa karibu hivyo. Vuteni . . . Chukua bizimu, kama ndugu alivyoshuhudia, mhudumu hapa hivi majuzi usiku, juu ya kuwa na bizimu, kuiona katika ono. Kuninii tu, inayofunga silaha zote za Mungu. Ivute tu, ikaze, sogeaneni karibu mmoja na mwenzake. Pendaneni, kwa vyovyote vile. Neneaneni mema, semeaneni mema nyinyi kwa nyinyi, na ndipo basi Mungu atawabariki.

⁸⁸ Sasa asubuhi ya leo, Bwana akipenda, kwa msaada Wake na neema, nina maswali kadhaa hapa, ya Maandiko, hasa. Na sasa kabla hatujalikaribia . . . Nafikiri nilisikia vinasu sauti vikibonyezwa mle ndani. Tutaleta Ujumbe sasa, kwa neema ya Mungu.

Kwanza, maombi mafupi.

⁸⁹ Bwana Yesu, nikizungumza na mwili huu wa Kanisa, kwamba imewapasa kushikana pamoja na mkono wa Mungu usiobadilika, Yakini yao, Neno; nikiwaonya, kama Paulo alivyolionya kundi lake, kwamba, “kutakuwa na mbwa mwitu watakaoingia.” Wewe ni Mungu yeye yule leo kama ulivyokuwa wakati huo, naye adui huyo ni yule yule. Jalia ushirika huu na vifungo vya upendo viwepo daima kati ya watu hawa, katika Kristo Yesu.

⁹⁰ Tusaidie, asubuhi ya leo, Bwana, tunapolisoma Neno. Roho Mtakatifu na atufunulie Hilo, ili Kanisa liweze kuimarishwa kikamilifu katika “Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu,” kuwashikilia. Na jalia, kama ulivyotoa ono miaka miwili iliyopita, “kuweka Chakula akiba,” mboga nzuri zenye

afya nilizoziona katika ono, zikihifadhiwa hapa katika maskani hii, jalia sisi leo tupokee pipa zima lililojaa Hizo (Tujalie, Bwana.), ama, mzigo wa kanda: ili ipate kutufunulia Yesu Kristo katika saa tunayoishi, ili kutupa nguvu za kutuendeleza, nguvu za kiroho kwa ajili ya kazi iliyo mbele yetu. Tujalie, Baba.

⁹¹ Wabariki hawa, watoto Wako. Wako hapa ndani asubuhi ya leo kutoka sehemu nyingi mbalimbali za taifa. Asubuhi yenye joto, inayonata, lakini hata hivyo tunahisi Uwepo wa Roho Mtakatifu, katika haya yote.

⁹² Tunawazia juu ya John Wesley, na Calvin, na Sankey, na Knox, Finney, na wengi wa hao, hata bila feni ya umeme, ambapo watu waliketi kwenye kumbi, na jasho likitiririka nyusoni mwao. Wanawake, wakiwa wamejifunika vizuri na wamevaa vizuri, waliketi kwenye kusanyiko na kutokwa na jasho mpaka mavazi yao yalikuwa yamelowa maji, wakisikiliza Neno la Mungu, wakizilisha nafsi zao. Sasa, tunajisikia, Bwana, ya kwamba wamepumzika mahali fulani huko ng'ambo, wakikungojea Kuja kwa Bwana.

⁹³ Tuweke pamoja, Baba. Hebu Roho Mtakatifu atuongoze na kutuelekeza. Tupe maisha marefu ya utumishi kwa ajili Yako. Tupe Ujumbe huu mkuu asubuhi ya leo tunaoutarajia kutoka katika Neno Lako, upate kwenda kwa kila moyo. Ifanye midomo inayonena, Bwana, inene Kweli. Ufanye moyo unaosikia uwe na rutuba ya kuipokea Kweli, pia jalia ikue iwe miti mikuu ya Uzima wa Milele, iwe mianga ing'aayo na nyaraka zinazosomwa na watu wote; wapate kujua kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu na anaishi miongoni mwetu. Utufanye tujazwe sana na upendo na tunda la Roho mpaka wanaume na wanawake wengine, wavulana kwa wasichana waweze kuona matokeo ya Uhai wa Kristo yangali yanaishi ndani yetu, baada ya miaka elfu mbili kutoka kwenye lile tukio kuu. Lijalie, Baba, kukuhesimu Wewe. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁹⁴ Sasa nataka kusoma kidogo kutoka kwenye Maandiko. Nami ninatumaini sasa ya kwamba mmeweka tayari penseli zenu na karatasi, na kila kitu.

⁹⁵ Na, Ndugu Neville, umeketi kimya. Nitavua tu koti langu. Hiyo ni... [Ndugu Neville anasema, "Hilo ni sawa. Amina."—Mh.] Ni ninii... Samahani kwa kuvua koti langu, lakini hapa—hapa pana joto sana.

⁹⁶ Sasa ninawatakeni mfungue Kitabu cha Wakolosai, mlango wa kwanza wa Wakolosai. Ndipo tunaposoma hili, kuanzia na... Nawatakeni ninyi, mtakaporudi nyumbani, msome sura nzima ya hawa Wakolosai. Lakini nataka msome asubuhi ya leo, pamoja nami, kutoka kifungu cha 15, 29, vyote pamoja.

⁹⁷ Na sasa iweni tu na subira mwezavyo, kwa maana ninahisi ya kwamba katika hili hapa, kama Mungu atanisaidia, litafunua na kukuletea akilini mambo haya mengine yote ambayo

nimeyazungumzia siku zote za maskani hii; kwa nini nimesema niliyosema, na ni kwa nini nimefanya yale nimefanya. Hii hapa sababu yake.

⁹⁸ Sasa kuanzia kifungu cha 15.

Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote:

Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana... visivyoonekana, ikiwa ni viti vya enzi, ... usultani, ... enzi, ... mamlaka: vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake:

Naye amekuweko kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.

Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa: naye ni mwanzo, mzaliwa wa kwanza katika wafu; ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza Baba utimilifu ulikaa—utimilifu wote ukae;

⁹⁹ Hebu niweke mkazo kidogo juu ya hilo tena, kifungu hiki cha 19.

Kwa maana ilimpendeza Baba kwamba ndani yake utimilifu wote ukae;

Na, kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, nasema, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.

Tazama ambako upatanisho huo ulienda.

Na ninyi, mliokuwa wakati mmoja mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa

Katika mwili wa nyama yake kwa kufa kwake, ili awalete ninyi watakatifu... wasio na lawama... mmekubalika machoni pake:

Mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa msingi mkawa imara, msipogeuzwa na kuliacha tumaini la injili, mliosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nafanywa mhudumu wake;

Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza mafungo... yale yaliyopungua ya upendo wa Kristo, katika... mwili wake, yaani kanisa:

Ambayo nalifanywa kuwa mhudumu wake, kwa utaratibu wa Mungu niliopewa kwa faida yenu, nilitimiza neno la Mungu;

Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, lakini sasa imedhihirishwa kwa watakatifu wake:

100 Na ninataka kusoma kifungu hicho tena.

Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, lakini sasa imedhihirishwa kwa watakatifu wake:

Ambao Mungu alipenda kuwajulisha ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii kati ya Mataifa; nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu:

Ambaye sisi tunamhubiri, tukimwonya kila mtu na kumfundisha kila mtu katika hekima yote; tupate kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo Yesu:

Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu.

101 Sasa kwa ajili ya somo nataka kuchukua kutoka hapo, hili kwa ajili ya somo, nikiliwekea msingi juu ya Biblia nzima, lakini nataka tuliite hili: *Kristo Ni Siri Ya Mungu Iliyofunuliwa*. Kristo akiwa ni siri ya Mungu iliyofunuliwa! Sasa, nililichukua kwa utaratibu kama somo la shule ya Jumapili, ili sote tuweze kusoma pamoja na—na kuwa na ushirika huu pamoja.

102 Sasa, siri ya Mungu ya fumbo, Yeye alikuwa nayo kabla ya ulimwengu kuanza. Sasa, huko nyuma katika sehemu ya nyuma ya akili ya Mungu, kulikuwa na jambo fulani ambalo Yeye alikuwa akijaribu na alikuwa anaenda kulitimiza, Naye alikuwa na kusudi la kufanya jambo hilo, kusudi aweze kujidhihirisha Mwenyewe. Kwa sababu, kwanza, hapakuwapo hata na mwezi, nyota, atomu, molekuli, wala chochote kile. Yeye alikuwa ni Mungu. Lakini Yeye hasa hakuwa Mungu wakati huo, kwa maana *Mungu* ni “kitu cha kuabudiwa,” wala hapakuwa na kitu cha kumwabudu Yeye.

103 Kwa hiyo, katika akili Yake kuu, alitaka sifa hizi zidhihirishwe. Na ndani Yake mlikuwamo upendo; ndani Yake mlikuwa kuwa Baba; ndani Yake mlikuwa kuwa Mwana; ndani Yake mlikuwa kuwa Mwokozi; ndani Yake mlikuwa kuwa Mponyaji. Na sifa hizi zote kuu tunazoziona zimedhihirishwa tayari, zilikuwa ndani ya Mungu.

104 Kwa hiyo, maoni yangu, kitu cha kwanza alichoumba kilikuwa ni Malaika. Ndipo wakamwabudu, na hilo likamfanya “Mungu.” Ndipo akaanza kutoka hapo. Kama vile katika Jumbe zilizotangulia nimejaribu kulielezea, kulifafanua. Na sasa, basi, wakati Malaika walipoanza kumwabudu, hiyo ilikuwa kabla hata hakujakuweko na molekuli duniani. Hakukuwa na chochote. Yote ilikuwa giza. Hakukuwa na jua, wala mwezi, hakuna nyota, hakuna chochote, basi Yeye alikuwa Mungu. Kama vile alivyomwuliza Ayubu, “Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya ulimwengu, mnaona, hapo nyota za

asubuhi zilipoimba pamoja, wana wa Mungu wakapaza sauti kwa furaha? Mnaona? Sasa, ulikuwa wapi?” Mnaona? Hiyo ilikuwa huko nyuma kabisa kabla ya dunia.

¹⁰⁵ Sasa, Mungu alikuwa na kusudi na siri iliyofichwa. Na hiyo ndiyo ninayotaka kulizungumzia Kanisa asubuhi ya leo, siri ya Mungu iliyofichika aliyokuwa nayo niani mwake kabla ya ulimwengu kuwako, na jinsi imejifunua yenyewe moja kwa moja hadi kufikia saa hii tunayoishi. Mnaona? Ndipo mtaelewa dhahiri basi, mnaona, juu ya, naamini, kile kinachofanywa.

¹⁰⁶ Siri kuu ya Mungu, ya jinsi ambavyo, ni siri. Aliiweka siri. Hakuna mtu aliyejua lolote kuhusu. Hata Malaika hawakuielewa. Mnaona, hakuifunua. Hiyo ndiyo sababu, chini ya siri yetu ya saba, wakati Muhuri wa Saba ulipofunuliwa, kulikuwa na kimya. Yesu, alipokuwa duniani, walitaka kujua ni lini angekuja. Akasema, “Sio...Hata Mwana Mwenyewe hajui itatokea lini.” Mnaona, Mungu anayo haya yote kwake Mwenyewe. Ni siri. Na hiyo ndiyo sababu kulikuwa na kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa, nazo ngurumo saba zikatoa sauti zao, na Yohana hata alikatazwa kuyaandika, mnaona, kule Kuja kwa Bwana. Hilo ni jambo moja ambalo bado hajalifunua, jinsi atakavyokuja, na wakati atakapokuja. Ni jambo jema kwamba halifunui. La.

¹⁰⁷ Ameonyesha au amelifunua katika kila mfano ulio katika Biblia. Kwa hiyo, Biblia nzima ni ufunuo wa siri ya Mungu katika Kristo. Hum! Biblia nzima ni dhihirisho la lengo moja ambalo Mungu alikuwa nalo, kusudi moja alilotaka kufanikisha katika Biblia nzima. Na matendo yote ya—ya waaminio katika Biblia yamekuwa katika mfano, kuonyesha lililo lengo kuu la Mungu, na sasa katika siku hii ya mwisho Yeye amelifunua na analionyesha. Na msaada wa Mungu, tutalionga papa hapa asubuhi ya leo, kile Bwana amekuwa nacho mawazoni Mwake wakati wote, na amekidhihirisha.

¹⁰⁸ Kwa hiyo, mnaweza kuona maana kuu ya jinsi imekuwa kujua jambo hili, na kisha ujaribu kulileta kwa watu. Mnaona? Na kisha huninii. . .Sijaingia katika utondoti kujaribu kulielezea kama vile Mungu alivyonifunulia.

¹⁰⁹ Sasa, kama ukitaka kuandika hili. Nina mahali pengi sana ninapotaka kusoma. Na sasa katika—katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 24 wa Luka Mtakatifu, tunaona ni... Ni wale wanafunzi wawili waliokuwa wakienda zao Emau. Naye Yesu akatokea, baada ya kufufuka Kwake, nao walikuwa wakienda za—zao Emau, wakitembea njiani, wakiwazia na kuongea, na kulia, kwa sababu ya kifo Cha—Chake, na jinsi walivyomwona akiteseka kwa kile walichokidhanja hakikuwa na manufaa yoyote; walimchukua Bwana wao wakamsulubisha. Na—nao walikuwa wakienda huko, wakilia.

¹¹⁰ Naye akatokea kando ya njia akaanza kuzungumza nao juu ya Kristo. Akasema, “Loo, enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito kuelewa. Je, hamjui kwamba manabii wote na Zaburi . . .” Mnaona, alikuwa akifanya nini? Akijitambulisha Mwenyewe kwa mitume hawa, ya kwamba manabii wote, na Zaburi zote, na kila kitu, kilikuwa ni Yeye, akidhihirishwa. Mnaona?

¹¹¹ Na sasa sababu sikuchukua kuhubiri asubuhi ya leo, ilikuwa ni kwamba, nilifikiri, katika kufundisha, tungelielewa vizuri zaidi kuliko kuchukua somo na kulipitia juu juu. Tungelifundisha tu.

¹¹² Sasa, Yeye alikuwa akisema ya kwamba Zaburi zote na manabii wote walinena juu Yake. Vema, hapo, kwa hiyo, hiyo inaonyesha kwamba Agano la Kale lote, Agano Jipya lote, na Zaburi zote, uimbaji, zile nyimbo zilizoimbwa, ziliimbwa kumhusu Yeye.

¹¹³ Chukua Zaburi ya 22, na uiimbe, kisha uilinganishe na ile asubuhi ya kusulubiwa. Unaona, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote, inanikodolea macho. Waliichoma miguu Yangu na mikono Yangu.” Hata hivyo, mambo hayo yote pale, hao wakiimba hiyo Zaburi kule chini hekaluni, huku wakimsulubisha Yule hasa. Mnaona? Mnaona, hao viongozi wakuu wa kidini, hao watu mashuhuri, hao waalimu wakuu, na hata hivyo wamepofushwa sana, ambao walikuwa wakiwasoma manabii na walikuwa wakiimba nyimbo, na kufanya uhalifu ambao walisema wangefanya.

Jambo lile lile linafanyika asubuhi ya leo!

¹¹⁴ Sasa sikilizeni kwa makini, maana . . . Sasa hata sitatilia maanani kile ambacho saa hiyo inasema. Nataka mpate hili. Mnaona? Nawatakeni, mlipate. Mnaona? [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.]

¹¹⁵ Kwa hivyo mnaweza kuona hapa, kimsingi, mwanzoni, wazo lenyewe ambalo Mungu alikuwa nalo akilini Mwake, alilificha kwa hao wasomi wote. Na . . . Idadi tu, idadi iliyochaguliwa tangu zamani, watu waliochaguliwa tangu zamani, ndio pekee walioisikia. Na sasa yachunguzeni tena Maandiko kote katika wakati wa manabii, muone kama halikuwa jambo lile lile. Mnaona?

¹¹⁶ Sasa, naye Yesu hapa akiwarejesha kwa manabii na Zaburi, Yeye alisema wote walinena habari Zake. Mnaona? Na hapa waalimu hawa wa Kiyahudi, marabi, madaktari wa torati, maprofesa, walikuwa wamefanya hasa kama walivyokuwa wamefanya hapo awali.

¹¹⁷ Sasa angalieni, tena, Yeye alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa maana Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Yachunguzeni Maandiko, Maandiko, Maandiko yote. Je, ninajaribu kufanya nini? Kuwaonyesha kwamba Biblia hii ndicho kitu kilicho sahihi.

118 Hivi majuzi, nikiwa nimesimama katika chumba cha hospitali, nikizungumza, dada mmoja alikuwa ameniomba nielezee kuhusu madhehebu, kwa nini tu—tuliyapinga madhehebu, pamoja na baadhi ya watu wa kimadhehebu.

119 Mnaona, haina budi kurudi kwenye Neno, kwa maana Neno ni Mungu. Mnaona? Naye Yesu akitangaza jambo lile lile hapa, ya kwamba Neno ni Yeye. Huwezi kuyafanya Maandiko kujipinga Yenyewe. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye, Neno, alifanyika mwili!” Mnaona?

120 Sasa hapa Yeye anasema, “Yachunguzeni Maandiko, Yananishuhudia Mimi. Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele,” na hiyo ni kweli, “na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Nami ninayashuhudia. Na nisipozitenda kazi zilizoahidiwa ya kwamba ningezifanya, basi msinisikie Mimi. Lakini nikizitenda zile kazi, nanyi hamwezi kuniamini, aminini hizo kazi, kwa sababu zinashuhudia ya kwamba Yeye ni Neno.” Loo, inaonekana kama isingeweza kuwa wazi zaidi. Mnaona? Vema. Sasa, “Yachunguzeni Maandiko.” Yeye alisema Musa na torati zote, na kadhalika, na manabii, na Zaburi, walinena habari Zake. Na, tena, Yeye alisema Maandiko yanamshuhudia.

121 Yeye ndiye kiini kikuu cha Biblia nzima. Ukisoma Biblia, wala usimwone Kristo katika kila kifungu Chake, rudi ukaisome tena. Unaona? Kama huwezi kumwona Kristo katika kila kifungu cha Biblia, basi isome tena, kwa maana ulikosa kitu fulani. Biblia ni Kristo. Yeye ni Neno. Unaposoma, “Hapo mwanzo Mungu aliumba,” huyo hapo Kristo. Unaona? Kila... Kuanzia hapo, mpaka ile “Amina” katika Ufunuo, ni kila Neno likimshuhudia Yesu Kristo.

122 Hiyo ndiyo sababu vitabu hivi vilivyoongezwa ambavyo wanaviita *Kitabu cha Pili cha Danieli*, na—na *Kitabu cha Wamakabayo*, huongezea toharani na upuuzi kama huo, mnaona, haijanenwa katika Maandiko. Mnaona? Haishirikiani na mengine Yake. Hakuna nafasi ya kuweka toharani humo. Hakuna nafasi ya kuweka maombezi ya watakatifu, na kadhalika. Hakuna nafasi ya hayo humo ndani. Hakuna nafasi ya dhehebu. Hakuna nafasi ya—ya kanuni za imani nje ya—ya Biblia. Mnaona? Kwa hiyo mnapoona mambo hayo, ha—hayatambulikani kabisa. Na hiyo ndiyo sababu watu wameviongezea hivyo, na kuvuruga mchezo-fumbo wa—wa—wao kabisa. Mnaona? Hawawezi kuifanya sahihi, “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

123 Lakini, kama kitu hicho kikiwekwa pamoja vizuri, hiyo hapo picha nzima ya kule kuanguka na kuzaliwa upya. Picha nzima ya uumbaji, na mpango wote wa Mungu ulifunuliwa mumo humo katika Yesu Kristo. Amina! Hiyo ndiyo picha nzima iliyowekwa pamoja, kila mpindiko mdogo na kona. Ni kama tu... Sasa,

simaanishi kukufuru kwa jambo hili, lakini ni kama tu kuweka mchezo-fumbo pamoja.

¹²⁴ Hiyo ndiyo sababu tunazo picha siku hizi zinazoonekana za kutisha. Wanasema, “Sisi ni waaminio,” huku ng’ombe akila nyasi juu ya mti. Haina maana. Hapo ndipo wanaposema, “Naam, Yeye yuko kila njia, lakini ninii fulani tu . . . Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, yote isipokuwa jambo fulani.” Unaona? Ndipo basi unaharibu picha yako.

¹²⁵ Biblia ilisema Yeye ni yule yule! Yohana Mtakatifu 5, ama Yohana Mtakatifu 14:12, Yeye alisema, “Yeye,” yeye, mtu yeyote, “yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

“Vema, hiyo ilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine.”

¹²⁶ Hapo umeiharibu picha yako tena. Una mtu anayevua samaki huko jangwani, akiwatafuta samaki, kwenye lundo la mchanga wenye joto ambapo hakuna samaki. Unaona? Unaona, huna budi kumrudisha mahali anapovua samaki, huko Galilaya, ambako kuna samaki wengi, unaona. Unaona?

¹²⁷ U—unapaswa kuifanya hiyo picha ione kane sawa. Ni picha kuu ya Mungu. Na kuna njia moja tu utakayoiona, hiyo ni hapo utakapomwona Yesu Kristo. Hiyo hapo Biblia nzima. Yeye ndiye kiini kikuu cha Biblia.

¹²⁸ Sasa unatambua kuwa sehemu yoyote kati ya hizi hapa ungeweza kuchukua somo, na ni vigumu tu kwa mhubiri kutulia. Anaonekana kana kwamba anataka kuendelea nalo, lakini huna budi kurudi kwenye kile tunachofundisha.

¹²⁹ Yeye ndiye kiini kikuu cha Biblia. Alikuwa katika manabii. Alikuwa katika Zaburi. Alikuwa katika historia ya Biblia. Biblia ni Kitabu cha unabii. Ni Kitabu cha historia. Ni Kitabu cha upendo. Ni Kitabu cha—cha nyimbo. Ni Kitabu cha Uzima. Na hapo ndani unampata Kristo. Alikuwa katika manabii. Alikuwa katika Zaburi. Alikuwa katika historia. Naye pia, katika Biblia, ndiye mambo yajayo. Kwa hiyo, alikuweko kabla na hata baadaye. Hiyo inamfanya nini basi? “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹³⁰ Nawe ukiingiza kitu Mle ndani, ambacho hakimfanyi Yeye “yule yule jana, leo na hata milele,” Ndugu Lee, unaenda wapi? Una picha mbaya sana hapo. Kwa maana, Yeye alikuwa ndiye historia, unaona, na Yeye ni Nabii. Yeye ni Zaburi. Yeye ni kila kitu. Na kama huwezi kumfanya kila kitu, na yeye yule, wapi, picha yako inaonekanaje? Mnaiona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

¹³¹ Yeye ndiye kitu chenyewe! Alikuwa ndiye manabii. Alikuwa ndani yao. Alikuwa katika Zaburi. Alikuwa katika historia, na Yeye ndiye mambo yajayo, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Waebrania 13:8, kama unaiandika. Anapaswa kuwa,

basi, Yeye anapaswa kuwa ndiye kiini, kama hivyo ndivyo alivyo. Nasi tunaamini hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, ikiwa Yeye yuko hivyo, basi anapaswa kuwa ndiye kiini kikuu cha mazungumzo yetu, cha mawazo yetu, cha kuimba kwetu, cha matembezi yetu. [“Amina.”] Anapaswa kuwa kiini kikuu cha maisha yetu. Kama Yeye ndiye kiini kikuu cha Biblia, nayo Biblia iko ndani yetu, basi anapaswa kuwa ndiye kiini kikuu cha kila kitu tunachofanya, tunachosema, au kuwazia; kinapaswa kuwa ni Kristo. Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Vema.

¹³² Kwa kuwa, tunawazia hivi, kwa kuwa amefanywa—amefanywa Kichwa cha “mambo yote,” kwetu. Wakolosai ilisema hivyo hapa. Yeye ndiye Kichwa cha “mambo yote,” kwetu. Kwa kuwa alifanywa...kwa ajili yetu, ambao tunafikiriwa “mambo yote.” Mnasema, “Na mwenye dhambi je?” Yeye alifanywa kuwa Hakimu wa mwenye dhambi kama hatalikubali. Alifanywa kuwa utukufu kwa ajili ya mwaminio anayelikubali. Kwa hiyo hapo, jambo, “vitu vyote viliumbwa na Yeye, na kwa ajili Yake.”

¹³³ Na inahitaji usiku, kuonyesha utukufu wa mchana. Inahitaji chombo cha aibu, kudhihirisha u—upendo na utunzaji wa chombo cha heshima. Inahitaji mwanamke mwovu, ambaye angevaa nguo za kizinifu na—na kuuza maadili yake, kudhihirisha maadili ya mwanamke mzuri wa kweli. Mnaona? Inahitaji jambazi na mwizi, ndani ya mtu, kuonyesha ukweli wa mwaminio halisi, Mkristo halisi. Inahitaji mnafiki, kuonyesha mwaminio, kile alichu.

¹³⁴ Kwa hiyo, “Vitu vyote viliumbwa na Yeye.” Na kwa kuwa alifanywa mambo yote...alifanywa, kwa ajili yetu sote, vitu vyote viliumbwa kwa ajili ya, kupitia Yeye. Basi, kwa kuwa hiyo ni kweli, tunapaswa kufanya utambulisho wetu (unapaswa kuwa) pamoja Naye. Tunapaswa kutambulishwa, sisi wenyewe, pamoja Naye, kwa sababu Yeye amejitambulisha Mwenyewe pamoja nasi. Tunapaswa kutambulishwa pamoja Naye. Vipi? Kwa kumwishia Yeye; si kuungama tu.

¹³⁵ Watu wengi sana huchukua maungamo, wanasema... Ninasema imefikia mahali hapa sasa. Je, wewe ni Mkristo? “Mimi ni Mmethodisti.” Vema, hiyo ni mbali sana na kuwa, kujitambulisha kama Mkristo. Vema, angalia vile Wamethodisti hufanya. “Mimi ni Mbaptisti.” Vema, angalia vile Wabaptisti hufanya. “Mimi ni Mkatoliki.” Angalia wanachofanya. Unaona?

¹³⁶ Lakini njia pekee ambayo unaweza kweli kuwa Mkristo ni Kristo kujitambulisha Mwenyewe ndani yako. Jinsi tulivyo na, mwiba hapo! Natumaini kila mtu kwenye kanda atapata hilo, pia. Mnaona? Mnaona? Mnaona?

Unasema, “Mimi ni Mpentekoste.” Hiyo haimaanishi chochote.

137 Ni Kristo akitambulishwa ndani yako. Hapo ni wakati Yeye amekutambua.

Wasema, “Nilinena kwa lugha.” Mashetani hufanya hivyo, pia.

138 “Nilipaza sauti.” Waislamu, Mabudha, na kila kitu hupaza sauti. Wahindi hupiga mayowe kwenye ngoma za nyoka. Mnaona? Hakika. Wote hufanya hivyo. Madhehebu, makabila, na chochote kile, hupiga mayowe na kupiga makelele. Wanapiga mayowe na kupaza sauti kwenye mchezo wa besiboli.

139 Lakini Kristo anapotambulishwa ndani yako, akijitambulisha Mwenyewe, basi wewe ni kama Kristo. Ambalo, neno *Mkristo* linamaanisha kuwa “kama Kristo.” Huo hapo utambulisho wako. Vema. Sasa, na kwa kuwa Yeye ndiye utambulisho wetu, basi tunapaswa kutambulishwa pamoja Naye, kwa kumwishia Yeye.

140 Angalieni, Mungu amekuwa na kusudi lenye sehemu tatu katika siri hii kuu ya fumbo. Mungu, katika siri Yake kuu ya fumbo aliyokuwa nayo kabla ya ulimwengu kuanza, ana kusudi lenye sehemu tatu ndani yake. Na sasa tunachotaka kufuatilia, asubuhi ya leo, ni, ni nini kusudi hilo lenye sehemu tatu? Mnaona? Sasa, naamini, kwa msaada wa...wa Mungu, Yule aliyeko, na Yeye—Yeye atatuonyesha. Sasa, kama Yeye alikuwa na kusudi hili lenye sehemu tatu, tunataka kujua ni nini kusudi hili lenye sehemu tatu.

141 Jambo la kwanza lilikuwa, kwamba, Mungu alitaka kujifunua Mwenyewe kwa watu.

142 Hangeweza kufanya hivyo kama Yehova Mungu mkuu Yule aliyefunika anga zote, wakati, na Umilele. Asingeweza. Yeye ni mkuu mno kupata kufunuliwa kwa watu, kwa sababu ingekuwa isiyoelweka kabisa. Angewezaje Kiumbe hicho kikuu ambacho hakikuanza kamwe...kwamba ukisha kwenda zaidi ya duara ya mamia ya mabilioni na matrilioni na matrilioni ya miaka ya anga ya nuru, na kuendelea ukaingia kusiko na kikomo, ukaingia katika Umilele, na Kiumbe kikubwa kilichokuwa hayo yote, na bado kingali.

143 Lakini alichotaka kufanya, Yeye alipenda ubaba, kwa maana alikuwa Baba. Na njia pekee ambayo Yeye angeweza kuudhihirisha ilikuwa ni kufanyika Mwana, Mwanadamu. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliendelea kusema, “Mwana wa Adamu.” Mnaona, hawakujua alichokuwa anazungumzia, wengi wao. Lakini sasa mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Alitaka kujidhihirisha Mwenyewe. Hilo lilikuwa ni Lake, mojawapo ya makusudi Yake makuu yenye sehemu tatu, lilikuwa ni kujidhihirisha Mwenyewe, kujitambulisha Mwenyewe na wanadamu, kujifunua Mwenyewe katika Kristo.

144 Pili, kuwa na utangulizi katika Mwili Wake wa waaminio, yaani, Bibi-arusi Wake, apate kuishi ndani ya watu.

¹⁴⁵ Sasa, Yeye angeweza kufanya hivyo katika Adamu na Hawa, lakini dhambi iliwatenganisha, kwa hiyo sasa ilibidi kuwe na njia fulani ya kuurejesha tena. Loo, jamani! Loo, wakati mimi... Hili, hili lina kilindi, kwangu mimi, hata kuliwazia tu. Mnaona? Mnaona kilichokuwa kusudi la Mungu? Sasa kwa nini hakuwadumisha tu Adamu na Hawa namna hiyo? Basi asingeweza kamwe kudhihirisha utimilifu Wake, sifa Yake kamili. Kwa sababu, Yeye angeweza kuwa Baba pale, hiyo ni kweli, lakini pia Yeye ni Mwokozi. Unasema, “Unajuaje alikuwa hivyo?” Ndivyo alivyo, kwa sababu nimekuwa na ujuzi. Mnaona? Mnaona? Yeye ni Mwokozi, na ilimbidi kudhihirisha hilo. Naye angewezaje kufanya hivyo? Kwa njia ya Kristo pekee. Angewezaje kuwa Mwana? Kwa njia ya Kristo pekee. Angewezaje kuwa Mponyaji? Kwa njia ya Kristo pekee. Mnaona, vitu vyote vimejumuishwa katika Mtu huyo mmoja, Yesu Kristo. Loo, jamani! Wakati mimi—wakati mimi...

¹⁴⁶ Ninapoliwazia, mimi—mimi ninaona tu madhehebu yakitoweka jukwaani, na kila kitu kikitoweka tu, mnaona, ninapoonaa kusudi kuu la Mungu. Akijifunua Mwenyewe, na akiwajibika, kwanza, kujifunua Mwenyewe katika Kristo, “utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Halafu, basi, kuleta huo “utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili” ndani ya watu, ili apate kuwa na utangulizi, uangalizi, uongozi.

¹⁴⁷ Mwingine, ule usiku, kama hukupata ile kanda, nilihubiri hapa usiku mmoja, juu ya “Mfungwa wa Yesu Kristo.” Paulo, mfungwa! Unaona? Mungu anapokufanya kuwa mfungwa Wake, basi huwezi kufanya lolote ila yale Roho anayosema ufanye. Paulo, pamoja na akili zake zote kuu, alifundisha... alifundishwa na Gamalieli apate kuwa kuhani mkuu au rabi, siku moja. Na alikuwa na tamaa ya makuu. Alikuwa mtu mkuu kiakili, mamlaka makuu, mtu mashuhuri nchini. Lakini ilimbidi kusalimisha kila sehemu yake, mnaona, apate kuwa sehemu ya Neno, kumdhihirisha Yesu Kristo. Alijua maana ya kusema...

¹⁴⁸ Alikuwa na dhana ya kwenda mahali fulani, ndugu fulani walikuwa wamemwita, lakini alikatazwa na Roho kufanya mapenzi yake mwenyewe. Loo, laiti—laiti watu wa kiroho nusunusu wanaweza kuelewa hilo! Mnaona? Alikatazwa kufanya mapenzi yake mwenyewe. Angeweza tu kufanya... “Roho alinikataza.” Mnaona? Alikuwa mfungwa wa Kristo.

¹⁴⁹ Ndipo, maskini mpiga ramli huyu siku moja, ambaye alimjua, Paulo alijua alikuwa na uwezo wa kumtoa huyo ibilisi, lakini angeweza tu kufanya sawasawa na mapenzi ya Mungu. Siku baada ya siku alimfuata, akilia nyuma yake, lakini siku moja Roho akampa ruhusa. Ndipo akamkemea, roho aliyekuwa ndani yake. Mnaona? Alijua kilichomaanisha kuwa mfungwa.

¹⁵⁰ Musa, usomi wake, ilimbidi aupoteze kusudi ampate Kristo, kuwa mfungwa. Ndipo Mungu akauondoa ulimwengu wote

kutoka kwake, na utu wake wote mkuu aliokuwa nao, na kusimama Mbele za hiyo Nguzo ya Moto siku hiyo, alikutwa amepigwa tu na butwaa. Hata, asingeweza kuongea, alisema. Mungu alikuwa na mfungwa basi. Mnaona? Hutajaribu baada ya utafutaji wako mwenyewe. Ndipo ikambidi Mungu ampatie mtu huyu, ama, amjalie uwezo wa kutosha hata angeweza kwenda kule chini.

¹⁵¹ Naye akasema, “Bwana, nilimwambia Farao yale uliyosema, naye hakufanya hivyo.”

¹⁵² Akasema, “Basi chukua hii, fimbo yako,” Mungu akinena, hilo ni Neno la Mungu, “nenda huko nje na uielekeze upande wa Mashariki, na uitishe nzi.” Ndipo nzi wakaumbika, kwa sababu alikuwa na mfungwa ambaye Farao asingeweza kumnunua kwa chochote. Hakuna mtu mwingine angeweza kumgeuza kwa vyovyote. Alikuwa mfungwa kamili katika minyororo ya Neno la Mungu, amefungwa kwa BWANA ASEMA HIVI pekee.

¹⁵³ Loo, laiti Mungu angalijipatia wafungwa kama huyo! Sasa, hapo ndipo Yeye anapoweza kudhihirisha utangulizi, mnaona. Yeye, Yeye ameshika mwanamume, ama mtu, hata asijue lolote ila Kristo. Mnaelewa ninachomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Hilo ni la pili.

¹⁵⁴ Kwanza, kujidhihirisha Mwenyewe kikamilifu, Mungu katika Kristo.

¹⁵⁵ Pili, kuwa na utangulizi, kwa hili, katika Kanisa Lake, ambalo ni Mwili Wake, Bibi-arusi, mpaka angeweza kuwa na utangulizi wa kujieleza Mwenyewe kupitia kwao. Sawa.

¹⁵⁶ Na, la tatu, kuurudisha Ufalme mahali pake pafaapo, ulioanguka kwa dhambi kwa Adamu wa kwanza, kurudi mahali alipotembea wakati wa jua kupunga, pamoja na watu Wake, akazungumza nao, akafanya ushirika pamoja nao.

¹⁵⁷ Na sasa dhambi na mauti vilikuwa vimewatenganisha na Uwepo Wake na udhihirisho Wake wote. Je, mnalisoma? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kudhihirisha sifa Zake—Zake—Zake zote, kile alichokuwa.

¹⁵⁸ Kwa hiyo, kama Mwanautatu yeyote hapa ungejiachilia kwa dakika moja, unaweza kuona kwamba Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu si Miungu watatu. Ni sifa tatu za Mungu yeye yule. Unaona, ni dhihirisho. Baba, Yeye alikuwa, alitaka kuwa Baba, Yeye alikuwa Baba. Alikuwa Mwana. Pia Yeye ni Roho Mtakatifu. Naye Baba na Roho Mtakatifu ni Roho yeye yule. Hivi hamwoni? Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sio Miungu watatu. Ibilisi amewaambia mambo hayo, ili kuwafanya ninyi waabudu sanamu. Mnaona? Ni Mungu mmoja aliyedhihirishwa katika sifa tatu. Kuwa Baba, kuwa Mwokozi, kuwa Mwana, kuwa Mponyaji, mnaona, ni madhihirisho Yake.

159 Nataka kuendelea kidogo tu ili hata watu wanaosikiliza kanda wapate fununu, wanaoweza kuona. Ingenichukua mzunguko, mzunguko wa saa hiyo ya ukutani, kwa kila moja ya masomo hayo. Lakini natumai ninaliweka wazi vya kutosha hata mnaweza kuona yale ninayoyajia. Mnaona?

160 Mungu, aliyedhihirishwa katika Yesu Kristo, aliyekuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu pia, “utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.”

161 Sasa “utimilifu kamili wa Uungu kwa jinsi ya mwili” unakaa ndani ya Kanisa Lake, ule utangulizi. Yote aliyokuwa Mungu, aliyamimina ndani ya Kristo; na yote aliyokuwa Kristo, yalimiminwa ndani ya Kanisa, waaminio.

162 Si dhehebu! Tatalifikia hilo baada ya dakika chache, nalo litaliondoa mawazoni mwenu milele, mnaona; kuwaonyesha kinachosababisha hilo, kwa msaada wa Mungu, endapo tu ataturuhusia hilo.

163 Kusudi Lake ni nini sasa? Kujidhihirisha Mwenyewe kama Mwana, mnaona, unaona, na, sasa, ili kwamba ndani Yake ukae “utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Mimi, nina Wakolosai iliyowekwa hapa, papa hapa mbele yangu. Mnaona? Hivyo, kote katika Maandiko, hilo ndilo lililokuwa kusudi la Mungu. Halafu, kupitia Uzima huu wa Mwana huyu, msalaba Wake, “Damu,” linasema hapa, “ya msalaba Wake,” ili aweze kuupatanisha Mwili, Bibi-arusi, Kwake; ambao ni Hawa, Hawa wa pili. Naye Mungu alilitoa katika mfano, kama alivyomfanyia Musa na hao wote. Alifanya jambo lile lile katika Adamu na Hawa, akitoa mfano, ya kwamba walikuwa ni Kristo na Bibi-arusi. Yeye ni Adamu wa pili; Kanisa ni Hawa wa pili.

164 Na mradi Hawa wa pili anapatana dhidi ya Neno, je, si yeye anafanya jambo lile lile Hawa wa kwanza alilofanya? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kujaribu kusema, “Vema, ilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine.” Nasi tutafikia jambo hilo katika dakika chache, kama Yeye alisema ya kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Inawezaje kuwa wakati mwingine, wakati Yeye ni “yeye yule jana, leo, na hata milele”?

165 Lakini Mungu amekusudia hilo na “akayaficha kutoka kwa macho ya wenye busara na hekima, na kuyafunua kwa watoto wachanga waliochaguliwa tangu zamani” ambao walikuwa wamechaguliwa tangu zamani kuupokea.

166 Hiyo ndiyo sababu, ukiangalia kote katika wakati, wakati wowote Nuru hiyo ilipowagusa wengine, wangeikataa, na kuiondosha. Nao wasomi mashuhuri na hao makuhani wakuu wamesimama pale, palikuwapo na marabi kutoka kwa walimu wakuu na mamlaka, kama watu mbalimbali, kama vile Nikodemo na hao wengine, yule mtu aliyebobea katika usomi, wala hakuweza hata kulielewa.

¹⁶⁷ Pia kulikuwako na wale makuhani wakuu waliosimama pale nje, na marabi waliofundishwa katika Neno hilo. Jamani, walilifahamu, kiakili! Ndipo akasema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mtazifanya.” Wazieni jambo hilo, watu watakatifu, usingeweza kuelekeza kidole chako popote kwenye maisha yao, wala maisha ya baba yao, wala maisha ya babu yao, au maisha ya babu-wa babu-wa babu-wa babu yao. Wangalifanya hivyo, walikufa katika aibu, walipigwa mawe wakafa. Lakini huyu hapa Yesu amesimama, akiliita kundi hilo, “kundi la mashetani,” watu wa kidini.

¹⁶⁸ Sasa, loo, ule ufunuo mkuu sasa! Sasa kurudisha jamaa Yake, kurudisha... Sasa, ilimbidi kuwaacha wapotee. Mnalielewa? Ilimbidi kuwaacha watende dhambi, awape uhuru wa kujichagulia... A—asingeweza kuwafanya watende dhambi, na abaki Mungu, halafu awaadhibu kwa jambo alilowafanya Yeye watende.

¹⁶⁹ Lakini Yeye alipomweka mwanadamu katika ushirikiano pamoja Naye, kisha akampa uhuru wa kujichagulia, mnaona, kitu kile kile alichokuwekea leo hii. Unaona? Unaona? Unatenda vyovyote utakavyo; wewe una uhuru wa kujichagulia. Kwa hiyo, basi, kama alimweka yule wa kwanza namna hiyo, hana budi kumweka wa pili namna hiyo, hana budi kumweka kila mtu namna hiyo, la sivyo Yeye alikosea kwanza kabisa. Mnaona? Lakini kila mtu yuko kwenye msingi uo huo.

¹⁷⁰ Sasa tukiona, katika kumrudisha huyo; na kumwacha mtu huyo afanye jambo hilo, huku akijua ya kwamba angelifanya, alijua angelifanya. Lakini hilo lilifanya nini? Ilionyesha sifa Yake kama Mwokozi. Na kusudi zima basi limeachwa katika Yesu Kristo, kuwa... Mungu Mwenyewe kuchukua adhabu ya sheria Yake Mwenyewe, kifo, kufa, kumkomboa mke aliyeptotea kwa kumkataa Yeye.

¹⁷¹ Hawa alipojitenga na Neno, alijitenga na mwenziwe. Na wakati kanisa linapoondoka kwenye Neno, kuyaendea madhehebu, hukataa na kufanya uasherati na ulimwengu wa hekima ya mwanadamu, likikataa mamlaka ya Neno la Mungu. Hilo linasikika dhahiri? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Biblia ilisema, “Kufanya uasherati wa kiroho.” Neno lolote katika Biblia, linalokataliwa, ama kama tafsiri yoyote ya kibinafsi ikiwekwa Kwake, ni kukataa kabisa na kuzini dhidi ya Mungu ambaye ni Mume wako. Mzinzi kamwe haingii katika Ufalme wa Mbinguni, tunajua hilo. Mnaona? Sasa, mnaona, hivyo ndivyo Hawa alivyofanya kwanza kabisa.

¹⁷² Sasa angalieni tena, sasa, kusudi Lake lenye sehemu tatu ni nini? Kujidhihirisha Mwenyewe katika Yesu Kristo; kuingia katika Mwili, kwa njia ya Yesu Kristo, kuwa na utangulizi; ili (nini?) kuirejesha Edeni, kurudisha kile kilichopotea. Hicho

ndicho kitu pekee kilichokuwa nje ya utaratibu. Mambo Yake mengine yote yalikuwa katika utaratibu.

¹⁷³ Lakini ilimbidi kumwacha, kumweka mwanadamu katika uhuru wa kujichagulia, apate kuanguka, kusudi Yeye apate kuwa Mwokozi, kuonyesha kile kilicho ndani Yake, mnaona, sifa Yake ya Mwokozi. Ilibidi kitu fulani kipotee. Na jambo lenyewe, kwamba mwanadamu huyo alianguka na kupotea, Yeye akawa Mwokozi wake, akichukua sheria Yake Mwenyewe. Naye asingeweza kufanya hivyo kama yule Yehova mkuu aliyefunika anga lote, wakati; unaona, asingeweza kufanya hivyo. Naye ilimbidi awe Mwanadamu. Naye akachukua udugu na mwanadamu aliyepotea, amina, na akawa Mwanadamu: Mungu, aliyefanyika mwili!

¹⁷⁴ Haleluya! Mnadhani nimesisimkwa; lakini sivyo. Ni kitu Fulani ndani!

¹⁷⁵ Mungu alifanyika, kutoka kwa Mungu, akawa mimi, kujitwika dhambi yangu, apate kunifanya Yeye, amina, kurudi kwenye kusudi Lake kuu la wana na binti za Mungu, kwa maana Yeye ni Baba wa Milele. Sifa hiyo ilikuwa ndani Yake, mnaona, kwa hiyo hiyo ilibidi idhihirishwe.

¹⁷⁶ Sasa mnaona kusudi lote lenye sehemu tatu? Mnaona, kujidhihirisha Mwenyewe, anataka kuwa... Sasa, u—ulimwengu umepotea, sasa hana budi kujidhihirisha Mwenyewe katika Mwanadamu, apate kuwa Mwokozi, kwa upatanisho wa Damu kutoka kwa msalaba Wake. Sasa, ilibidi awe hivyo, apate kufa, ili kuokoa na kujirudisha Mwenyewe Kanisani, kuwa na utangulizi katika Kanisa Lake.

¹⁷⁷ Sasa kumbukeni, haliwezi, na halitakuwa, na kamwe halitakuwa, wala haliyawahi kuwa, dhehebu! Yeye hana budi kuwa na utangulizi, na Yeye ni Neno. Amina! Kanuni yoyote ya imani inawezaje kusukumiwa Mle? Ni... inaligeuza kanisa kuwa kahaba, kuchukua maneno ya mtu yeyote ya kanuni yoyote ya imani au dhehebu lolote. Limewekwa alama upesi, katika Ufunuo 17, kama kahaba na malaya; Kanisa Katoliki la Kirumi likiwa ndilo kahaba mkuu, na Waprotestanti wakiwa ndio makahaba. Ni dhahiri kabisa kadiri mtu yeyote angeweza kulisoma. Tumepitia kwenye Nyakati za Kanisa, nanyi mnaweza kuona hilo katika kanda hi—hizo mkitaka. Kweli kabisa. Basi, chochote kinachojiunga na kanuni ya imani nje ya Biblia, ni kahaba machoni pa Mungu. Na kimefanya jambo lile lile alilofanya Hawa; kajitenga na Neno, ambalo ni Kristo. Loo, jamani! Vema.

¹⁷⁸ Sasa tunaona siri Yake aliyokuwa ameificha akilini Mwake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Sasa mngependa kusoma machache ya hili? Hebu tulisome tu. Je, mna muda mwingi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tuta—tutalisoma. Sasa hebu sote tufungue, kwa somo moja

tu, kwa vyovyote vile, kwenye Kitabu cha Waefeso, na hebu tuanzie kwenye m—mlango wa kwanza wa Waefeso, kusoma. Na sasa wakati somo la shule ya Jumapili likiendelea sasa, katika madhihirisho haya yenye sehemu tatu ya Kristo, hebu na tusome.

Paulo, mtume wa Yesu Kristo, kwa mapenzi ya Mungu, . . .

179 Sasa angalieni, halikuandikiwa walimwengu, lakini:

. . .kwa watakatifu walioko Efeso, na waaminio katika Kristo Yesu:

180 Unaingiaje ndani ya Kristo Yesu? Kwa kujiunga na kanisa? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Kwa Kuzaliwa! “Kwa Roho mmoja,” Wakorintho wa Kwanza 12, “sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Mnaona?

181 Sawa, hao ndio anazungumza nao. Hilo halikuandikiwa ulimwengu wa nje. Hatuwezi kumzungumzia mwenye dhambi kuhusu haya, maana yeye hajui lolote kulihusu. Paulo hakuliandika kwa wenye dhambi wowote. Alisema, “Hili ni kwa kundi lile—lile—lile lililo katika Kristo Yesu.”

Neema na iwe kwenu, na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohani (wapi?) katika ulimwengu wa roho ndani yake Kristo:

182 “Ulimwengu wa Roho.” Loo, laiti ningalikuwa na wakati! Hapa nimeliweka alama papa hapa katika Biblia yangu, kuhusu ulimwengu wa Roho, kwamba ulimwengu wa Roho ni nini. *Ulimwengu wa Roho*, kwa muda kidogo tu, ni “mahali pa mwaminio katika Kristo,” mnaona, “mahali mwaminio anaposimama katika Kristo,” katika ulimwengu wa Roho.

Kama vile alivyotuchagua . . . (sikiliza kwa makini) . . . alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, . . .

183 Alituchagua lini? “Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu,” wakati ile siri Yake kuu iliyofichwa, siri Yake kuu.

. . .Alituchagua katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika (nini?) upendo:

Kwa kuwa (nini?) alitangulia kutuchagua ili tufanywe wana kwa njia ya Yesu Kristo mwenyewe, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,

184 “Alitangulia kutuchagua!” Hilo hapo fumbo. Yeye, kabla ya Kristo ama chochote kile kuwepo duniani, mnaona fumbo Lake kuu, ya kwamba alimchagua Bibi-arusi. Akijua Hawa

angeanguka, kutokana na kutokuliamini Neno, akijua ya kwamba angeanguka; lakini Yeye angechagua Bibi-arusi ambaye hataanguka, ambaye angeshikilia Neno hilo haidhuru ulimwengu wote ungesema nini kulihusu. Wangelishikilia Neno hilo! Wamechaguliwa tangu zamani kusimama hapo, “kufanywa wana wenye mamlaka na Yesu Kristo,” akalichagua Kanisa tangu zamani kwenye msimamo huo mkuu, wenye utukufu!

¹⁸⁵ Sasa mnaiona siri Yake? Ya kufanya nini? Kumrejesha Hawa aliyeanguka, kwa kuwa alikuwa mfano tangulizi wa Kanisa. Na sasa angalieni, kama vile Mungu alivyofungua ubavu wa Adamu na kumtoa Hawa, kwa mwili wake na damu yake mwenyewe; na kutenganisha roho yake kutoka kwa ya kiume na ya kike, ikawa ya kike, na kuiweka ndani ya Hawa. Akautwaa ubavu chini ya ubavu wake, akamfanya Hawa kutoka kwake; kwa hiyo Mungu alifanya jambo lile lile, akitoa kutoka ubavuni mwa Kristo, Damu na maji. Naye Kristo ni Neno, na kuchukua Neno na kufanya Kanisa Lake, Hawa; mnaona, kurejea Kwake tena, akikombolewa kwa Damu iliyotoka katika Mwili Wake. Mnaliona sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁸⁶ Fumbo kuu la Mungu sasa likifunuliwa, ambalo limefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, lakini akatangulia kulionyesha kwa mifano kote kote. Sasa angalieni, tunaona ya kwamba, ya kwamba Yeye—ya kwamba Yeye alifanya hivyo. Na hapa katika Waefeso, na sehemu nyingine nyingi, lakini hayo yatawapa ya kutosha... Sasa, kote katika nyakati, amekuwa akifunua fumbo hili polepole. Mnaweza kuona sasa? Sasa, kote katika...

¹⁸⁷ Alifanyaje...? Ilikuwaje katika kivuli sasa? Aliufungua ubavu wa Adamu na kuchukua sehemu ya mwili wake, ambao ulikuwa ni Adamu, kumfanya Hawa. Bibi-arusi hana budi kuwa Neno, kwa maana Yeye ni Neno. Hawezi kusimama juu ya kanuni za imani. Hawezi kusimama juu ya madhehebu. Hawezi kusimama juu ya matendo mema. Hana budi kusimama peke yake juu ya Neno, kwa maana Yeye ni sehemu Yake. Alitwaliwa kutoka kwa Kristo. Mnaona?

¹⁸⁸ Na ili kuwa na hakika, ya kwamba, Unyakuo mzima sasa: Luther alikuwa sehemu, Wesley alikuwa sehemu, manabii walikuwa sehemu. Ikiwa wao—sio sehemu... Katika ufunuo tu waliokuwa wakiutengeneza, mwili, miguu, vidole vya miguu, mikono, na kadhalika, mpaka Kichwa (ambacho tutakifikia hicho katika dakika chache), mnaona, hiyo inafanyiza Unyakuo kamili. Ni Mwili wa Neno, ambao ni Kristo. Amina!

¹⁸⁹ Nje ya Huo, umepotea. Sijali jinsi ulivyo mzuri, au uhusiano wako ni upi, au ushirika wako ni upi, au shirika lako ni lipi, umepotea, nje ya hilo Neno kuwa ndani yako.

¹⁹⁰ “Mkikaa ndani Yangu, Neno, Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo,” kwa sababu wewe na Neno ni kitu kimoja. Yeye ana utangulizi. Anao utawala. Wewe ni—wewe ni mfungwa Kwake. Ulimwengu umekufa. Huna chochote zaidi. . . Unawaona watu wengine wakiishi jinsi wanavyoishi, lakini hata hivyo wewe hufanyi hivyo. Wewe ni mfungwa. Umefungwa nira pamoja Naye. “Nira yangu ni nyepesi.” Umefungwa nira pamoja na Kristo, pamoja na Neno Lake. “Ninafanya kile tu ambacho ninii. . . kinampendeza Baba. Na endapo hamwezi kuamini ya kwamba Mimi Ndiye, basi liaminini Neno.” Kamilifu kabisa! Angalieni.

¹⁹¹ Angalieni sasa, kote katika nyakati, Yeye amekuwa akiliachilia hili pole pole, akilifunua fumbo hili polepole, kwa njia ya manabii na kwa njia ya mifano. Sasa tunaweza tu kuendelea na jambo hilo, na, akijidhihirisha Mwenyewe.

¹⁹² Alijidhihirisha Mwenyewe katika Musa. Mwangelie Musa. Alizaliwa wakati wa mateso ya watoto. Alizaliwa awe mkombozi. Alifichwa kwenye manyasi, kama vile tu Yesu alivyopelekwa Misri. Akatoka nje. Akapanda juu mlimani, akarudi na zile amri.

¹⁹³ Yesu alipanda mlimani, mahubiri Yake ya kwanza, Mahubiri ya Mlimani, akashuka chini na zile amri. “Mliwasikia wakisema, watu wa kale, ‘Usizini.’ Nawaambia, mtu amtazamaye mwanamke, kwa kumtamani, amefanya uzinzi.” Mtoa-Sheria, Kuhani, Mfalme, Kiongozi, sawa kabisa!

¹⁹⁴ Alijidhihirisha Mwenyewe katika Yusufu, aliyezaliwa miongoni mwa madhehebu, ndugu zake. Walimchukia, bila sababu, kwa sababu alikuwa wa kiroho. Aliona maono. Mungu alikuwa pamoja naye. Angeweza kufasiri ndoto. Nao ndugu zake wakamchukia. Aliuzwa kwa ka-. . . na ndugu zake, karibu vipande thelathini vya fedha. Kama vile tu Yeye alivyouzwa na Yuda Iskariote, mmoja wa ndugu Zake, kwa vipande thelathini vya fedha. Alitupwa shimoni na kudhaniwa amekufa. Hiyo ni kweli. Baba na hao wengine waliambwa kwamba alikuwa amekufa. Kwamba ametupwa kwenye shimo hili; akatwaliwa juu, akaenda kwenye mkono wa kuume wa Farao.

¹⁹⁵ Gerezani, jinsi alivyoteseka huko! Na—na kulikuwa na wawili waliookolewa. . . Mnyweshaji na mwokaji, mmoja wao alipotea na mmoja akaokolewa, hasa. Naye m—mnyweshaji. . . Mmoja wao alipotea na mwingine akaokolewa. Kama vile tu pale msalabani, alipokuwa katika nyumba Yake ya gerezani, ametundikwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, akawa Mfungwa, mwizi mmoja alipotea na mmoja akaokolewa. Mnaona, sawa kabisa.

¹⁹⁶ Ndipo akaja kwenye mkono wa kuume wa Farao, mfalme ambaye aliota ndoto, ambaye alipata ono kwamba angeketi miguuni pa mfalme, na mamlaka yote katika Misri akapewa

yeye. Ono lake ilibidi litimie. Huenda alisoma habari zake, mara nyingi, alipokuwa katika—katika gereza hilo huko chini. Masharubu yake yakikua, na kadhalika, bali aliisoma. Siku moja ilibidi ono lake litimie.

¹⁹⁷ Ingawa linakawia, halina budi kutendeka! Kama nilivyonena jana usiku, ama hivi majuzi usiku, Jumatano usiku hapa kwenye ibada. Mnaona, halina budi kutukia. Mungu anaposema hivyo, halina budi kutukia. Ni nabii aliyethibitishwa, na halina budi kutimia, maana ni Neno la Mungu.

¹⁹⁸ Nalo Neno humjia tu nabii. Neno *nabii* maana yake “mfunuzi wa Neno la Kiungu lililoandikwa,” sawasawa na inavyomaanisha “mtabiri,” mnaona, au “mwonaji.” Angalieni. Na mwonaji, jinsi gani, yule unayejua anatabiri, yeye amethibitishwa Kiungu kwa kuona awali, na yanatimia. “Kama kuna mmoja ambaye ni nabii, atazungumza nanyi na kuwaambia mambo fulani yatatukia. Na ikiwa halijatukia, msimsikilize. Lakini likitukia, basi niko pamoja naye. Afadhali mumwogope, kwa maana niko pamoja naye, mnaona.” Hiyo ni kweli hasa. Hilo hapo thibitisho, pale unapojua kama ni Kweli ama kama sivyo.

¹⁹⁹ Mungu anajibu kupitia Neno Lake, kwa watu Wake, kwa njia ya watu. Mnaona, Mungu hunena tu kupitia kwa mwanadamu. “Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi.” Mzabibu hauzai matunda. Matawi huzungumza, huzaa matunda ya Mzabibu. Angalieni, daima imekuwa hivyo.

²⁰⁰ Sasa tunamwona Yusufu, basi, kwamba wakati hakuna mtu angeweza kumgusa ama kuja kwa Farao bila kwanza kumwona Yusufu. “Hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba, ila tu kwa njia ya Mwana.” Ndipo Yusufu alipoondoka kwenye kiti cha enzi, walipiga baragumu, “Kila goti liiname! Yusufu anakuja!”

²⁰¹ Utukufu! Na siku moja kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri, atakapoondoka kwenye Kiti cha Enzi cha Baba Yake, mnaona, kuja huku. Kila mtu atashuhudia kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Ama wewe . . . Umechelewa kupita kiasi basi. Fanya hivyo sasa.

²⁰² Sasa tunaona ya kwamba kupitia kwa mifano, tungeweza kumchukua hata Daudi, kama nilivyonena habari zake muda mfupi uliopita, akitoka katika kiti chake cha enzi, amekataliwa na watu wake mwenyewe; akipanda mlima ule ule, Mlima wa Mizeituni, anapoelekea kwenye gereza lake. Alikuwa akienda kwenye nyumba yake ya gereza kwa sababu alikataliwa na ndugu zake na watu wake mwenyewe. Akapanda juu, akilia. Huyu alikuwa ni Roho wa Kristo ndani yake, kukataliwa, alipoitazama Yerusalemu na kulia, na kusema, “Yerusalemu, ni mara ngapi Mimi. . .” Mfalme aliyekataliwa. Miaka mia nane baadaye, Mwana wa Daudi alisimama juu ya Yerusalemu, kule

juu ya Yerusalemu, na amekataliwa, na kuililia Yerusalemu, na kusema, “Sasa saa yako imefika.” Hiyo ni kweli. Mnaona?

²⁰³ Mambo hayo yote yalikuwa ni mfano Wake, kwa njia ya mfano tu, bali hata hivyo fumbo lilikuwa limefichwa. Hao watu hawakujua walichokuwa wakifanya. Walijua tu kwamba waliongozwa na Roho kufanya mambo fulani. Sasa, kuificha katika siku za mwisho, kwa ajili ya ufunuo mkuu. Bali, akilidhihirisha, akijidhihirisha Mwenyewe katika Musa, na Daudi, na Yusufu, na Eliya, na kote kote. Wewe... tungeweza kuchukua kila mmoja wa hao manabii, na kuyafafanua maisha yao na kumdhihirisha Yesu Kristo kikamilifu, hasa. Hata hivyo, pasipo kutoa siri Yake kwa ukamilifu; akingojea kuitangaza katika siku za mwisho kama alivyoahidi, akingojea ieleweke kikamilifu, mnaona, kabla Yeye hajaidhihirisha. Kama angalisema hilo jambo lote...

²⁰⁴ Kwa sababu, Biblia imeandikwa katika mafumbo. Yesu alimshukuru Baba kwa ajili yake, mnaona, ya kwamba iliandikwa katika mafumbo.

²⁰⁵ Sasa, Kuja kwa Bwana ni katika siri. Hatujui atakapokuja, jinsi anavyokuja, lakini tunajua Yeye yuaja. Mnaona? Na vivyo hivyo siri zote za Mungu zilikuwa zikingojea siku hizi za mwisho. Ikiisha kukamilika, ndipo Yeye hufichua na kuonyesha yale aliyofanya. Loo, jamani! Kamwe hakutoa siri Yake kwa ukamilifu.

²⁰⁶ Ni hivi tu, kulinganisha ile Mihuri Saba. Sasa, Mungu alipomtumia Martin Luther kwa ajili ya kutoka kwenye kanisa la kwanza ama wakati huo wa kanisa, na alipomtumia John Wesley, Naye akawatoa hatua kwa hatua, na alikuwa akifunua ndani yao wakati huo wa kanisa. Wakati sisi... inaporudi katika Biblia sasa na kujua. Lakini katika siku za mwisho, sababu ya hilo kuwa jambo kubwa sana, hata akanena habari zake hapa na kuzionyesha hizo Ngurumo Saba. Na ninii ya *Look na Life*...

²⁰⁷ Gazeti la *Life* basi likachapisha Duara hiyo ya Wingu na Nuru pale ambayo wasingeweza kuelewa, wala bado hawajui. Lakini huku nikiambiwa, “Nenda huko ukangojee siri hizi zifunuliwe,” na hapa miezi kadhaa kabla halijatokea, halafu likatukia jinsi hasa Yeye alivyosema lingetukia. Je, mliona kwenye hiyo picha? Hata Malaika huyo kwenye mkono wa kulia, alipokuwa akianza kuonekana, akishuka chini, huku mbawa zake zimerudi nyuma na kichwa chake kiko upande mmoja, huyo papo *hapo* kwenye picha, vivyo hivyo kabisa. Miezi kadhaa kabla halijatukia, ilielezewa hapa, kwamba, “Atauleta Mwili wa waaminio pamoja; kufunua, kuleta miisho iliyopotea.”

²⁰⁸ Huyu hapa Luther anapita, alihubiri tu kuhesabiwa haki, akatwanga tu katika wakati huo. Hakujua huo wakati ulikuwa nini. Huyu hapa Wesley akaja, naye akautwanga wakati wake kweli kweli. Mnaona? Midomo mingi ya mito ilitoka kwake,

yale makanisa mengine yakiinuka. Ndipo hii hapa Pentekoste inakuja, ikitwanga-twanga, nao wakaunda madhehebu na kurudi moja kwa moja mautini tena; kama tutakavyolifikia katika dakika chache, ikarudi moja kwa moja katika “mauti.”

²⁰⁹ Halafu basi ukaja ufunuo wa hilo fumbo, kufunua kwamba yote yanahusu nini. Ambapo, mafundisho haya madogo madogo, kama vile Luther alivyotoa katekismo na kadhalika; naye Wesley akaleta *hili, lile*, na *linginelo*, na mambo haya mengine; halafu basi Pentekoste ikaleta madhehebu vivyo hivyo, na ubatizo wa “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” na kadhalika; bila kujua tofauti yoyote, maana. . . Kisha kurudi katika siku za mwisho na kufukota siri hizi zote na kuzifafanua waziwazi, kuzifunua. Kwa nini? Ni kote katika siku za mwisho ambapo siri hii kuu ambayo Mungu alikuwa nayo moyoni Mwake inapofunuliwa.

²¹⁰ Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mkishindwa, rudini kwenye kanda hii tena. Sijui nitakuwa nanyi kwa muda gani zaidi. Kumbukeni, hii ndiyo Kweli, ya BWANA ASEMA HIVI. Ndiyo Kweli. Ni Maandiko.

²¹¹ Kama yale mafumbo saba ya ile Mihuri saba ya mwisho, mafumbo yake. Mihuri ilikuwa tayari imevunjwa, na kila wakati ulikuwa umeshuka, na hapo walikuwa wameacha mtawanyiko mwingi. Naye Mungu, pasipo kupenda kwamba itawanyike, Yeye anarudi na kuyaokota mambo hayo, hayo mafundisho waliyoanzisha, na kuyaleta na kufunua kitu hicho chote. Jambo lile lile analofanya sasa katika kufunua siri ya Kristo, jinsi Yeye alivyokuwa kusudi la Mungu lenye sehemu tatu kwa ajili ya Kanisa! Loo, jamani! Kumwacha atoke nje. Kufunua!

²¹² *Kufunua*, Webster inasema, ni “Fahamisha. Fahamisha, na, hasa sana,” Webster inasema, “katika Ukweli wa Kiungu,” ndivyo *ufunuo* unavyoamaanisha. Ufunuo, ni njia ya Kristo ya kujitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa Lake.

²¹³ Sasa tutasema, “Sasa, Ndugu Branham, unasema hivi tu.” Sasa, hatutasema, *kusema* tu hivi.

²¹⁴ Sasa angalieni, Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa Petro. Sasa kama unataka kuandika hili, nasi. . . Mkitaka kulisoma, tuta—tutalisoma, mkitaka, katika Mathayo Mtakatifu 16:15 na 17. Nitalinukuu. Walipokuja kutoka Mlima wa Kugeuka Sura, Yeye anasema, “Watu huninena mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

²¹⁵ “Wengine wanasema, loo, wanafikiri Wewe ni ‘Eliya,’ na wengine wanasema Wewe ni ‘mmoja wa manabii,’ ‘Yeremia,’ au baadhi yao.” Lakini hilo silo alilouliza.

²¹⁶ Alisema, “Mnafikiri Mimi ni nani sasa?” Sasa hilo hapo Kanisa analozungumza nalo. Mnaona?

“Watu wanafikiri mimi ni nani?”

217 Leo, “Yeye ni mwanafalsafa; dini hii ya kijamii. Alikuwa mtu mwema. Tunaamini mafundisho Yake ni sahihi. Ni somo la kuishiwa. Nafikiri lingetufanya sote bora zaidi, kama tungeliishia. Tunapaswa kuwa na makanisa yetu, kadhalika yetu—yetu.” Huyu ni Baba Krismasi, kama hadithi ya Baba Krismasi.

218 Sio matamshi ya kanisa fulani ambayo tunapaswa kuelezea jambo fulani. Ni maisha usiyoishi wewe mwenyewe, bali Yeye anaingia ndani yako na kuishi Mwenyewe, ndipo unakuwa mfungwa; kwa mwanadamu yeyote wa kielimu hata kidogo. Unaongozwa na Roho. Nawe unajuaaje?

219 Sasa unasema, “Huenda nikajua nilikuwa nikirukwa na akili. Labda mtu anayerukwa na akili hufanya hivyo.”

220 Lakini ikiwa unayo nia ya Kristo, Kristo anajidhihirisha Mwenyewe kupitia kwako, inaonyesha kuwa ni Yeye wala sio... hujarukwa na akili.

221 Baadhi ya watu, chini ya udanganyifu wa mambo, wanatoka wakaingia wazimu. Vema, hilo, tunajua hilo ni kosa. Huyu ni ibilisi akijaribu kuiga kitu kilicho halisi kabla hakijafika hapa, mnaona, daima ni bandia. Mnaona?

222 Lakini mtu halisi ni kupoteza mawazo yake mwenyewe na fikra zake! Sio kuja kwa upofu namna hiyo. La, bwana. Unakuja na hisi zako nzuri, naye Kristo anakuchukua na kujidhihirisha Mwenyewe. Na sasa, kwa ulimwengu, wewe ni mwendawazimu.

223 Sasa, kama wewe ni mwendawazimu, wewe ni mwendawazimu kweli, basi hakuna kitu...ibilisi hawezi kukuchukua katika udhibiti kamili. Atakufanya ufanye kila kitu kinyume na hili Neno.

224 Lakini Kristo atakapokutawala, Yeye atalidhihirisha Neno hilo moja kwa moja kupitia kwako, kwa sababu ni Yeye. Yeye ni Neno! Unaona? Na ndipo unaweza kuona udhihirisho wa Kristo. Si udanganyifu wa namna fulani, bali Kristo halisi wa kweli akijidhihirisha Mwenyewe moja kwa moja kupitia kwako. Ni nzuri jinsi gani!

225 Sasa angalieni. Yeye alisema, “Nyinyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?” Analiuliza Kanisa, wale kumi na wawili Wake. Kati ya mamilioni wa siku hiyo, Yeye aliuliza kumi na wawili, Kanisa Lake.

Katika mamilioni katika siku za Nuhu, Yeye aliwauliza wanane. Uh-huh. Mnaona?

226 Naye akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, unaona, ambapo watu wanane waliokolewa.”

227 Sisemi kutakuwa na wanane watakaokolewa sasa. Sasa msilielewe hilo vibaya. Sikusema hivyo. Sijui watakuwa wangapi, watakaokolewa katika hilo, kwamba hivyo ndiyo...

dakika hiyo ya mwisho kabla ya—ya Kulinyakua kundi hilo dogo. Litakuwa kundi dogo, nitawaambia hilo. “Kwa kuwa mlango ni mwembamba, na njia imesonga, lakini waionao ni wachache.”

²²⁸ Lakini wakati ule Mwili mkuu uliokombolewa katika nyakati zote utakapotokea, basi hiyo itakuwa enzi kuu sana kule! Ufunuo 7 inaliezea, “Umati mkubwa sana, ambao hakuna mtu awezaye kuhesabu,” kote katika nyakati zote wametokea, hao waliotembea katika Nuru ya Biblia kadiri ilivyofunuliwa kwao. Na sasa tunajua ya kwamba Wesley alikuwa na Nuru kuu kuliko aliyokuwa nayo Luther. Tunajua Pentekoste iling’aa zaidi kuliko Wesley. Mnaona? Bila shaka, huwa hivyo.

²²⁹ Kwa sababu, iliachiliwa hatua kwa hatua, kama ilivyofanya kupitia kwa manabii, na kadhalika, mpaka ikajulikana kikamilifu, “Uungu kwa jinsi ya mwili katika Kristo.”

²³⁰ Na sasa Kristo Kanisani ndio kwanza anatambulishwa. Jambo lote ni ufunuo wa Mungu, kumrudisha Hawa mahali pake sahihi tena pamoja na Mumewe. Angalieni, na Mungu ndiye Mume wa Kanisa, nalo Kanisa ni Bibi-arusi Wake.

²³¹ Sasa, Petro, alipoita, alisema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

²³² Sasa angalieni. “Heri wewe, Simoni *Bar-yona*,” anasema, ambalo linamaanisha, “mwana wa Yona.” Mnaona? “Heri wewe, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia Hili. Hukujifunza Hilo kutoka kwa shule fulani. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia.” Angalia alichomwambia, “Juu ya mwamba huu. . .” Huyu ni Petro, Mzao wa Mungu aliyechaguliwa tangu zamani ambaye alikuwa amepokea Nuru hii, na kupewa funguo za Ufalme. “Juu ya mwamba huu wa ufunuo kwamba Yesu Kristo ni Nani,” Yeye ndiye Mungu kamili, aliyedhihirishwa. “Juu ya mwamba huu. . .” Si Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; Naye akiwa ni Mtu wa pili. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalitikisa kamwe, kamwe hayatalishinda.” Mnaona? “Nitalijenga Kanisa Langu juu ya mwamba huu,” ufunuo wa Yesu Kristo.

²³³ Angalieni, Kristo ndani yako anamfanya Yeye kuwa kiini cha Uzima wa ufunuo. Mnaona? Uhai wa Kristo ndani yako unamfanya Yeye kiini cha ufunuo. Kristo, katika Biblia, huifanya Biblia kuwa ufunuo kamili wa Kristo. Kristo ndani yako hukufanya ufunuo kamili wa jambo hilo zima, unaona, yale Mungu anayojaribu kufanya.

²³⁴ Kuzaliwa upya ni nini basi? Ungesema, “Vema, Ndugu Branham, Kuzaliwa upya ni nini?” Ni ufunuo wa Yesu Kristo kibinafsi kwako. Amina! Unaona? Si kwamba ulijiunga na kanisa, ukapeana mkono, ulifanya jambo tofauti, ulikariri kanuni ya imani, uliahidi kuishi kwa m—mfumo wa kanuni. Lakini Kristo, Biblia, Yeye ni Neno lililofunuliwa kwako. Na

haidhuru mtu yeyote anasema nini, kinachotukia, ni Kristo; mchungaji, kasisi, chochote kile. Ni Kristo ndani yako, huo ndio ufunuo ambao Kanisa lilijengwa juu yake.

²³⁵ Unasema, “Vema, mimi ni Mlutheri. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri.” Hilo halimaanishi moja, halimaanishi [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] *hivyo* kwa Mungu, si kitu, si mdato wa kidole chako.

²³⁶ Ni nini? Ni Kristo akifunuliwa, Naye ni Neno. Nalo Neno linapofunuliwa, linajidhihirisha Lenyewe. Mnaona? Hilo ndilo kusudi la Mungu kwa Yesu Kristo, lilikuwa ni kujidhihirisha Mwenyewe, kuchukua sheria Zake Mwenyewe na kuishi kwa sheria Zake, athi- . . . na kuitimiza sheria Yake, kwa mauti. Naye Kristo, Mungu, alikufa katika mwili, ili aihukumu dhambi katika mwili, apate kujiletea Mwenyewe Bibi-arusi mtukufu, aliyekombolewa tena, ambaye ataamini tu katika Neno la Mungu; wala asilibadilishe, kama Hawa alivyofanya, kwa mawazo ya kiakili ya mwanadamu. Unaiona? Hilo ni wazo la Kristo. Hilo ni wazo la Mungu. Kuzaliwa upya kunaonyesha hili.

²³⁷ Basi mtu akisema amezaliwa mara ya pili, na kujaribu kuweka ahadi hizi za Kristo, katika siku hizi za mwisho, kwenye wakati mwingine, kumfanya Kristo jana lakini sio leo, basi mwanamume huyo au mtu huyo amekuwa katika u—udanganyifu wa Shetani. Na kama mtu huyo akisema ya kwamba anaamini Hilo, wala halijidhihirishi kupitia kwake?

²³⁸ Yesu alisema, katika Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; ulimwenguni kote, na kwa kila wakati.” Kuwatoa pepo, na kunena kwa lugha, na—na madhihirisho haya yote makuu ya karama ambazo zingefuata, ya kwamba, “zitafuata!” Si, “*huenda zikawa; zinapaswa.*” “Zitafuata!” Na mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake halitapita.

²³⁹ Kwa hiyo ni Kristo akijidhihirisha Mwenyewe katika mtu binafsi, awe ni msomi au ha—hajui ABC zake. Nusu ya mitume hawakuzijua, hiyo ni kweli, bali walimjua Kristo. Hawakuwatambua Petro na Yohana, wakijua kwamba walikuwa wametoka katika seminari fulani. Walisema, “Wakatambua na kuona kwamba walikuwa pamoja na Kristo,” walipomponya yule kiwete, mnaona, langoni. Walitambua wao—walikuwa pamoja na Kristo.

²⁴⁰ Kuzaliwa upya ni Kristo, ni ufunuo. Mungu amekufunulia siri hii kuu, na huko ndiko Kuzaliwa upya. Sasa utafanya nini ukileta kundi hilo lote pamoja? ambapo ufunuo unapatana kikamilifu, naye Mungu akilidhihirisha kupitia Neno Lake kwa matendo yale yale, mambo yale yale aliyofanya, akilidhihirisha Neno. Loo, laiti Kanisa lingejua mahali pake! Litajua, siku moja. Ndipo, Kunyakuliwa kutakwenda wakati litakapojua ni nini. Angalia sasa.

²⁴¹ Unasema, “Ndugu Branham, lakini hilo—hilo si. . .” Loo, naam, ni, pia. Ni Kweli.

²⁴² Je, mlitambua? Paulo hakuwahi kumjua Yesu, kimwili. Paulo hakumjua kamwe. Njia pekee ambayo Paulo alimjua ilikuwa kwa ufunuo, kwa ono. Je, hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Paulo alimjua Yesu tu kwa ufunuo, kama tu Petro alivyomjua.

²⁴³ Petro alikuwa amemwona katika mwili, bali hakumjua kwa mwili, maana Yesu alisema hivyo. “Mwili na damu havikukufunulia. Hata maisha Yangu Mwenyewe hayakukufunulia. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia jambo hilo,” kwamba Yeye ni Neno la Mungu, “na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Petro hakumjua kwa mwili. Mwanadamu alitembea, na kumshika Yeye, na chochote kile.

²⁴⁴ Paulo alikuwa na kitu kikubwa kuliko mtume yeyote. Mnaona?

²⁴⁵ Walisema, “Naam, ni—nina ufunuo mwingi kuliko wewe, Paulo, kwa sababu, unajua, nilitembea pamoja Naye. Nilienda kuvua samaki pamoja Naye, siku moja. Nilimsikia akiongea. Alikaa kwenye mashua pamoja nami, na kwa kweli akaniambia, ‘Hebu twende hapa tukavue samaki mahali hapa, na tutapata samaki wengi zaidi.’ Nasi tulifanya hivyo.” Unaona? Unaona? “Tulimwona akifanya mambo.”

²⁴⁶ Lakini Paulo alimwona baada ya kufa, kuzikwa, kufufuka tena, na kujidhihirisha Mwenyewe katika Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Akijua...Paulo, akiwa Myahudi, kamwe hangeiita hiyo “Bwana” isipokuwa aliona lile dhihirisho, alikuwa amerudi, yeye yule jana na hata milele. Alisema, “Paulo,” kwa maneno mengine, “Mimi ni Mungu yeye yule niliyekuwa jana. Mimi hapa, katika Nuru ile ile, ile Nguzo ya Moto ambayo Musa alizungumza nayo, kwenye kile kichaka kilichowaka moto.” Si ajabu angeweza kutenganisha sheria kutoka kwa neema, kwenye Kitabu cha Waebrania; alikutana na Nguzo ile ile ya Moto. Alisema, “Mimi ni Yesu, unayenitesa.”

²⁴⁷ Naye huyu hapa leo hii, kwa namna ile ile, kwa Nguzo ile ile ya Moto, akijidhihirisha Mwenyewe na kujithibitisha Mwenyewe vivyo hivyo, akiifunua siri ya Mungu ambayo imefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaiona?

²⁴⁸ Paulo alimjua tu—alimjua kwa ufunuo. Petro alimjua kwa ufunuo.

²⁴⁹ Alitembea pamoja Naye, akazungumza Naye. Kwa hiyo, unaweza kuketi katika Neno hili. Sasa, ndiyo kwanza niseme ya kwamba Yeye alikuwa Neno. Sasa, mwanachuoni anaweza kuketi chini na kulisoma Neno hilo mpaka anaweza tu kufunga mawazo yako kwa njia yoyote ile, unaona, kama akitaka kufanya hivyo, maana yeye ni mwerevu, ana akili. Hebu mchukue kasisi

wa Katoliki, ama, zaidi sana si huyo, kama mwanatheolojia mzuri sana, aliyefunzwa katika Biblia. Ndugu, Mbaptisti, ama Mpresbiteri, ama yeyote yule, atakufanya ufikiri ya kwamba hujui lolote, unaona, inapofikia kuzungumza. Ati nini? Unaona, kwa sababu kwamba amemjua katika mwili, Neno. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.]

250 Lakini njia pekee ya kuokolewa ni kwa kumjua Yeye kwa ufunuo!

251 Kama ninaweza kuchukua, ninaweza kuchukua fundisho la Kipresbiteri na kuwafunga ninyi Wapentekoste mpaka hamtajua. Ninaweza kuchukua fundisho la Kibaptisti na kuwaonyesha Wapentekoste mambo milioni moja ambayo hamjui lolote kuyahusu. Hiyo ni kweli, lakini hilo silo. Hilo silo Kanisa Lake. Hilo silo Kanisa Lake.

252 Kanisa Lake ni Yeye Mwenyewe akifunuliwa, (Amina! Mnaliona?) na kudhihirishwa na Neno Lenyewe, ya kwamba Yeye ni Mungu. Mnaona?

253 Mnawezaje kusema, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” basi, na kubatizwa hivyo? Wapagani! Kweli! Mnawezaje kusema mnamjua Yesu Kristo, Yeye ni Neno, wakati, hakuna Andiko katika Biblia, hakuna mahali ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”?

254 Na nyinyi—na nyinyi wa Yesu-Peeke, mkitumia jina tu “Yesu” kwa ubatizo! Mimi binafsi ninafahamiana na Yesu wanne au watano, mimi mwenyewe. Kwa hiyo mnaona kile ambacho madhehebu yenu yanawaelekezea? Hilo ni giza, udhihirisho wa Kaini, aliyeleta matunda badala ya damu. Mnaona?

255 Lakini ufunuo huja kupitia kwa Damu, mnaona, kupitia Yesu Kristo, Ambaye ni Damu ya Mungu, Damu umbaji katika tumbo la uzazi la Mariamu. Naye Paulo alimjua kwa ufunuo. Hivyo ndivyo tunavyomjua Yeye siku hizi, ndiyo njia pekee ungeweza kumjua. Unasema, “Mimi ni Mmethodisti.” Hilo halimaanishi kitu. “Mimi ni Mbaptisti.” Hilo halimaanishi chochote. “Mimi ni Mkatoliki.” Hilo halimaanishi chochote. Lakini kwa ufunuo, ya kwamba Mungu amekufunulia Neno! Yeye ni Neno. Nalo Neno, jinsi unavyojua limefunuliwa, linajiishi Lenyewe na kujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwako. Loo!

256 Makanisa yamesahau kwa mbali ufunuo huo mkuu. Hiyo ni kweli. Ufunuo wa Kweli, wameusahau. Waliendea . . .

257 Sasa, Luther alipoinuka, alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa na ufunuo wa siku hiyo. Lakini nini kilitokea? Kundi la akina Ricky lilingia, wakata nywele ubapa, vile tungekuita siku hizi, na Mariketa, na hao wote, walifika kule. Na—na—na, muda si muda mwajua, liko pale.

258 Udhihirisho huo. Laiti—laiti mngelijua numerojia ya Biblia, mpate kujua *Elvis* au—au *Ricky* yanamaanisha nini, kwa Maandiko! Uh-huh. Kama tu vile, kwa nini Yesu. . . Mnasema, “Halina kitu hilo, jina lako.” Ati halina? Jina hilo lingeweza tu kuja katika siku hizi za mwisho, kwa ajili ya watu hawa wa siku za mwisho.

259 Kwa nini Yesu akabadilisha jina la Abram kuwa Ibrahimu, kisha, Sarai likawa Sara? Kwa nini akambadilisha Sauli kuwa Paulo? Kwa nini akambadilisha Simoni kuwa Petro, na kadhalika? Unaona, bila shaka linamaanisha kitu fulani.

260 Jina hilo halingeweza kutamkwa mpaka siku hizi. Hiyo ndiyo sababu tuna jambo hili la kiwazimu tulilo nalo duniani siku hizi, kwa sababu ya mambo kama hayo. Jamii nzima ya binadamu imepotoshwa. I—imekwisha, mnaona, na ndiyo maana liko.

261 Angalia sasa, alikuwa sawa, alikuwa katika siku zake, Luther, naye alikuwa na ule ufundo; lakini mara alipoondoka, angalieni waliyofanya. Wesley alikuwa na ujumbe; angalia jinsi ulivyofanya. Maskini Wapentekoste wa kale walikuwa na ujumbe; angalieni walichofanya. Walikusanya kundi la watu pamoja, kama vile kitu kile kile hasa. . .

262 Mungu, kwa neema, aliwatumia Israeli Nguzo ya Moto, nabii, dhabihu, na kujionyesha miongoni mwao, na kuwatoa Misri, kuvuka Bahari ya Shamu. Nao walitaka sheria, kusudi wapate watu mashuhuri sana, wapate kuhusika juu yake. Basi walifanya nini? Waliachwa nyikani kwa muda wa miaka arobaini, kutangatanga, wala hakuna hata mmoja wa madhehebu hayo aliyewahi kuingia huko.

263 Kalebu na Yoshua, wale wawili pekee waliosimama na kusema, “Tunaweza kuiteka, kulitazama Neno la Mungu.”

264 Kila mmoja wao alikufia nyikani. Naye Yesu alisema wamepotea Milele, kweli, baada ya Yeye kuonyesha baraka na nguvu Zake katika nyakati zao; kama vile Luther, Wesley, na kadhalika. Sivyo?

Kasema, “Baba zetu walikula mana nyikani.”

265 Akasema, “Nao, kila mmoja, amekufa.” Yaani, wametengwa na Mungu Milele. Mizoga yao iliagamia nyikani. Mnaona? “Wamekufa. Lakini Mimi ndimi Mkate wa Uzima utokao kwa Mungu Mbinguni.” Wasingeweza kuliona. Kamwe wasingeweza kuliona.

266 Vema, kanisa limeisahau kwa muda mrefu. Walikubali ujumbe wa kiakili, wasomi, uanachama, maarifa, badala ya ufundo wa Ukweli wa Neno.

267 Sasa angalia hapa, wanasema siku hizi. Je, unaamini kwamba Mungu alitugiza kwenda ulimwenguni kote, na

kuwaponya wagonjwa, na kuhubiri Injili, na kutoa pepo? “Loo, loo, naam, nadhani hiyo ni sawa, lakini. . .” Unaona?

268 Mama mmoja, akiongea nami hivi majuzi, alisema, “Vema, makanisa yote yana uwiano.”

269 Nikasema, “Hakuna hata moja lililo na uwiano na lingine.” Kuna Wakatoliki wamesimama pale. Nikasema, “Na wewe je? Wewe ni Mmethodisti na yule ni Mkatoliki, je, mnapatana ninyi kwa ninyi?” Nikasema, “Papa huyu amekuja kuwaunganisha pamoja, hilo ni jambo jema kwa watu wa aina hiyo.”

270 Lakini Kanisa la Mungu halina uhusiano wowote nalo, hata kidogo. Limetoka kwa kundi hilo lote. Uh-huh. Kweli. Naam, bwana.

271 Mnataka kuunganisha hayo pamoja, na moja linaamini kitu *fulani* na kingine; Methodisti inachukua kunyunyizia, Baptisti inachukua kuzamisha, na yote mawili yakimkana Roho Mtakatifu katika utimilifu wa nguvu Zake. Walisema, “Tulimpokea Roho Mtakatifu *wakati* tulipoamini.”

272 Biblia ilisema, “Je, mmepokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?” Hiyo hapo tofauti. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona?

273 Nao wanasema, “Sisi ndio kanisa Katoliki. Tulianza mapema. Tulifanya *hivi*.” Wamethodisti wanasema, “Tumewekwa msingi juu ya Biblia.”

274 Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa ziko wapi? Uh-huh. Mnaona? Naam. “Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya,” kila kiumbe, kila mtu anayemwamini. Sasa liko wapi? Hayo ni Maneno Yake. “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitashindwa kamwe.” Sasa liko wapi? Mnaona? Loo, inaonyesha tu!

275 Ni nini? Ni hali ya kichotara. Angalieni hapa, hebu chukua punje kubwa nzuri ya mahindi ambayo ni chotara, nawe uchukue mahindi hayo chotara, ni mahindi mazuri. Lakini ukiyapanda, unapata nini? Shina dogo linatokeza namna *hii*, na kugeuka manjano na kunyauka kabisa. Hivyo ndivyo kila dhehebu lilivyo, wakati likiwa ni chotara, huku maneno ya mwanadamu yamechanganywa na Maneno ya Mungu. Litafikia kwenye ishara na maajabu, na yale Yesu aliyosema kuhusu kuamini Neno, ndipo litageuka manjano, na kusema, “Hatuwezi kulikubali Hilo,” na kurudi nyuma.

276 Kama tu vile wale wapelelezi wengine wote walivyofanya waliokwenda na kuipeleleza Kanaani. Walikuja kule na kusema, “Loo, tunaonekana kama panzi kando yao! Hatuwezi kuwashinda! Waamaleki watafanya, hawa wote, kile watakachofanya!” Nao wakarudi nyuma.

277 Ndipo Kalebu na Yoshua, wakiwa ukoo safi, amina, kwa Neno la Mungu, walijua Mungu alisema, “Nimewapa nchi hiyo.” Wakasema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuitwaa!”

278 Inategemea umezaliwa wapi. Kama umezaliwa kwa Neno la Mungu, Neno la Mungu lina utangulizi katika Kanisa Lake. Hilo ndilo alilolifia. Hilo ndilo kusudi Lake, apate kufanikisha, kuwa na utangulizi Wake akifanya kazi katika Kanisa Lake. Hebu Neno la Mungu liangaze, kwanza, haidhuru kitu kingine chochote kinaonekanaje. Sijali kama wasomi wanasema *hili, lile, linginelo*, halina uhusiano wowote Nalo. Neno la Mungu lilisema hivyo, nasi tunaweza hata na zaidi kulichukua!

279 “Kama nikihubiri hilo kanisani mwangu,” mhudumu mmoja aliniambia, kasema, “ningehubiria nguzo nne kanisani.”

280 Nikasema, “Ningehubiria hizo.” Naam, bwana. Neno la Mungu lilisema hivyo. Tunaweza kufanya hivyo. Mungu alisema tufanye hivyo. Amina!

281 Loo, naam, wanajitolea udhuru kwa jambo hili. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu wao ni vipofu kwa Ujumbe wa wakati wa mwisho, siku hizi za mwisho, wakati Mungu anajithibitisha Mwenyewe. Wanajaribu kuliainisha kama aina fulani ya mizimu, ama, loo, (ningeliitaje?) jambo la kiakili, udanganyifu, ama kitu fulani cha namna hiyo. Mnaona, wao—wanajaribu kulifanya kitu kingine lisicho.

282 Kama tu walivyofanya alipokuwa hapa, wakati Yesu alipokuwa hapa, walimwita “Beelzebuli; mpiga ramli,” sasa wanasema ni kitu kama telepathia ya kiakili. Mnaona? Wakati, wao wanajua ya kwamba Yeye angeweza kusimama pale na kuwatazama watu na kuyatambua mawazo hasa yaliyo moyoni mwao. Biblia ilisema hivyo.

283 Vema, si Waebrania mlango wa 4, inasema, “Neno la Mungu ni jepesi, tena lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, tena laweza kuyatambua mawazo ya moyoni”? Naye alikuwa ndiye Neno hilo. Na Neno hilo linapokuwa na utangulizi ndani ya mwanadamu, jambo lile lile linatukia tena, kwa maana ni Neno! Amina! . . . Tazama jinsi unavyoweza kujikwaa juu ya hili tangu sasa. Hapo ni wazi kabisa. Mnaona? Vema.

284 Hiyo ndiyo sababu wao ni vipofu, sawa sawa na ilivyokuwa katika zile siku Kristo alipokuwa duniani. Loo, jamani! Wanayumbayumba vivyo hivyo. Wao walisema, “Yeye ni Beelzebuli. Beel- . . .” Waliona angeweza kufanya hivyo, kwa hiyo wakasema, “Yeye ni . . . Alizaliwa mwana haramu, na kidogo ni mtu wa kipekee. Amepagawa tu na ibilisi fulani. Yeye ni—yeye ni Msamaria kule, naye ana pepo ndani yake. Hivyo ndivyo anavyofanya hivyo.”

285 Yesu akasema, “Nitawasamehe hilo,” mnaona, kuliita Neno la Mungu, kazi za Mungu, pepo mchafu. Akasema, “Nitawasamehe hilo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja,

wala neno moja dhidi Yake kamwe halitasamehewa, katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao, wala Siku ile kuu. Halitasamehewa.” Kwa hiyo, mnaona, hilo limeandikwa dhahiri katika Maandiko.

²⁸⁶ Basi watu watakapoifikia Siku hiyo, haidhuru ni wasomi jinsi gani, na jinsi dhehebu lao lilivyo kubwa, limehukumiwa. Hawana budi kuhukumiwa! Wamemkufuru Roho Mtakatifu, wakimwita “mtakatifu anayejifingirisha” na kitu kingine ambacho kilikuwa na jina lisilopendeza, ama kitu kama hicho. Na Kanisa la Mungu lilipaswa kuvumilia wakati huo wote.

²⁸⁷ Hata Paulo, mbele ya Agripa, alisema, “Kwa njia inayoitwa ‘uzushi,’” ambalo linamaanisha “kichaa,” “hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.” Ilimbidi mwanachuoni huyo mashuhuri kufikia mahali hapo, “kwa njia inayoitwa ‘uzushi.’”

²⁸⁸ Kwa nini? Ilifunuliwa kwake. Ile Nguzo ya Moto ikining’inia mbele yake, kasema, “Mimi ni Yesu, yule Mungu mkuu aliyekuwa kule jangwani pamoja na Musa. Mimi Ndimi, na ni vigumu kwako kupiga teke mchokoo.”

²⁸⁹ Ndipo Paulo akiwa amesimama pale, alijua ya kwamba maisha yalikuwa hatarini, akasema, “Njia iitwayo ‘uzushi,’ ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.” Iliitwa hivyo. Kwa sababu ilifunuliwa kwake vile ile Kweli kuu ya Kristo ilivyokuwa.

Na siku hizi, watu wanasema, “Ni dhehebu.”

²⁹⁰ Ni Yesu Kristo, Kuzaliwa upya, akifunuliwa ndani yako, ya kwamba Yeye ana utangulizi, apate kueleza Maneno Yake. Na chochote ambacho ameahidi katika siku hizi za mwisho, Yeye anaweza kukitimiza, kupitia kwa Mwili Wake anapofanya kazi. Amina! Ni Neno la Mungu hasa likidhihirishwa. Angalieni. Sawa.

²⁹¹ Sawa sawa na katika siku za Kristo, Mungu anashikilia ufunguo wa ufunuo huu wa Kristo, Mwenyewe. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Shule za theolojia haziwezi kamwe kuupata. Yesu alisema hivyo. Ukitaka kulisoma sasa, katika Mathayo Mtakatifu 11:25 na 27. “Nakushukuru Wewe, Baba, Mungu wa mbingu na nchi, kwa kuwa umelificha machoni pa wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga ambao watajifunza.” Mnaona? Mnaona? Sijali. . .

²⁹² Waangalie hao wasomi wa siku hizo, hao Wayahudi, watu wazuri sana, madhehebu yao ya Mafarisayo, Masadukayo, na Maherode, na chochote wanachoweza kuwa. Mnaona? Madhehebu yao yote makuu, ndipo Yesu akasema, “Ninyi ni vipofu; mnaongoza vipofu. Isaya alisema vema juu yenu, ‘Mna masikio, wala hamwezi kusikia; na macho, hata hamwezi kuona.’ Maana, Isaya alisema hili katika Roho, kwa hiyo Mungu wa Mbinguni ameyapofusha macho yenu. Mnafanya kama Hawa

alivyofanya, kukubali upande wa kiakili, pasipo kujua lolote juu ya Roho wa Mungu. Kwa hiyo, wote si wataanguka shimoni, kiongozi na kipofu, pia?” Huyo kiongozi ataanguka pamoja na kipofu, maana yeye ni kipofu pia. Kiongozi anaanguka, ambaye ni kipofu, akimwongoza kipofu, wote wawili wanaanguka shimoni.

²⁹³ Naye Mungu pekee ndiye anayeshikilia ufunguo huu! Alidhihirisha jambo lile lile katika Maandiko ya awali pale muda mfupi uliopita nilipoyasoma, aliposema, “Watu husema mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

²⁹⁴ Ndipo Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

²⁹⁵ Akasema, “Heri wewe Simoni, mwana wa Yona. Mwili na damu havikukufunulia hili. Baba Yangu aliye Mbinguni! Juu ya ufunuo huu hapa, peke yake, nitalijenga Kanisa Langu. Malango ya kuzimu hayatalishinda kamwe.” Mnaona? Sasa mnaona?

²⁹⁶ Kwa hiyo basi hakuna shule, hakuna wanatheolojia, hakuna mafundisho ya Biblia miongoni mwa shule yoyote, wanaojua lolote kulihusu. Hawawezi kujua lolote juu Yake. Haiwezekani kwao kujua lolote juu yake. Mungu ameficha hizo hisia, za kulijua Hilo, kutoka kwa waalimu waliochaguliwa hasa na chochote kile.

²⁹⁷ Ni jambo la kibinafsi, la mtu binafsi na mtu huyo, kwamba Kristo anafunuliwa kwao.

²⁹⁸ Na kama ukisema, “Amefunuliwa kwangu,” halafu Maisha ambayo Kristo alitoa hapa katika Biblia, Uzima uo huo ulio ndani Yake, haujitokezi Wenyewe ndani yako, basi una ufunuo mbaya.

²⁹⁹ Kama nikiweka uhai wa mboga ndani ya uhai wa mpera, ungezaa maboga. “Kwa matunda yao mtawatambua.” Hasa kabisa. Na kama wa kwanza . . . ukiweka mti nje, mzabibu, nao utoe kichala cha zabibu; chipukizi la kwanza lililochipiza, lilitoa zabibu, la pili likatoa malimau, na lingine likatoa peasi, linalofuata likatoa matofaa, kuna kitu cha kupandikiza mle, ambacho kinazaa uhai wake chenyewe. Kila dhehebu litazaa uhai wake lenyewe. Lakini kama mzabibu huo asilia ukitoa chipukizi lingine, litazaa zabibu kama ulivyofanya mara ya kwanza.

³⁰⁰ Na kama Uhai—Uhai wa Yesu Kristo kamwe ukitoa mwili mwingine wa waaminio, utazaa tunda ambalo ule wa kwanza ulizaa. Wataandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, maana ni ule ule, Uhai ule ule. Mnaona ninachomaanisha? Huwezi tu kujiepusha nayo. Ni Uhai wa Kristo ndani yako, umeingizwa ndani yako, na Roho Mtakatifu Mwenyewe akiyaishi Maisha Yake kupitia kwako.

301 “Viongozi vipofu wa vipofu!” Angalieni, Mungu anao ufunguo huu, peke yake. Hakuna mwanatheolojia anayeweza kukwambia; Hiyo haijulikani. Imefichwa kwao. Hawajui lolote juu Yake.

302 Kwa hivyo hizo shule, unaposema, “Nilipata Ph., LL.D.,” unafanya tu... Kwangu mimi, na, ninaamini, na kwa Mungu na kwa mwaminio yeyote wa kweli, hiyo inamaanisha kuwa uko mbali hivyo, ulirudi tu nyuma. Mungu hajulikani kwa elimu. Yeye hajulikani kwa jinsi ya kulifafanua.

303 Mungu anajulikana kwa urahisi na kwa ufunuo wa Yesu Kristo kwa mtu asiyejua kusoma na kuandika kabisa. Unaona? Sio theolojia yako. Ni ufunuo wa Yesu Kristo. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Hakuna miamba mingine inayokubalika, hakuna vitu vingine vinavyokubalika, hakuna mwamba mwingine wa Kirumi, hakuna mwamba mwingine wa Kiprotestanti, hakuna shule nyingine, hakuna kitu kingine chochote, ila juu ya ufunuo kamili wa Yesu Kristo kupitia Kuzaliwa upya. Yeye huzaliwa mle ndani, Naye anaumimina Uhai Wake Mwenyewe, na uhai wako umetoweka. Nao Uhai wa Kristo unajidhihirisha Wenyewe kupitia kwako, pamoja na utangulizi, kwa watu; hata wanaona Uzima wenyewe, na kazi, na ishara, na maajabu, aliyofanya, anafanya jambo lile lile kupitia kwako. Mbali na hayo, mengine yote hata hayakumbukwi, hata kidogo. Tazama ufunuo mkuu wa Mungu ukitokea!

304 Ukosefu wa ufunuo huu ndio maana tuna migawanyiko mingi mbali mbali kati yetu, na dhihaka chungu nzima. Migawanyiko mingi sana miongoni mwetu, ni kwa sababu watu wanakosa huo ufunuo. Mnaona, wanaukosa ufunuo huo, waalimu.

305 Paulo, baada ya ufunuo wake mkuu wa Kristo, alisema, katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa pili. Hakikisheni mnalisoma hilo mnapoliandika. Angalieni! Loo! Yeye alisema, “Sikuja kwenu kwa hekima.” Mwangalieni mtu huyo ambaye kweli alikuwa na hekima, ama, mwangalieni huyo mtu aliyekuwa na elimu, “Sikuwajia na maneno kama hayo.” Wakorintho wa Kwanza, mlango wa pili wa Wakorintho wa Kwanza. Loo, natamani...

306 Vema, hebu tulisome tu. Vipi... Je, mnaweza kusimama kwa dakika moja na tusome kifungu kimoja au viwili tu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ningependa tu kulisoma ili ha—hamtaninii... Ingewafanya hata watu kwenye kanda kurejea kwake, kwa vyovyote vile, kuwapa nafasi.

307 Wakorintho wa Kwanza, mlango wa pili. Msikilizeni mtume huyu mashuhuri hapa, Paulo, mtumishi wa Mungu mwenye elimu. Hebu tuangalie hapa.

...Mimi, Paulo, *nilipokuja kwenu, sikuja kwa ufasaha wa maneno...kwa hekima, nikiwahubiri ninyi*

ushuhuda wa Mungu. Sikuwahi kusema mimi—mimi ni Dk. Nanii. Mnaona?

Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa.

Nami nalikuwa kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi.

. . .hotuba yangu na—na kusihi kwangu hakukuwa kwa maneno kushawishi hekima ya watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu. . . za nguvu.

308 Hapo, mnaona, hiyo hapo Injili. Mnaona? Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Hakusema, “Enendeni mkafundishe.” Alisema, “Enendeni mkahubiri.” Kwa maneno mengine, “Dhihirisheni zile nguvu, na ishara hizi zitafuatana na hao.” Kufundisha tu hakutoshi. Inahitaji Roho Mwenyewe akionyesha ishara hizi. Mnaona? Sikilizeni hili.

Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

309 Loo, jamani! Mnaona, kumbadilisha huyo mtu! Sio katika yale ninayoweza kuelezea vinginevyo, na kusema, “Yeye si yule yule,” wakati Yeye ni yule yule. Nikifanya hivyo, inaonyesha, kwangu mimi, ni—ni. . . Hakika, mtu akiniambia hivyo, angenionyesha kuwa hana ufunuo, ule ufunuo wa Mungu wenye sehemu tatu. Mnaona? Sasa, na. . .

Walakini katika udhaifu. . . miongoni mwenu walio wakamilifu: ila si kwa hekima ya dunia hii, bali ya wanaoitawala dunia hii inayobatilika:

Bali twanena hekima ya Mungu katika. . . siri, (mnaona, siri ya Mungu yenye sehemu tatu) ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliazimu tangu milele kwa utukufu wetu:

Ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja: hakuna hata mmoja wa makuhani, rebi—marabi. . . (samahani). . . au chochote, aliyejua chochote juu yake; kwa maana kama wangelijua, hawangalimsulubisha Bwana wa utukufu.

310 Ulisema, “Umekosea kuhusu marabi na wahubiri hapo.” Ni nani aliyemsulubisha? Uh-huh.

311 Loo, na kuendelea na kuendelea, tungeweza kwenda. Yasomeni, mnaona, endeleeni mbele, mwokoe wakati, maana tuna ninii tu. . . Sio kuchelewa bado, lakini tunayo mengi tu hapa ya kusema kama Bwana atatusaidia. Sasa, ukosefu wa hii, sasa. . .

312 Naye Paulo, mtu huyu mkuu wa elimu, kamwe hakujaribu kueleza maneno yake makuu ya kitheolojia juu ya watu. Alilikubali Neno la Bwana kwa unyenyekevu, naye akaliishia

Neno hata likadhihirika kupitia kwake. Aliishi mtauwa sa—sana hata wakamwona Yesu Kristo ndani yake, sana, hata wakataka lesu yake, kuichukua na kuiweka juu ya wagonjwa. Huo hapo Uzima wa Kristo.

³¹³ Sasa watazameni wengine wakisema, “Loo, vema, unaona, Eliya alifanya hivyo, muda mrefu uliopita, aliweka fimbo yake; lakini, loo, hizo zilikuwa siku za Eliya.” Sasa, ulimwengu ulifikiria hayo. Makuhani wasomi na kadhalika, na makanisa ya siku hizo, walifikiria hilo.

³¹⁴ Lakini kwao waaminio, walijua vinginevyo. Waliona ufunuo wa Kristo ulikuwa ndani ya Eliya, kitu kile kile kilichokuwa ndani ya Paulo, kikionyesha Maisha ya namna iyo hiyo, maana yeye alikuwa nabii. Mnaona? Alitabiri mambo yaliyotukia jinsi yalivyokuwa, nao walijua huo ulikuwa ni utambulisho wa Mungu kwa nabii. Nao walijua ya kwamba alikuwa nabii wa Mungu. Usingeweza kuwatikisa kutoka kwake, hata kidogo. Hata walipomwona Petro akitabiri mambo hayo yaliyotimia, walisema, “Acha tu kivuli chake kipite juu yangu.” Amina! Hilo ndilo Kanisa. Hao ndio wanaoliamini. Naam, bwana. Ilifunuliwa na . . .

³¹⁵ Kwa nini Paulo alisema, “Kwa sababu ni—nina Ph., LL.D., kadhalika, wananiamini? La,” alisema, “Nilisahau mambo hayo yote, hekima ya mwanadamu,” kasema, “ilinibidi kufa, nami ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, hilo ndilo nililokuja kwenu nalo, kwa udhihirisho wa nguvu za Mungu?”

³¹⁶ Ilikuwa ni nini? Kumfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele. Kazi zile zile alizofanya Yesu, Paulo alifanya zizo hizo. Nao wakamwona Mungu, yule Baba mkuu ambaye alikuwa amedhihirisha kwenye kichaka kilichowaka moto, alikuwa amelidhihirisha kwa Paulo, na hapa lilikuwa likidhihirishwa.

³¹⁷ Naye ni yeye yule katika kila wakati. Njia ya Mungu yenye sehemu tatu, “jana, leo na hata milele.” Ati nini? Mkombozi; katika Kanisa Lake; utangulizi katika Ufalme ujao. Amina! Mnaiona? Kamilifu tu iwezekanavyo!

³¹⁸ Loo, angalieni! Roho Mtakatifu ndiye Mfunuaji pekee wa ufunuo wa Kiungu wa Kristo. Hakuna shule inayoweza kufanya hivyo. Hakuna msomi anayeweza kufanya hivyo. Hakuna mwanadamu, awe ameelimika vizuri kiasi gani, awe mcha Mungu kiasi gani, ama chochote kile, hakuna mwanadamu awezaye kufanya hivyo.

³¹⁹ Ningeweza kuchoma kwa nguvu hapa. Ni wangapi walio Wakristo, waliozaliwa mara ya pili; inueni mikono yenu, waliojazwa na Roho Mtakatifu? Vema. Haya basi. Vema. Angalieni.

³²⁰ Naye atafanya hivyo tu kwa waliochaguliwa tangu zamani. Hiyo ni kweli kabisa. “Wote alionipa Baba watakuja, wala

hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa Baba amenipa Mimi kwanza.” Mnaona?

³²¹ Waangalie hao makuhani, wakisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni ibilisi.”

³²² Na maskini mwanamke huyo akitembea huku na huko, akiishi na waume sita; alikuwa akiishi na watano, na alikuwa na wa sita wakati huo. Ndipo Yesu akasema, “Nenda kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

³²³ Kasema, “Naam, unao sita. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

Akasema, “Bwana!” Nini? Nuru hiyo iliigusa hiyo Mbegu.

³²⁴ Iipowagusa hao makuhani, walisema, “Mtu huyu ni mpiga ramli.” Unaona, hamna Uzima hapo. Chotara, kuja hadi kwenye dhehebu, lakini wakafa tangu hapo na kuendelea.

³²⁵ Lakini mwanamke huyu hakuwa chotara. Kasema, “Bwana, naona!” Ninaweza kuona macho yake makubwa mazuri yaking’aa namna hiyo, machozi yakitiririka mashavuni mwake. Kasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Ninamtafuta Masihi. Na ajapo huyo Masihi, Yeye atafanya jambo lili hili. Atatwambia mambo haya.”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

³²⁶ Ee Bwana! Akaacha mtungi wake. “Huyu hapa! Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo.” Ilikuwa ni nini? Nuru hiyo iliigusa Mbegu hiyo. Uhai huo ulikuwepo. Ukatokea.

Jambo lile lile leo!

³²⁷ Lakini mwanatheolojia atasema, “Sasa hebu kidogo. Nitaona kama *Nanii*, Mchungaji Moody alisema, ama . . .”

³²⁸ Mchungaji Moody ana uhusiano gani na hili, leo hii? Mchungaji Moody aliishi katika siku zake, lakini sio sasa. Hakika. Luther aliishi katika siku zake, lakini sio katika siku ya Wesley. Wesley aliishi katika siku zake, sio katika siku ya Pentekoste. Wapentekoste waliishi katika siku zao, lakini wako mbali sana na Hili katika saa hii. Tuko katika majira ya mwisho. Hakika.

³²⁹ Madhehebu yao, na mahangaiko, huthibitisha ya kwamba Hilo halipo. Neno halijawahi kuthibitishwa kwa usahihi; ni kwa nguvu Zake tu. Mbegu, madhehebu . . . Nao wangeunda dhehebu, kisha kuweka maskini hizo mbegu za magugu sumu pamoja na hiyo ngano halisi; ikafa papo hapo. Mazao yakaenda kwenye magugu sumu, kweli, mbigili kijani na magugu miiba, uh-huh, mnaona, yakarudi huko. Ikafa moja kwa moja. Kisha wakalima shamba na kuanza tena, wakapanda Mbegu halisi, na baadhi yazo zikachipuka, zikaisonga.

³³⁰ Lakini basi, Mungu alisema, katika siku hizi za mwisho angewatoa watu waliooshwa katika Damu Yake, nao walichaguliwa tangu zamani kuwa huko. Hawana budi kuwepo. Mungu alisema hivyo. Na ingefunua... Na ishara yenyewe, “nitawape-...” Malaki 4, na kile ambacho angefanya, “kurejesha tena,” kurudisha, katika siku za mwisho, mambo haya makuu aliyoahidi, yangeleta ufunuo. Ni nini... Atafanya nini, Malaki 4? Ilikuwa ni kurudisha Imani ya baba, kwa watoto. Mnaona? Hiyo ni kweli, kuleta kitu kile kile, Nguzo ile ile ya Moto, jukwaani; ishara zile zile, maajabu yale yale, Yesu yule yule; ikimfanya yeye yule, kumhubiri yeye yule, kumthibitisha yeye yule jana, leo, na hata milele.

³³¹ “Nitarudisha,” asema Bwana, “miaka yote ambayo mdudu wa Methodisti, na mdudu wa madumadu, na Mbaptisti, na Mkatoliki; na hao wadudu wote waliila imani hi—hiyo wakaimaliza,” mpaka ikawa kisiki cha kimadhehebu ambapo hamna mbegu zilizosalia mle. “Lakini nitarudisha tena,” asema Bwana, “miaka yote.” Ati nini? “Ishara zote na maajabu ambayo wameyaacha. Nitairudisha moja kwa moja kwenye ule Mti wa asili tena, nami nitaaurudisha,” asema Bwana. Nabii huyo alikuwa nabii aliyethibitishwa. Maneno yake hayana budi kutimia. Amina.

³³² Roho Mtakatifu, pekee, ndiye Mfunuaji wa ufunuo wa Kiungu wa Kristo, na amekuwa hivyo katika nyakati zote. Kumbukeni, nyakati zote! Neno la Bwana lilikuja kwa nani? Nabii, peke yake. Hiyo ni kweli. Je, hiyo ni kweli? Naye nabii ilimbidi kuthibitishwa, kwanza. Si kwa sababu alisema yeye alikuwa nabii; kwa sababu alizaliwa nabii, akathibitishwa kuwa nabii, na kila kitu alichosema kilikuwa kwenye Neno hasa na kikatimia, basi mengine yote yaliachiliwa. Mnaona? Lilikuwa, Neno la Bwana lilikuja tu kwa Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, “Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, unaona, waliandika Neno.”

³³³ Angalieni. Yohana Mbatizaji asingalimjua Yesu kama si Roho Mtakatifu kumwonyesha. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³³⁴ Yohana Mbatizaji, yule nabii mkuu aliyetokea, na kusema, “Kuna Mmoja anayesimama kati yenu sasa hivi. Na Mtu wa kawaida anayesimama hapa mahali fulani, huyo ndiye Mwana-Kondoo wa Mungu.” Yohana alisema, “Basi nilishuhudia. Ninashudia. Nilimwona Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, akishuka kutoka Mbinguni kama hua, Naye akaenda juu Yake. Ndipo Sauti ikasema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependezwa naye.’”

Ilikuwa ni nini? Roho Mtakatifu alisema, “Nitamtambulisha.”

335 Hiyo ndiyo njia pekee utakayomjulia siku hizi, njia pekee utakayopata ufunuo wa Mungu wenye sehemu tatu, ni kwa Roho Mtakatifu. Na njia pekee inayoweza kuwa, ni kwamba umechaguliwa tangu zamani kuliona. Asipokuonyesha, hutawahi kuliona. Ikiwa hujachaguliwa tangu zamani kuliona, hutalionna kamwe; maana Nuru hiyo inaweza kumulika nawe utaondoka na kuidhihaki, na kuelezea vibaya, kwa dhana fulani za kiakili. Wakati Mungu yule yule, Mwenyewe, alijidhihirisha Mwenyewe na kulithibitisha, mnaona, lakini, kama hujapewa kuliona, hutalionna.

336 Mungu hakusema tu, “Nitamchagua *huyu*, nimchague *yule*,” bali Yeye alijua kwa ninii Yake... Sababu ya Yeye kuweza kukusudia tangu zamani, ni kwa kuwa Yeye hana kikomo, na Yeye—Yeye anajua kila... Yeye hana kikomo, kwa hiyo basi alijua kila kitu. Alijua mwisho, na angeweza kujua mwisho tangu mwanzo. Yeye ni Mungu. Kama hawezi kufanya hivyo, Yeye si Mungu. Naam, bwana. Yeye hana kikomo. Vema.

337 Yohana hangemjua kamwe, la, bwana, kama Roho Mtakatifu hakumtambulisha. Unaona jinsi Mungu anavyoificha siri Yake kwa walio juu, wenye elimu na kadhalika? Angalieni, kila mmoja wa hao watu akisema... kwa urahisi hulifunua kwa yule ambaye amemchagua tangu zamani kuliona. Angalieni hapa! Wengine wakisimama na hata hawakumwona yule hua, hawakusikia Sauti yoyote, kwa maana ilitumwa tu kwa hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani. Ilichaguliwa tangu zamani! Bila shaka, ilichaguliwa tangu zamani!

338 Mbona, Isaya, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, katika Roho, aliinuka kutoka katika hisi hizi za kibinadamu, na kusema, “Kuna sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Bwana, na kuyafanya ninii Yake...’”

339 Basi, kama Isaya angeweza kuliona, hivi Malaki hangeweza kuliona jambo lile lile akiwa nabii wa mwisho aliychaguliwa tangu zamani, kule kutiwa muhuri kwa manabii wote wa Agano la Kale, huyo mkuu... nabii huyo mkuu aliyesimama pale mwishoni mwa wakati? Unaona? Anasema amechaguliwa tangu zamani. Bila shaka, alichaguliwa. Malaki alimwona, pia.

340 Yesu alisema, “Ikiwa mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa habari zake, ‘Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu,’ Malaki 3, ‘kuitengeneza njia mbele Yangu.’” Mnaona? Hakika, alichaguliwa tangu zamani kuuona ujumbe huo. Si ajabu aliweza kutazama kule na kumwona huyo Hua akishuka, ile Nuru iliyokuwa nyikani pamoja na Israeli, ikija, ikishuka chini.

341 Mungu mwenyewe, akisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependeza kukaa ndani Yake.” Mungu na mwanadamu wakiwa Mmoja.

342 “Ninashuhudia,” Yohana alisema, “Nilimwona, Mwana wa pekee wa Baba. Mimi ni shahidi wa hilo.” Amina!

343 Haya basi. Urahisi! Akiwa na mhubiri mzee, baba yake; baba yake alikuwa mwanatheolojia mashuhuri, mnajua, alitoka shuleni. Inaonekana kana kwamba angerudi kwenye madhehebu ya baba yake. Hayo hayangekuwa mapenzi ya Mungu.

344 Wakati Mungu alipomgusa wakati wa kuzaliwa kwake kule nyuma, naye akampokea Roho Mtakatifu miezi mitatu kabla hajazaliwa. Naam, bwana. Wakati Mariamu alipokwenda kule, naye mtoto Yohana alikuwa na umri wa miezi sita, katika tumbo la uzazi la mama yake, wala kamwe hakuwa... Hiyo misuli midogo ilikuwa haijasogea bado. Ndipo Mariamu akahofu... Ile Misuli midogo ilikuwa inakua, lakini asingeweza kuhisi uhai wowote, Elisabeti, mama yake, hasa. Ndipo Mariamu alipokuja na kumshika, na kumkumbatia, akaweka mikono yake, akaweka mikono juu yake. Mnaona? Akasema, “Mungu amesema nami, nami nitapata Mtoto mchanga, pia.”

“Kwani wewe na Yusufu mmefunga ndoa?”

“La.”

“Mariamu, hii inawezekanaje?”

345 “Roho Mtakatifu atanitia uvuli, na ndani yangu kutaumbwa. Nami nitaita Jina Lake ‘Yesu.’ Atakuwa Mwana wa Mungu.”

346 Na mara tu Neno hilo ‘Yesu’ lilipotajwa, maskini Yohana akaanza kurukaruka, na kupaza sauti, na kuruka huku na huko katika tumbo la uzazi la mama yake.

347 Akasema, “Ahimidiwe Bwana Mungu! Kwani mama wa Bwana wangu ametoka wapi?” Mama wa Bwana wangu! Loo, jamani! “Ametoka wapi mama wa Bwana wangu? Kwa maana, mara sauti ya kuamkua kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto changu kichanga kiliruka ndani ya tumbo langu kwa shangwe.”

348 Si ajabu hakutaka seminari yoyote, kitu cha kumtia kasumba kwa kitu fulani, kingine. Alikuwa na kazi muhimu. Alikuwa mtu wa nyikani, alitoka akaenda nyikani na kungoja. Mungu alimwambia huko nje, kasema, sasa, na kumfunulia. Loo, huo hapo ufunuo wako tena! “Nami nitawaambia Yeye ni Nani. Wewe ni nabii. Neno ni kwa ajili yako. Unajua wewe ni nani. Huna budi kuja.” Hilo linajibu swali la Jumapili iliyopita. Mnaona? “Unajua wewe ni nani, Yohana. Tulia; usiseme lolote. Nenda huko nje. Na utakapomwona Huyu, kutakuwa na ishara ikija kutoka Mbinguni, kama Nuru, hua atashuka. Huyu atakuwa Ndiye utakapomwona.”

349 Hiyo ndiyo sababu, wakati Yesu alipotoka majini, Yohana alitazama na akamwona huyo hua akishuka, akasema, “Tazama Mwana-kondoo wa Mungu! Huyu hapo! Ndiye atakayeondoa dhambi ya ulimwengu.”

350 Yesu akatoka moja kwa moja majini, akamwendea. Hayo macho mawili ya Yohana yakakutana na macho mawili ya Yesu. Walikuwa binamu wa pili, kimwili. Mariamu na Elisabeti walikuwa binamu wa kwanza. Macho yao yalikutana. Huyu hapo Mungu na nabii Wake, amina, wamesimama hapo.

351 Yohana akasema, “Nina haja ya kubatizwa na Wewe. Kwa nini Wewe waja kwangu?”

352 Yesu akasema, “Kubali iwe hivyo sasa, lakini, kumbuka, hivyo ndivyo imetupasa kutimiza haki yote.”

353 Kwa nini Yohana akafanya hivyo? Kwa sababu Yeye alikuwa ni Dhabihu. Yohana alikuwa nabii, alijua; nayo Dhabihu haina budi kuoshwa kabla haijatolewa. Loo! Loo! Naye akamruhusu, na akambatiza.

354 Basi alipofanya hivyo, tazama, Mbingu zikafunguka, loo, jamani, na huyo hua akashuka juu Yake, ndipo Sauti ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependeza kukaa ndani Yake.” King James inasema, “Ambaye nafurahia kukaa ndani Yake.” Kwa hivyo ni njia yoyote unayotaka kuligeuza, kitu kile kile, “kukaa ndani,” au . . . “Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye ninapendeza kukaa ndani Yake,” au, “kukaa ndani,” vyovyote unavyotaka kuliweka, kitu kile kile. Vema.

355 Tunaona basi ilifunuliwa kwake. Wengine waliosimama hapo hawakusikia chochote kuhusu hilo. Roho Mtakatifu, peke yake, hulifunua.

356 Vivyo hivyo wakati alipojifunua Mwenyewe kwa Paulo, Mzao mwingine aliyechaguliwa tangu zamani.

357 Kulikuwa na Paulo akizunguka, huenda alisema, “Nikilishika kundi hilo, nitawararua vipande vipande, kwa sababu mimi ni Dk. Sauli. Nilikuja chini ya Gamalieli. Ninatoka kwenye ninii ya Biblia ya Moody . . .” ama mwingine, mnaona. “Mimi, mimi ni msomi. Ninajua ninachozungumzia. Nitalirarua kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha vipande vipande. Nami nakwambia, baba mkubwa mtakatifu, nipe tu ruhusa ya kwenda kule, nami nitamkamata kila mmoja wa hao wapiga kelele kule chini. Upuuzi huu wote wa uponyaji wa Kiungu, tutaukomesha.”

Akaiweka mfukoni mwake, akasema, “Ninashuka kwenda zangu.”

358 Na siku hiyo, jamani, yapata saa tano mchana, Nu—Nuru ikamulika usoni mwake, akaanguka chini.

359 Kwa nini? Alikuwa ni Mzao aliyechaguliwa tangu zamani. Mungu akasema, “Nimemchagua. Naam. Nami nitamwonyesha yaliyo mengi atakayopitia kwa ajili ya Jina Langu. Nitamtuma kwa Mataifa, nao watamfedhehi kwa kila njia wawezayo ku—kumfedhehi, lakini hata hivyo atalibeba Jina Langu.”

³⁶⁰ Paulo akashuka, basi, mpaka mambo yake yote ya kikanisa yakakatiliwa mbali, huko chini upande wa nyuma ya jangwa, kwa miaka mitatu na nusu. Huko chini Uarabuni, mpaka alipojifunza Neno, nalo Neno likawa yeye. Naye akawa mfungwa; huyu hapa akirudi amefungwa minyororo ya upendo! “Ujuzi wangu wote wa seminari umekwisha! Mimi ni mfungwa wa Yesu Kristo. Amina! Filemoni, ndugu yangu, mimi ni mfungwa wa Yesu Kristo. Ninaweza tu kuongea na kusema kile Yeye anachoniambia.”

³⁶¹ Mungu anahitaji wafungwa leo ambao utajifunga mwenyewe kwa mapenzi Yake, kwa Neno Lake.

³⁶² Hivyo ndivyo Paulo alivyokuwa. Haidhuru alikuwa amejifunza kiakili kiasi gani, alikuwa amemjua Mungu kwa ufunuo. Naam, bwana. Wasomi walipoteza kazi kabisa, ufunuo ulipokuja; ambao, juu ya ule mwamba Kanisa limejengwa. Naam, bwana. Angalia, yeye alikuwa ni Mzao aliyechaguliwa tangu zamani.

³⁶³ Roho Mtakatifu, peke yake, anakuonyesha Yeye ni Nani. Hakuna mtu; watakufanyia “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” na chochote kile, kutoka kwake. Unaona? Lakini Roho Mtakatifu atamfunua kama Bwana Mungu wa Mbinguni aliyedhihirishwa, ya kwamba huyo ni, loo, Yeye!

³⁶⁴ Sasa angalieni. Si manabii, si wafalme, si kitu kingine chochote; lakini hapa, kwa mara ya kwanza, Mungu alifunuliwa katika Kristo, katika utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, katika mwili wa kibinadamu. Huo ndio ufunuo. Loo, jamani! Nitawaimbia ubeti sasa:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka, (Sivyo?)

Ishara walizotabiri manabii;

Mataifa (kanisa katika dhehebu,) siku zao zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;

“Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.”

(Mmefukuzwa kutoka kwao.)

Siku ya ukombozi imekaribia,

Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;

³⁶⁵ Vichekesho vyao vyote vya Hollywood haviyafuniki. Kama mvulana mdogo anayepiga mbinja, akipita makaburini usiku. Unaona?

Jazweni na Roho, taa zenu zikiwa zimesafishwa na kuwa safi,

Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya, Neno la Mungu wanalikana,

Kwamba Yesu Kristo ndiye Mungu wetu; (Hiyo ni kweli.)

Kizazi hiki kinaukataa ufunuo wa Mungu,

Lakini tunatembea mahali ambapo mitume
wamekanyaga.

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zikiwa
zimesafishwa na kuwa safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

³⁶⁶ Pata ufunuo, ndugu. Kizazi hiki, kinaukataa ufunuo wa Mungu! Mnaona? Manabii wa uwongo wanafanya hivyo. “Kwa matunda yao mtawatambua.” Wao ni—wao ni chotara. Wamezaliwa katika shirika; badala ya Neno la Mungu, ufunuo wa Mungu akijifunua Mwenyewe kupitia kwa Kristo, ambaye ni Neno. Loo, jamani!

³⁶⁷ Tungeweza kuachia hapa, lakini kama...tulichukue tena nitakaporudi, mkitaka. Sasa kuna...Mkitaka kwenda mbele, hiyo ni juu yenu. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Kidogo tu...Nitaharakisha, kwa hivyo, lakini tuchukue muda wa kutosha ili muweze...Mnao muda wa kupumzika, baada ya hili. Vema.

Vile vile, angalieni, hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani!

³⁶⁸ Roho Mtakatifu, peke yake, anakuonyesha Yeye ni Nani; hakuna manabii wala wafalme Wake. Na hapa Mungu anadhihirishwa katika mwili. Huu hapa utimilifu. Yeye amefunuliwa kabisa na kujulikana kwa ulimwengu. Loo, jamani!

³⁶⁹ Angalieni kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, wakati ushuhuda wa Mungu Mwenyewe, “Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye!” Hapo alisimama Musa akiwakilisha torati. Hapo alisimama Eliya akiwawakilisha manabii. Lakini Yeye...Walitoweka, Naye akasema: “Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye!” Kulikuwa na watatu wakiwakilishwa pale; sheria, manabii, na Mu...na Kristo. Naye akasema, “*Huyu* Ndiye.” Mungu, kikamilifu; si aliyedhihirishwa katika manabii, si aliyedhihirishwa na torati; bali aliyedhihirishwa katika Kristo, Ndiye.

³⁷⁰ Kristo ana rehema. Sheria ilikutia gerezeni, bali haikuweza kukutoa. Manabii ni haki ya Mungu, ili kukuhukumu na kukuulia hilo. Hiyo ni kweli. Lakini Yesu alikuwa ni upendo wa Mungu na ufunuo, kufanya ijulikane, kwa Uzao uliochaguliwa tangu zamani, kwamba alikuwa amekuita. “Huyu Ndiye. Msikieni Yeye!”

³⁷¹ Kujua! Utimilifu wa Uungu unajulikana. Siri hii ya fumbo sasa imefichuliwa, ya kwamba Mungu amedhihirishwa. Mungu na mwanadamu wanakuwa Mmoja, Mwanadamu aliyetiwa mafuta, Kristo! *Kristo* linamaanisha nini? “Aliyetiwa mafuta,”

Mpakwa mafuta aliyepakwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Loo, jamani! Watu wanawezaje kulitilia shaka?

³⁷² Ambapo wakati mmoja, kwa sehemu, Musa alikuwa Naye; kwa sehemu, Daudi alikuwa Naye; loo, jamani, lakini huyu hapa amedhihirishwa katika utimilifu, Uungu Wenyewe ukisimama duniani. Mungu, katika utimilifu Wake, kufa kwa ajili ya dhambi ya watu, apate kuleta Kanisani Mwake Maisha yaliyotakaswa; ili awe na utangulizi, katika utimilifu, Kanisani Mwake, kudhihirisha kila ahadi katika siku hizi za mwisho, alizoahidi kwa ajili ya siku za mwisho. Mnaona? Kile kilikuwa . . .

³⁷³ Sikilizeni sasa. Mnasikiliza? Sasa jichune kidogo tu sasa. Angalia.

³⁷⁴ Yesu alidhihirishwa kwa sababu gani? Kumwonyesha Mungu. Alikuwa ni Mungu. Ilibidi awe; hakuna mtu angeweza kufa, hakuna nabii angeweza kufa. Alikuwa Mungu. Alikuwa Mungu wa manabii. Alikuwa manabii. Alikuwa ni wafalme. Alikuwa ndiye historia. Alikuwa Yeye yule atakayekuja. Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, na Yeye atakayekuwako katika siku hii; yeye yule jana, leo, na hata milele. Alidhihirishwa kwa kusudi hilo.

³⁷⁵ Na kupitia kusudi hilo akapata Kanisa, ili Yeye, utimilifu wa Mungu, apate kutimiza kila Neno la Mungu lililoahidiwa katika siku hizi za mwisho; atakapopata utangulizi, utangulizi katika Kanisa, nafasi, mahali Pake Kanisani. Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; hata zaidi ya hizi atazifanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu.” Unaona, hilo lilikuwa ndilo kusudi Lake. Kulikuwa na udhihirisho. Na sasa, siku hizi, Yeye anataka kupata mtu anayeweza kuona sana, hata waweze kuruhusu Neno . . .

³⁷⁶ Unaona, Yesu aliona hivyo, alizaliwa kikamilifu sana kwa ajili ya siku hiyo, mpaka Mungu akadhihirisha kila hatua aliyochukua. Alikuwa ni ufunuo wa Mungu; Mungu, aliyefunuliwa.

³⁷⁷ Sasa Yeye alitakasa, kwa Roho na Damu Yake, Kanisa, apate kufanya kila ahadi katika siku hii ya mwisho ifunuliwe. Sasa, mnaona, Yeye angeweza kurudi na kuokota yale ambayo jamaa hawa wengine wameachilia hapa, katika siku za mwisho, na kwa Roho Wake Mtakatifu afunue siri yote ya ile Mihuri Saba. Mnaona, Yeye anajieleza Mwenyewe. Hilo ndilo kusudi Lake. Ndiyo maana alikufa. Hiyo ni sehemu ya pili ya udhihirisho Wake wenye sehemu tatu. Kwanza, kujidhihirisha Mwenyewe katika Kristo, kisha kujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa Kanisa. Na jambo lile lile, Kristo alikuwa Neno, nalo Kanisa linakuwa Neno linaporuhusu Neno lipite ndani yao.

³⁷⁸ Lakini wanapokubali madhehebu ya chotara, Neno linawezaje kupitia humo? Limeunganishwa na ardhi, basi linasababisha shoti na kulipua fyuzi. Mnaona?

³⁷⁹ Lakini mkondo wa umeme unapoendelea kwa njia huru, Neno la Mungu, linajidhihirisha Lenyewe. “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, pia.” Na katika siku za mwisho itatimia: “Angalieni, nawapelekea Eliya nabii, naye ataigeuza mioyo ya—ya watoto ielekee Imani ya baba zao.”

³⁸⁰ Na mle ndani, kungekuwa na wakati ambao angeweza kujieleza Mwenyewe katika utimilifu wa Uungu Wake, Uungu, kupitia Kanisa Lake, awe na utangulizi katika Kanisa hili. Loo, jamani! Ati nini? Mtu aliyetiwa mafuta; sasa watu waliotiwa mafuta; loo, jamani, kumrudisha Bibi-arusi na Bwana-arusi waliotiwa mafuta. Waliotiwa mafuta na (kwa nini?) kukubali yale ambayo Hawa alikataa, na Adamu; akirudi na upako wa Neno, kwa maana Yeye alisema, “Neno Langu ni Roho.” Mnaona, aliyetiwa mafuta kwa Neno. Kile ambacho Hawa alikataa, Yeye anarudi na tunakubali.

³⁸¹ Mnaona jinsi hiyo hali ya kichotara, tena, yale hasa aliyomfanya Hawa.

³⁸² Alimwambia Hawa, “Usifanye *hivi*, wala usifanye *vile*; na unaweza kufanya *hivi*, na *vile*.”

³⁸³ Ndipo Shetani akasema, “Loo! Wajua. . .” Lakini akageuka na kumsikiliza.

³⁸⁴ Lakini yule Hawa katika siku za mwisho hatafanya jambo hilo, kwa maana alichaguliwa tangu zamani asilifanye. Naam, bwana. Mungu atalifanya. Anajua. Atakuwa nalo. Alisema ninii Lake, doa. . . “Kanisa lingekuwa pale bila ila wala kunyanzi.” Atasimama pale katika fahari Yake, Neno Lake likidhihirishwa.

³⁸⁵ Atakuwa ishara kwa ulimwengu. Atakuwa mf- . . . Atakuwa kitu fulani kwa ulimwengu ambacho ulimwengu unaweza kutazama na kusema, vema, ulimwengu wote useme, “Aha, Yeye ni mtakatifu anayejifingirisha. Yeye ni binamu wa pili. Si wa kundi letu.” Najua. Hilo ni jambo jema, mnaona. Ni—ni mfuasi wa Kundi hili *hapa* juu.

³⁸⁶ Mtu fulani alisema hivi majuzi, akaniambia, huku tukisimama na kuzungumza, akasema, “Vema, wewe ni wa dhehebu gani?”

Nikasema, “Hakuna.”

“Ati nini?”

“Hakuna.” Nikasema, “Mimi ni mwenyeji wa Ufalme.”

“Vema, kwani unajiungaje na huo?”

“Hujiungi nao. Unazaliwa ndani yake.” Uh-huh.

“Ufalme gani huo?”

Nikasema, “Mwili wa siri wa Yesu Kristo.”

³⁸⁷ “Kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili huu,” tukazaliwa kwa Roho Wake, ndipo sisi ni raia wa Ufalme. Nayo maisha yetu si Wamarekani, sisi si Wajerumani, sisi si

kitu; sisi ni Wakristo. Tumetulia, na tunatembea katika Roho, mtumwa wa upendo. Kutoka kwa mambo ya ulimwengu, na haki zetu kwa ulimwengu, tumeuza na kununua Lulu hii ya Thamani Kubwa, na kutembea na kumwacha Roho Mtakatifu ajidhihirishe Mwenyewe. Hivyo ndivyo Kanisa Lake halisi lilivyo. Hivyo ndivyo ulivyo, jinsi nilivyo, ikiwa tutajiachilia kwenda na kumtumikia Mungu, na kwa Neno Lake, wala si kwa yale kanuni fulani ya imani isemayo.

³⁸⁸ Angalia, yule Mtu aliyetiwa mafuta, yule Kristo Mwenyewe hapa, Ee Mungu, anatambulikana. Lakini sasa, tazama, lakini—lakini sasa (Salaala!) Yeye ana utangulizi. Mungu akidhihirishwa kikamilifu, katika Yesu Kristo, siri kuu ya Mungu ya ufunuo Wake.

³⁸⁹ Hii Nuru kuu ya ufunuo daima imepofusha hekima ya ulimwengu huu.

³⁹⁰ Katika siku za Yesu Kristo, alipokuwa hapa duniani, wa—walikuwa wamewapofusha. Walisema, “Mbona, hata unajifanya Mungu! Unajifanya kuwa sawa na Mungu!” Hakuwa tu sawa na Mungu; alikuwa Mungu Mwenyewe. Mnaona, hawalipati. Na jambo lingine, baadhi yenu wanaweza. . .

³⁹¹ Nimewasikia makafiri wakati mmoja wakiniambia kwamba Yesu hakuwahi kusema Yeye ni Mwana wa Mungu. Hakika alisema. Bila shaka alisema. Ni kwamba tu huijui Biblia yako. Alimwambia nini yule mwanamke kisimani? Mnaona? Alimwambia nini?

³⁹² “Najua Masihi yuaja. Naye atakapokuja, atafanya mambo haya.”

Akasema, “Mimi Ndiye, na ninazungumza nawe.”

Na kwa Paulo, pia, na wengine mbalimbali.

Angalieni. Lakini sasa Kanisa lina utangulizi.

³⁹³ Siri kuu ya Mungu sikuzote imepofusha hekima ya ulimwengu. Hawawezi kuipata. Kamwe hawaelewi. Shetani haielewi. Hakuna hata mmoja wa hao wengine anayeielewa, ila wale tu waliochaguliwa tangu zamani kuelewa, jinsi Mungu na Kristo ni Mmoja. Watamfanya kuwa watatu kila wakati. Mnaona? Hakika watafanya hivyo.

³⁹⁴ Angalia, kinachofuata, cha pili, Kristo aliyedhihirishwa ndani yako, tumaini la utukufu. Huyo Mungu mkuu, alidhihirishwa katika Kristo; sasa Kristo anadhihirishwa ndani yako.

Tutaharakisha.

³⁹⁵ Tazama! Kile kilichokuwa ni siri kuu ya Mungu wakati mmoja, siri kuu ya mafumbo akilini Mwake, sasa kimewekwa ndani ya mioyo ya mwaminio, yaani, Mwili wa Kristo. Kile ambacho kilikuwa siri kuu ya Mungu niani Mwake

wakati mmoja, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, sasa kimedhihirishwa. Wazia hilo, rafiki. Loo, loo, mimi. . .

³⁹⁶ Nina hakika hatuninii, hatulipati. Naam, si—siwezi kuliona jinsi ninavyopaswa kuliona, na—na nina uhakika hamlioni. Mnaona?

³⁹⁷ Lakini siri kuu ya Mungu, kile ambacho Mungu wa Milele alikuwa nacho kama siri, sasa kimefunuliwa katika Yesu Kristo, kisha kikawasilishwa moja kwa moja kwa Kanisa Lake. Kile kilichokuwa niani mwa Mungu wakati mmoja sasa kiko katika Mwili wa Kristo. Yesu akifanya mapenzi na Kanisa, Bibi-arusi Wake, akimnong'onezea siri.

³⁹⁸ Unajua jinsi unavyomwambia mke wako mambo, unajua, msichana mdogo utakayemwoa. Unampenda sana, unamwambia tu siri, na kumweka karibu nawe, na kukupenda wewe na kadhalika. Unajua jinsi ilivyo.

³⁹⁹ Hivyo ndivyo Mungu, Kristo, analifanyia Kanisa. Mnaona? Anamjulisha siri, siri tu. Sio hawa wafanya utani; ninamaanisha Mke Wake (Unaona? Vema, sasa angalia.) anajua, kwa kuwajulisha ufunuo wa siri Yake, kwa neema Yake! Jinsi neema ya Mungu! Watu, najua. . . Natumai hamdhanii hili linaonekana la kibinafsi, kwa ku—kundi la watu, ama *hili, lile*; lakini siri ambayo Mungu anashiriki na Kanisa zima, laiti tu wangelipokea. Mnaona? Haimaanishi mimi tu au wewe. Inamaanisha Kanisa, kwamba Yeye—Yeye anajaribu kuingia ndani yake.

⁴⁰⁰ Nanyi mnasema, “Vema, kwa nini hawaipokei?” Hawawezi kuipokea. Alisema, tena, alisema mambo haya. “Nao wangepokea?” Kwa sababu Isaya alisema hawawezi kuiona. Mnaona? Naye daima alisema. . .

⁴⁰¹ Nabii Paulo alisema, “Katika siku za mwisho watu wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizua, na wasiowapenda walio wema; wakaidi, wenye kujivuna, mnaona; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Maana hawa ndio waendao nyumba hadi nyumba, na kuwaongoza wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi,” wamevaa kaptura, na kukata nywele, na kadhalika. “Waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, na kusema, ‘Ni sawa. Loo, wana wazimu huko nje. Usijali. . .’” Mnaona? “Wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa ile Kweli. Nao watu hawa waliipinga Hiyo, kama vile Yambre na Yane walivyompinga Musa,” wanaweza kuanzisha kanisa, na kupata kundi la watu. Naam, bwana.

⁴⁰² “Lakini upumbavu wao utadhihirika,” wakati Yesu atakapomchukua Bibi-arusi Wake na kumweka hapa juu, na kusema, “*Huyu* Ndiye,” na kwenda pamoja Naye. Hiyo ni kweli. Nao upumbavu wao utajulikana.

403 Liangalieni, kuwajulisha siri hii kwa neema Yake! Angalieni! Wakati ufunuo huu mkuu, siri iliyofunuliwa, inapofunuliwa kwako, basi unayakataa mambo yote ya ulimwengu.

404 Sasa nitarudi kwa mara nyingine tena. Afadhali niliseme tu, ninaliekezea kidole, kwa ajili ya kanda, na zile zinazosambazwa kote; kanda hii husambazwa ulimwenguni kote. Mnaona?

405 Ninyi wanawake mnaodai mna ubatizo wa Roho Mtakatifu, wala hamna ujasiri wa kuziacha nywele zenu zikue; wakati Biblia inalishutumu na kusema ninii ya mwanamke... mwanamume ana haki ya kumwacha mke wake kwa talaka kama akinyoa nywele zake. Anaheshimiwa mbele za Mungu, kufanya hivyo. Biblia ilisema, kama akikata nywele zake, anakiaibisha kichwa chake. Na ni kawaida; tu, mnajua, jambo lolote la kawaida ni nini, kwa mwanamke hata kuomba akiwa amekata nywele. Mnaona?

406 Kuvaa kaptura, na suruali hizi, na kadhalika! Biblia ilisema, "Mwanamke yeyote atakayeninii," (loo, unasema. . .) "anayevaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo kwa Mungu," mchafu, kinyaa, kama bafu kuukuu inayonuka mahali fulani. Mnaona? Loo, jamani! Uchafu puani mwa Mungu! Na kisha unajaribu kuomba au kuomba dua katika kitu kama hicho? Mungu anakataa, anayakataa. Hiyo ni kweli.

407 "Vema," unasema, "sasa ngoja kidogo, Ndugu Branham, unazungumza kuhusu Agano la Kale."

408 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ni ufunuo kamili wa Mungu. Mungu akisema lolote, kamwe hawezi kulibadilisha. Yeye hulikuza kila wakati, si kulibadilisha. Torati ilikuzwa, si kubadilishwa. Imekuzwa!

409 "Kila aziniye atakuwa na hatia ya kifo,' lakini yeyote," sasa imekuzwa, "amtazamaye mwanamke kwa kumtamani!" Hakuwahi kubadilisha amri. Aliikuza.

410 "Ikumbuke siku ya sabato; uitakase," siku moja katika juma; sasa ameikuza, "raha" huja kwa kumdumisha Roho wa Mungu. "Amri juu ya amri, na kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo, na hapa kidogo. Shikilia lililo jema. Kwa maana kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hiyo ndiyo raha. Huko ndiko kuburudika kutoka kwenye Uwepo wa Bwana."

411 Na hata hivyo hawakulisikia, na kutikisa vichwa vyao na kuondoka, kwa ajili ya madhehebu yao. Uh-huh. "Hii ndiyo raha," unaona, kuikuza siku ya sabato; kwenu ninyi Wasabato, na kadhalika. Loo, jamani! Yeye habadiliki. Anaikuza. Kuzimu imetandaza milango yake ili kuwapokea.

412 Sasa, mnaweza kuona sasa, Ujumbe wa wakati wa mwisho, kwa nini umekataliwa. Mnaweza? [Kusanyiko linasema,

“Amina.”—Mh.] Sasa, si dhehebu, bali ufunuo wa siri Yake. Mnaona, si dhehebu. Ufunuo! Mungu hajulikani kwa dhehebu. Anajulikana kwa ufunuo.

413 Angalieni! Mungu katika Mwili Wake, Kristo; na Kristo katika Mwili Wake, Bibi-arusi. Loo-loo-loo, jamani! Mungu akidhihirishwa katika Kristo; Kristo akidhihirishwa katika Bibi-arusi! Na kama vile Mungu alivyomtwaa katika mwili wa Adamu, mwanamke, naye akaanguka; basi Mungu ametwaa kutoka katika mwili wa Kristo, mwili Wake, Mwili Wake, ambao ni Neno Lake, na ni kumtoa Bibi-arusi ambaye hataanguka kwa madhehebu au kanuni za imani. La, bwana. Bali anarudi kwa Neno safi, lisiloghoshiwa la Mungu likidhihirishwa.

414 Natumaini kila mwanamume anayeisikia kanda hii, na kila mwanamke, ataelewa jambo hilo. Mnaona?

415 Yeye ni Hawa wa pili, lakini Yeye havunji na—na kuharibu sketi Zake za usafi na utakatifu, kwa Mume Wake. Atadumu na Neno Lake bila kujali mtu yeyote anasema nini. Unaweza kuwa na mienendo yote ya kiekumeni unayotaka, na mashirikiano yote.

416 Nao wataleta mateso, hivi karibuni sana, na kuyafunga makanisa yote. Mnaona hilo. Na makanisa kama hili, ambayo si dhehebu, watayatumia kama ghala, chochote kile. Na kama mtu yeyote akienda na kumwomba mtu mwingine yeyote ambaye si wa hilo shirika la kiuchumi, atapigwa risasi papo hapo. Yote yako tayari. Huyo mhudumu wa Kilutheri, kiongozi wake, alisema hivyo. Na liko papa hapa, unaweza kulisoma papa hapa kwenye gazeti lako. Kweli.

417 Haileti tofauti yoyote yale wanayosema, Kanisa hilo litasimama aminifu katika vita. Tayari lilithibitisha huko nyuma, Nalo litafanya hivyo tena mbele ya kila kitu. Ni Neno la Mungu. Basi acheni mienendo yote ya ekumeni na chochote kile kiondoke. Litakuwa Pale bila ila wala kunyanzi. Hiyo ni kweli. Litasimama hapo.

418 Angalieni, Mungu alijidhihirisha Mwenyewe katika mwili Wake, Kristo. Sasa mnaona kitu hicho kizuri, chenye sehemu tatu?

419 Kristo katika Mwili Wake, Kanisa, akithibitisha Neno Lake lililoahidiwa, kama vile Mungu alivyofanya kupitia Kristo.

420 “Ni nani awezaye kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi? Nisipozitenda kazi za Baba, basi nime—nimeshindwa wapi? Sasa ninyi jamaa mnasema ya kwamba mnafanya hilo, ninyi dhehebu sasa, sasa nionyeshe ni Mimi. Naam. Nionyeshe ni mahali ninaposhindwa kuwa Masihi. Nionyeshe ni mahali niliposhindwa, kwenye ishara moja ambayo Mungu alisema Masihi angefanya, ambayo sijaitimiza,” alisema. Mnaona? Mungu katika mwili Wake.

⁴²¹ Sasa Kristo, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaona, mnaona, Mungu yeye yule. Mnaona? “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba Yangu,” Kanisa litakuwa katika Nuru kwa muda mrefu zaidi, mnaona. Kuthibitisha Neno Lake lililoahidiwa. Kama vile Mungu alivyofanya ahadi Zake katika mwili wa Kristo, vivyo hivyo Kristo anafanya kazi Zake zile zile katika Mwili wa Kristo, Kanisa, mnaona, sasa akifanya siri Yake ijulikane kwa Mti Wake wa Bibi-arusi katika siku ya mwisho, ukizaa matunda yaliyokuwa kwenye ule Mti hapo mwanzo.

⁴²² Angalia, huo mti ukatoa tawi, Mlutheri. Ulifanya nini? Wakati huo mti ulipoanza kukua, hili hapa tunda linakuja pamoja nao. Nini kilitokea? Wakaliundia dhehebu. Kwa hiyo mpogoaji akapitia hapo, Baba, Mkulima, na kuukata huo, akasema, “Umekufa.”

⁴²³ Wakaja Wawesley; ukafanya vizuri wakati ukikua. Ulifanya nini? Lile tunda likarudi moja kwa moja kwenye huo mti tena, kwa hiyo akaukata huo mzabibu, ukafa.

⁴²⁴ Nionyeshe kanisa moja, moja... Nataka kujua. Nina miaka thelathini na mitatu ya historia ya kanisa. Nionyeshe wakati mmoja, mahali pamoja, ambapo kanisa lolote liliwahi kuunda dhehebu ambalo halikufa papo hapo. Nionyeshe mahali pamoja walipowahi kuinuka tena, nje ya idadi tu na kadhalika, sio uamsho. Mnaona? Halipo. La, bwana. Lote limekwisha.

⁴²⁵ Kwa hivyo huyo Mkulima alifanya nini? Alikuwa akaupogoa. Mnaona? Ulizaa tunda la kimadhehebu; limau kwenye mti wa mchungwa, kwa hiyo akaupogoa, mnaona. Akauleta huku, ukaendelea.

⁴²⁶ Lakini moyo wa huo mti uko wapi? Papo hapo katikati. Naye ameyapogoa yote, mpaka juu kabisa...

⁴²⁷ Ana Mbegu hapa chini kwenye mzizi. Kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji, yeye achukuaye sheria za Mungu na upendo moyoni mwake. “Naye atakuwa kama mti,” Zaburi 1, “uliopandwa kando kando ya mito ya maji; majani yake hayatanyauka; kwa majira yake atazaa tunda lake.” Nalo hili hapa papa...

⁴²⁸ Nalo tunda huivia wapi haraka? Huko juu ya mti. Kwa nini? Nuru iko juu yake. Amina! Hiyo ni kweli. Na papo hapo juu ya mti, katika siku hizi za mwisho, Yeye analeta Mti wa Bibi-arusi.

⁴²⁹ Sasa kumbukeni, Yeye ndiye huo Mti wa Uzima, kinyume na “uzao wa nyoka,” mnaona. Yeye ndiye ule Uzao, “Uzao wa mwanamke,” ule Mti wa Uzima katika bustani. “Na kusudi wasije wakanyoosha mikono yao na kuuondoa Mti huu, wangekula Mti huo na kuishi milele.” Naye ndiye Mti pekee unaoweza kutwaliwa, ambao unaweza kuishi milele. Neno Lake ni Uzima. Na hilo liwe Neno basi, Neno la Mungu ambalo Hawa

alilikataa katika bustani ya Edeni; basi huyu hapa Kristo, Neno, lililodhihirishwa.

⁴³⁰ Ndipo alipokuja duniani, Yeye alikuwa ndiye ule Mti wa Uzima. Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nayo Rumi, walifanya nini? Ilibidi apogolewe. Ndipo akawekwa juu ya mti wa aibu, “amelaaniwa aangikwaye juu ya mti,” akawa laana kwa jamii ya wanadamu.

⁴³¹ Na sasa kupitia hilo, Yeye analeta Mti wa Bibi-arusi, ambao utakuwa ni Mti wa Uzima uliorejeshwa Kwake, kama Mume na Mke katika bustani ya Edeni, (loo, utukufu kwa Mungu) kwa Neno lile lile na Mungu yeye yule aliyedhihirishwa katika Mume na Mke, Mti ule ule wa Bibi-arusi ukirudi tena.

⁴³² Angalieni, kulifanya lijulikane! Vile... Jamani, kuna mengi sana hapa, tungeweza tu kuendelea. Angalieni, Mti huu, wa Mwili wa Kristo, bustanini. Akifanya, sasa akiujulisha Mti huu wa Bibi-arusi siri yake.

⁴³³ Angalia, ulikombolewa na Kristo, Adamu wa pili. Mnaamini alikuwa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kurudi Nyumbani, huko Edeni, pamoja na mke Wake aliyeanguka amekombolewa apate kurudi Nyumbani tena. Huyu ni Kristo Kanisani siku hizi, akimrudisha Mke Wake tena. Mnaiona ile siri yenye sehemu tatu sasa? [“Amina.”] Mungu akidhihirishwa katika Kristo; Kristo akidhihirika katika Kanisa; wote pamoja, kuwarudisha Adamu na Hawa wa asili tena, mwanamume na mwanamke, ambao ni mmoja, waliofanywa kwa Damu ile ile na Roho yule yule, na kadhalika.

⁴³⁴ Kanisa ni Damu ya Kristo, kwa Roho, kwa sababu U—Uhai uko katika Damu. Huo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao hutubatiza tukawa Mwili Wake, ambao hutambua tu Mwili Wake, nyama Zake, Neno Lake. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.]

⁴³⁵ Dhehebu halitagusa jambo hilo kamwe. Ni ufunuo. Yeye anajua hilo. Vivyo hivyo Hawa alilijua, lakini alianguka; bali huyu naye anajua, wala hataanguka. Amekusudiwa! Haleluya! Whiu! Amekusudiwa asianguke. Yeye hataanguka. Amechaguliwa tangu zamani kwa ajili yake. “Heri mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia dhambi.” Ninyi wahudumu mnajua ninachozungumzia, wakati kuna dazeni kadhaa ya ninyi mmeketi hapa. Mnaona? “Heri mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia dhambi,” Daudi.

⁴³⁶ Angalia, kukomboa tena, pamoja Naye, kwenda Nyumbani; kurudi kwenye Uzima wa Milele katika mwili wa mwanadamu, akila, akinywa, akiishi milele. Isaya alisema, “Watajenga nyumba na kuishi, watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga na mwingine achukue.” Watoto hawatachukua, lakini watakuwa huko pamoja na watoto wao. Ataijenga na kukaa humo. Amina. “Hajengi, na mwingine akala; anajenga na

kula, mwenyewe.” Amina! Ni kitu gani? Bibi-arusi Wake akirudi pamoja Naye, amekombolewa akawa Adamu na Hawa wa asili tena, kwa maana mauti imeachwa nyuma. Wanatazama nyuma kwenye msalaba na kuona mauti imelipiwa.

⁴³⁷ Na sasa, kwa imani, tumefufuliwa pamoja Naye, tumeketi katika mahali pa Mbinguni sasa hivi, tukiangalia nyuma kwenye kile kilichotukomboza; tukimngojea Mume aje, twende Nyumbani taratibu pamoja Naye.

⁴³⁸ Kusudi la Mungu lenye sehemu tatu, lililodhihirishwa katika Adamu na Hawa, na kila nabii, na kote katika nyakati, na Yeye atakayekuja; Yeye aliyekuwako, Yeye aliyeko, na Yeye—Yeye atakayekuja. Udhahirisho kamili, ufunuo wa Neno la Mungu, Adamu na Hawa wakirudi Nyumbani tena, wamekombolewa, Mungu akijitambulisha Mwenyewe!

⁴³⁹ Hapo ataketi juu ya Kiti cha Enzi cha Daudi (Hiyo ni kweli?) na atamiliki, atatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Kutakuwako na m—mti kila upande, na kila taifa linaloingia, uponyaji huu utakuwa kwa ajili ya...majani haya yatakuwa kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. Wafalme wataleta heshima yao ndani yake. Hakutakuwa na chochote kitakachoweza kutia unajisi, wala chochote kitakachoringia. Nao Mlima Sayuni utakuwa na Nuru juu yake, mchana kutwa na usiku kucha, na waliokombolewa watatembea katika Nuru hiyo. Loo, haleluya!

⁴⁴⁰ Kuwazia, sio hadithi ya kubuni, sio dhana fulani ya kitheolojia. Ni ufunuo wa Yesu Kristo, kwa Neno Lake, ambalo linang’aa zaidi, limekuwa kweli katika nyakati zote. Na ni kweli katika wakati huu. Ni kweli hapa sasa. Ni kweli kwangu mimi, ni kweli kwako wewe, na kila mwanamume na mwanamke aliye na ufunuo huu. Amina.

⁴⁴¹ Na kumwona Mungu Mwenyewe akijitambulisha Mwenyewe, na kudundadunda Mwenyewe kupitia maishani, kwamba wewe ni mfungwa Wake sasa. Wewe ni mfungwa Wake wa upendo. Ulimwengu unaweza kucheka, kuwadhihaki, kusema, “Njoni huku nje.” Ungeweza kwenda, lakini wewe ni mfungwa. Unaona? Wanawake wengine wanaweza kuigiza Hollywood, lakini si wewe. Wewe ni mfungwa. Amina. Unaona, wewe ni mfungwa wa Kristo. Wanaume wengine wanaweza kuvuta sigara na kunywa pombe na kufanya yasiyofaa, wakitaka, na kujiita Wakristo, mashemasi, na hata wahubiri, lakini si wewe. Wewe ni mfungwa, mfungwa wa Neno. Naam, bwana. Naam, bwana.

⁴⁴² Akijulisha siri Yake kwa Mti wa Bibi-arusi; uliokombolewa na Kristo, Adamu wa pili; akirudi Nyumbani, kurejeshwa tena kwenye Edeni ya asili, huru na kifo, magonjwa, huzuni, aibu, akirudi na Uzima wa Milele.

⁴⁴³ Basi, sikilizeni, watu wengi sana wana mawazo mabaya. Ninii—ninii... Kuwaongoa watu kwa Ukristo, na kwa utawala

wake, sio wazo la Mungu hata kidogo. Unasema, “Tunawafanya waongofu kwa Ukristo kwa utawala Wake.” Si hivyo. “Kweli, hawapaswi kunywa pombe. Hawapaswi kusema uwongo.” Je, mnajua Waislamu wanaweza kuwashinda? Mnajua makafiri huko Afrika, hao watu weusi, nao wana sheria miongoni mwa makabila yao ambazo zinashinda chochote mnachoweza kuzalisha katika Ukristo.

⁴⁴⁴ Mbona, nimeenda kwenye kabila hilo la Washangaani huko. Ikiwa msichana mdogo hajaolewa kwenye umri fulani, lazima aondoke—aondoke kwenye hilo kabila, aondoe rangi ya kabila lake. Anaingia mjini; yeye ni kibarua tu. Na kama yeye... Kabla ya kuolewa, anapaswa kupimwa ubikira wake. Akipatikana na hatia ya kufanya uzinzi na mwanamume fulani, yeye... hana budi kusema ni nani, na wote wawili wanauawa, pamoja. Uh-huh. Loo, wanaweza—wanaweza kuwashinda hawa wanaojiita...

⁴⁴⁵ Vipi ikiwa ungefanya hivyo katika wale wanaojiita Wakristo? Asilimia tisini na tisa kati yao wangekufa kabla ya mapambazuko. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, wanaume na wanawake pia. Mnajua hiyo ni kweli.

“Ati nini?” Unasema, “Vema, mimi ni safi!”

⁴⁴⁶ “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Sasa vipi kuhusu hilo? Na wewe je, dada, uliyejianika kwa mwanamume huyo namna hiyo? Una hatia tu kana kwamba ulifanya hivyo. Unaona?

⁴⁴⁷ “Loo, lakini ni sawa.” Mchungaji anaogopa kusema hivyo, kwa sababu gani? Makao makuu ya dhehebu lake yatamfukuza kama akiyakemea hayo. Wao ni machotara. Hawalichukui Neno. Neno lilisema hiyo ni kweli. Yesu alisema ni kweli, na Yeye ndiye Kichwa.

⁴⁴⁸ Sasa angalieni, Mungu akijitambulisha Mwenyewe. La, hatupaswi kuwafanya waongofu kwa Ukristo kwa utawala; bali kwa ufunuo, Kristo ndani yako, kama vile Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo. Kama vile Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo, Kristo ndani yako! Wakati, yale ambayo Mungu alifanya ndani ya Kristo, Kristo anafanya ndani yako! Ishara alizofanya Mungu ndani ya Kristo, Kristo anafanya ndani yako! Loo, hilo si ni zuri sana? Uh! Loo, jamani! Napenda hilo.

⁴⁴⁹ Yesu alisema, “Siku hiyo,” hiyo ni siku hizi. “Siku hiyo,” ufunuo huu utakapofanywa ujulikane, “mtajua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Ufunuo utakapodhihirika, “Siku hiyo mtajua ya kuwa mimi na Baba tu Mmoja; Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu.” Ndipo ufunuo huo utakapokuja, basi ni, “Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Haya basi. Mnaona sehemu mbalimbali, sehemu tatu mbalimba...Za kufanya nini? Kulirudisha. Tunapaswa kuwa...

Kama vile Yesu alivyokuwa Neno la Mungu, Yeye alithibitisha vivyo hivyo.

⁴⁵⁰ Kama Yeye—kama asingekuwa Neno, hangalilidhihirisha Neno, angalikuwa mwanatheolojia mkuu. Huyu angekuwa ndiye masihi halisi ambaye ulimwengu ulikuwa ukimtazamia. Unaona? Naam, bwana, huyo angekuwa ndiye.

⁴⁵¹ Huyu ndiye wanayemtafuta leo hii, m—m—mtu anayeweza kumzidi Billy Graham, au mtu anayeweza kulizima dhehebu lao, aje na kuwaonyesha hao Wabaptisti hawajui wanaposimama. Hakika. Wanamtafuta huyo. Bali Kanisa linatafuta unyenyekevu na ishara za Mungu aliye hai, Kristo.

⁴⁵² Yesu hakuwa mwanatheolojia mashuhuri. Alikuwa Mkulima mdogo wa kawaida, mwana wa seremala, alivyoitwa. Mnaona? Alitembea kote, lakini Mungu... Alisema, “Baadhi yenu mnionyeshe kile ambacho Biblia inasema kwamba nitafanya, ambacho sijakidhihirisha.”

⁴⁵³ Kwa hiyo Kanisa linaweza kufanya jambo lile lile siku hizi. Yale aliyofanya Kristo, ndiyo Kanisa linafanya sasa. “Siku hiyo mtajua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Mnaona? Haya basi, mkitembea kwenda Sayuni, kuelekea (wapi?) Ufalme! “Siku hiyo mtajua kwamba mimi niko ndani yenu.”

⁴⁵⁴ Pia angalieni hapa. Hapa, ni nzuri. Sitaki mkose hili. Sasa kila mtu, na ninyi watu kwenye kanda, huko porini na popote mtakapoisikia, sasa sikilizeni.

⁴⁵⁵ “Na kama vile Baba alivyonituma Mimi, nami nawatuma ninyi,” Yesu alisema. Mnaona? Sasa angalieni. Baba aliyemtuma aliingia ndani Yake, ili kujithibitisha Mwenyewe vyema, kwa maana Yeye alikuwa Neno. Naye Yesu yeye yule anayewatuma, anaenda pamoja nanyi na ndani yenu, kumthibitisha Mungu yeye yule. “Kama vile Baba alivyonituma, nami ninaishi kwa Baba; kwa hiyo nitawatuma, nanyi muishi kwa Mimi.” Yeye ni nini? Yeye ni Neno. Mnaishi kwa Neno. Loo, jinsi ningetaka kuchukua somo juu ya jambo hilo, na kuhubiri sasa kwa yachata saa kadha juu yake, mnaona, juu ya hilo, jinsi alivyokuwa... juu ya hilo. Angalieni, angalieni, “Naye Baba aliyenituma,” aliambatana Naye. Baba anayetuma... Yesu anayetutuma anaenda ndani yetu.

⁴⁵⁶ “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona, kwa maana Mimi,” kiwakilishi nafsi, “Mimi,” ule Utu, Yesu, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa dunia. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Sasa rudi nyuma uone kile Yeye alichofanya, kisha uone kile unachofanya, kisha ujilinganishe.

⁴⁵⁷ “Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu. Na kama vile siku za Lutu,” wakati Billy Graham na Oral Roberts

mamboleo waliposhuka wakaingia Sodoma na kuwahubiria hao Wasodoma, na kuyapofusha macho yao, mnaona, kwa Injili. Malaika mmoja alibaki nyuma, Mjumbe pamoja na Ibrahimu na lile kundi la Wateule, basi alifanya ishara ya aina gani? Mnaona? Naye Ibrahimu alimwitaje? Elohimu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yesu akionyesha ya kwamba Yeye Mwenyewe, Mungu ndani Yake, atadhihirishwa katika Bibi-arusi Wake katika siku za mwisho! Loo, jamani, jamani! Hakuna mwisho wake; ufunuo tu wa Mungu! Ni wa Milele, unaendelea tu mbele zaidi na zaidi na zaidi.

⁴⁵⁸ Angalieni, basi, Mtu kama Adamu na Hawa wa kwanza, kabla dhambi haijawatenganisha katika mauti; sasa Kristo, Adamu wa pili, Uzimani, anamkomboa Bibi-arusi Wake kutoka mautini; na sasa akiwa njiani kurudi kwenye Edeni ya asili, akimrejsha Bibi-arusi Wake katika ushirika, kurudi pamoja na Mungu, kama Mume na Mke, katika bustani ya Edeni, Kristo na Bibi-arusi Wake.

⁴⁵⁹ Naye Mungu, siku hiyo, “Ufalme apewe Baba; apate kuwa yote katika yote.” “Wakati angali ananena, nitasikia.” Daudi, Kristo, Daudi akiketi kwenye Kiti cha Enzi, Mfalme juu ya jamii yote ya wanadamu. “Na wakati wangali wanafikiria, nitajua wanachofikiria. Kabla hawajazungumza, nitawajibu. Mbwa-mwitu na mwana-kondoo watakula pamoja. Simba atakula majani kama maksai, nao watakula pamoja na kulala chini. Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu,” kurudi moja kwa moja katika Edeni tena, upesi iwezekanavyo!

⁴⁶⁰ Hilo hapo kusudi Lake lenye sehemu tatu. Ee Mungu, tujalie kulijua hilo! Tujalie kulijua!

⁴⁶¹ Sikilizeni kwa makini sasa tena tunapoendelea, tukirudi kwenye Edeni ya asili.

⁴⁶² Kisha tunapozaliwa Naye, tunajazwa Naye. Unaona, maisha yako, Uhai Wake uko ndani yako. Basi, matendo yetu yote yanapaswa kumtangaza Yeye.

⁴⁶³ Kama kuchukua—kuondoa uhai kutoka kwa mti mmoja na kuuweka kwenye mti mwingine. Ukichukua uhai kutoka kwa mpea uweke kwenye mtofaa, utazaa mapea. Hauna budi, maana utomvu, uhai ulio ndani yake, chembechembe ni mpea. Sawa.

Basi, matendo yetu yote yanapaswa kumtangaza Yeye.

⁴⁶⁴ Tunalo Jina Lake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tunapaswa kulibeba Jina Lake.

⁴⁶⁵ Na kumbukeni, sisi sasa, kama Bibi-arusi Wake, tumetiwa mimba kwa Roho Wake. Loo, jamani! Kanisa, likizaa watoto, mnaona, lililotiwa mimba na Roho Wake kwa Jina Lake; likibeba Jina Lake, likibeba Uhai Wake; likitoa dalili za Uhai

Wake, likithibitika pamoja na utangulizi, ushahidi wa kufufuka Kwake; akionyesha kwamba hajafa, bali yu hai hata milele. Huu ni Uzima wa Milele, na umethibitishwa, unathibitishia ulimwengu ya kwamba sisi ni hai ndani Yake. Whiu!

⁴⁶⁶ Unajua, kwa sababu wewe ni mfuasi wa kanisa? Kwa sababu, Kristo anaishi kupitia kwako, umetiwa mimba sana na Roho Wake hata wewe—wewe ni mfungwa kwa kitu kingine chochote. Umefungiwa, loo, jamani, kwa Injili, umefungiwa kwenye Neno, na watoto wote unaoweza kuwazaa ni hao, maana wewe ni mfungwa.

⁴⁶⁷ Huwezi kufanya uzinzi; tayari umetiwa mimba. Utukufu! Haiwezi kushikilia. Tumbo la uzima limefungwa kwa kitu kingine chochote. Wewe tayari ni Wake, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Hiyo Mbegu imepata Uhai; hakuna ulimwengu unaoweza kuingia. Loo! Loo, jinsi tungependa kukaa juu ya hili kwa yapata saa moja! Nina hakika mnaelewa. Mnaona? Kristo, na Wake pekee, tayari imekwisha. Ile Mbegu ilikuwepo. Ile Mbegu ilikuwa, tayari. Iliwekwa humo lini? “Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ametuchagua tangu awali kwa Uzima wa Milele.” Na mara tu mtiririko utoao Uzima, hiyo Mbegu ikilala pale...Mbegu zingine ambazo zingeingia tu, hazingeshika, hazingeweza kufanya hivyo, hivyo. Lakini wakati Mbegu hiyo ilipoingia, upesi iliziba tumbo la uzazi; hizo mbegu zingine zote ziliondolewa, mnaona, namna hiyo.

⁴⁶⁸ Nawe unakuwa mfungwa, umezungukwa, katika Kristo. Kristo ndani yako, Uzima Wake ukitoa ushahidi Wake, ishara Zake. Loo, jamani, jamani, jamani! Tazama, akileta ishara Zake za Uzima kama ushahidi wa kufufuka Kwake, kuuthibitishia ulimwengu kwamba Uzima wa Milele, unathibitishia ulimwengu ya kwamba tuko hai ndani Yake. Basi liwazieni, hai pamoja na Mungu, Mkombozi wetu, Ambaye alitumba kwa kusudi lile lile, Kanisa, na Maisha Yake umbaji ndani yetu.

⁴⁶⁹ Yaani, Musa angeweza kusema, kwa Neno la Mungu, “Na waje,” ndipo nzi wakaja. Mungu anayeweza kuumba nzi aweza kuumba kuchakulo. Mnaona?

⁴⁷⁰ Anaweza kufanya lolote atakalo. Anaweza kuumba. Anaweza kufanya lolote. Yeye ni Mungu. Mungu yeye yule, Uhai huo umbaji, mnaona, ulio ndani yako, unaweza...Wewe ni mfungwa; huwezi kulinena mpaka Yeye aseme ulinene. Lakini, ulipolinena, ni Neno la Mungu. Amethibitisha kuwa hivyo. Kitu kingine chochote ni sawa, Naye anajua, hilo linaponenwa, haina budi kuwa hivyo. Unaona?

⁴⁷¹ Musa akachukua fimbo yake, akasema, “Vyura na waje,” kwa sababu Mungu alisema, “Na kuje vyura.” Alilitangaza tu. Hiyo ni kweli. Nao vyura wakawa katika kila kitu, kila mahali palikuwa na vyura. Walitoka wapi? Hakuna ajuaye.

Hawakuwepo awali. Lakini Muumba, Mungu, akifanya kazi kupitia mwanadamu, aliumba vitu, spishi hai.

472 Mungu yule yule aliyemwumba chura wa kwanza anaweza kumwumba chura wa pili. Anaumba vyura wote. Loo, jamani! Mnaona ninalomaanisha? Aliumba kuchakulo wa kwanza, anaumba kuchakulo wa pili, anaumba kuchakulo yeyote; anaweza kuumba kuchakulo mahali ambapo hapana kuchakulo. Anaweza kufanya chochote atakacho! Yeye ni Mungu! Yeye ni Mungu! Uhai Wake! Loo, jamani! Ninapowazia hilo, hunifanya nitetemeke! Uh-huh.

473 Loo, kuishi pamoja Naye, kwenda Nyumbani pamoja Naye, tukaishi Naye! Kwenda Nyumbani pamoja Naye tukaishi Naye milele, tukiwa na Uzima wa Milele!

474 Hii ni siri kuu ya Mungu ya upendo uliodhihirishwa, kwamba Mungu na mwanadamu wamekuwa kitu kimoja. Mnaona? Jambo lote ni Mungu na mwanadamu, mmoja. Mungu na mwanadamu walikuwa mmoja, huko; na Mungu na mwanadamu ni mmoja, hapa. Mnaona? Ni nini? Kujazwa na Roho Wake, Yeye akiwa na utangulizi. Hayo yalikuwa mafanikio ya Mungu, hilo ndilo kusudi la Mungu kufanya hivyo: ili Yeye apate kuwa ndani ya Kristo; na Kristo ndani yetu; na sisi sote pamoja, mmoja. Roho Mtakatifu, jambo lile lile; alilifunua kwa Kristo, analifunua hapa; Nguvu umbaji za kimbinguni. Loo, jamani!

475 Mungu yeye yule ambaye angeweza—ambaye angeweza kusema haya yote kupitia kwa Musa, “Vyura na waje,” yeye Yule aliyeweza kusimama pale, “Maji haya na yageuke kuwa divai.” Mnaona? Amina. Je, hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye ni Mungu yeye yule, Yeye yule.

476 Yeye kamwe habadiliki. Ni Mungu ndani ya mwanadamu. Huo ndio udhihirisho Wake. Hilo ndilo analofunua. Hilo ndilo analojaribu kufanya, na Neno la Mungu Mwenyewe likilifunua. Inaonyesha kwamba mwanadamu hawezi kuumba; Mungu ndiye Muumba. Na si mwanadamu tena; ni Mungu Muumba, ndani ya mwanadamu, ambalo ni Kanisa Lake sasa. Amina!

477 Likienda Nyumbani Mbinguni, likaishi Naye, milele. Mungu anaonyesha upendo wa Milele kwa Kanisa.

478 Sikiliza, sikiliza kwa makini sasa. Nataka usikose kupata hii. Hakuna kanisa lingine, hakuna ishara nyingine, hakuna ushirika mwingine, hakuna utawala mwingine, hakuna ushuhuda mwingine, hakuna kanuni nyingine ya imani, hakuna madhehebu, yanayokubalika nje ya Hili. Mungu hakubali chochote isipokuwa hicho, “Kristo ndani yako, tumaini la Utukufu,” kitu pekee ambacho Mungu anatambua. Hakuna ushirika, hakuna kanisa, hakuna kanuni za imani, hakuna dhehebu, hakuna chochote; kila kitu kimekufa. Ni vipande

vinavyopaswa kukatwa, vipogolewe vitoke kwenye kitu hicho, ili Kristo apate kuishi akiwa na utangulizi ndani yako.

479 Si kurejelea nyuma! Nina tawi moja hapa, linalosema, “Ni dhehebu langu.” Hilo halina budi kukatwa, pia. “Nina *ninii* yangu hapa. *Hii* inasema hivi. Mama yangu ataniambia mimi ni mtakatifu anayejifingirisha.” Hilo halina budi kukatwa, pia. Unaona? “Naam, najua mume wangu anataka nivae kaptura hizi.” Hilo halina budi kukatwa, pia. Unaona? Halina budi kukatwa na kupogolewa mpaka liwe ni wewe tu na Kristo, pekee. Unaona? Uh!

480 Wazieni! Kwa Uwepo ulio hai wa Kristo aliye hai kwa Neno lililo hai; loo, Kristo aliye hai, Uwepo ulio hai, Neno lililo hai! Angalieni! Kwa uthibitisho Wake Mwenyewe binafsi, huthibitisha Kanisa Lake.

481 Si wanachama! Kamwe hakufanya jambo hilo, siku za Musa. Hakufanya hivyo katika siku za mtu mwingine yeyote; mwishoni nwa ulimwengu, inapofika mahali ambapo ilikuwa ni maangamizi. Siku za Lutu, haikuwa uanachama. Ilikuwa ni uthibitisho wa kibinafsi, Mungu katika mwili, mnaona, thibitisho la kibinafsi.

482 Kumbukeni! Wazieni hilo, kwamba, watu waliozaliwa kwa Roho Wake, katika siku kama hii, katika wakati huu mkuu wa kimadhehebu tunaoishi, naye Mungu aliye hai huchukua Neno Lake lililo hai na—na kulithibitisha, kibinafsi, Uhai huu ulio katika Neno, chembechembe iliyo ndani ya Mbegu! Na Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alitoka kwenda kupanda. Na Uzima ni Kristo, katika Neno, kibinafsi ndani yako; kuthibitisha jambo ambalo huwezi kufanya, akithibitisha Mwenyewe ya kwamba si wewe, bali ni Yeye. Na umekuwa mmoja, m—m—mtumwa wa upendo Kwake, kuwa Bibi-arusi.

483 Ashukuriwe Mungu aliye hai aliyeziumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo! Si ajabu, “Yeye ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Shina, na Mzao wa Daudi; ile Nyota angavu na ya Asubuhi.” Yeye ni yote katika yote.

484 Uwepo Wake, ndani ya mtu binafsi, pamoja na thibitisho lake Mwenyewe kibinafsi akijieleza Mwenyewe, Neno lililo hai ambalo limeahidiwa kwa ajili ya siku hii, likijidhihirisha Lenyewe kupitia kwako, thibitisho la ufunuo mkuu wa Mungu. Angalia, katika mtu binafsi pekee, kamwe si katika kikundi! Mtu binafsi; sio kwenye kundi! Utambulisho Wake ni kwa mtu binafsi. Mnaelewa hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Si pamoja na Methodist, si na Baptisti, si Presbiteri, si Mlutheri, si Wapentekoste, bali kama mtu binafsi!

485 “Nitachukua mmoja, na kumwacha mmoja; nitawatenganisha.” Hiyo ni kweli. “Wawili watakuwa kondeni;

nitachukua mmoja na kumwacha mmoja. Wawili watakuwa kitandani, nami nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja.”

⁴⁸⁶ Sio kundi. Ni thibitisho la kibinafsi la mtoto wa Mungu aliyetiwa mimba, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, amejisalimisha sana kwa Mungu hata hajali kitu kingine chochote. Naye Roho Mtakatifu akiishi Maisha Yake, akidundadunda ndani yake, ikionyesha thibitisho la—la kibinafsi la Neno, Lenyewe, likijidhihirisha Lenyewe kwa watu na kwa ulimwengu.

⁴⁸⁷ Ulimwengu unawezaje kutembea kwa upofu karibu na kitu kama hicho? Kama vile tu Wakatoliki walivyopita karibu na Mtakatifu Patrick na hawakumtambua mpaka baada ya yeye kufa. Jambo lile lile walilofanya kwa Mtakatifu Martin, hawakulitambua. Jambo lile lile wamefanya katika nyakati zote.

⁴⁸⁸ Jambo lile lile walilomfanyia Joan wa Arc. Kanisa Katoliki lilimchoma moto, ati ni mchawi, kwa sababu alikuwa wa kiroho. Yapata miaka mia moja na hamsini baadaye, waliichimbua miili ya hao makasisi na kuwatupa ndani, kufanya toba.

⁴⁸⁹ Linapita moja kwa moja karibu nao, wala hawalitambui mpaka limekwisha. Inachukua tu Uzao uliochaguliwa tangu zamani ambao Mungu aliuchagua tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Jambo lile lile lilikuja kwenye siku za Nuhu, jambo lile lile likaja katika siku za Musa, siku za Eliya, siku za manabii, siku za Yesu, kuendelea hadi saa ii hii. Mtu aliyetiwa mimba na Uzao wa Mungu, Neno mle ndani likijidhihirisha Lenyewe, wamejitolea kabisa kwa mapenzi ya Mungu hata Neno, na Neno pekee, hujidhihirisha Lenyewe ndani ya mtu huyu, mfungwa, kwa mtu binafsi.

⁴⁹⁰ Sio kusema, “Kanisa langu . . .” Sasa, “kanisa langu” haina uhusiano wowote nayo.

⁴⁹¹ Ni mtu binafsi, mtu mmoja! Kuzimu yote iko kinyume na Mafundisho haya. Kuzimu yote iko kinyume na Ukweli huu, lakini ni Kweli.

⁴⁹² Yesu kamwe hakusema, “Sasa, Petro, wewe na Yohana, na watu wengine wote, mnao ufunuo, sasa kanisa lote limeokoka.” La.

⁴⁹³ Ilikuwa kwake, binafsi. “Nakwambia, wewe,” sio kwao, “kwako, wewe ndiwe Petro; juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Nalo neno *Petro*, maana yake “jiwe.” *Jiwe* linamaanisha “aliyekiri,” au, “aliyejitenga.”

⁴⁹⁴ Juu ya jiwe fulani, juu ya kitu fulani; unaona, walioitwa watoke, Kanisa lililoitwa litoke; juu ya *jiwe* hili, juu ya “ufunuo” huu. “Mwili na damu havikukufunulia jambo hilo. Lakini juu ya ufunuo huu, kundi lililoitwa, nitalijenga Kanisa Langu ndani yao. Na milango yote ya kuzimu haitaweza kulistahimili.”

⁴⁹⁵ “Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaopotea. Wewe ni Wangu! Nitakufua katika siku ya

mwisho, nitampa Uzima wa Milele, na nitamfufua katika siku za mwisho.” Huo hapo, ufunuo. Sio wao; lakini “yeye,” mtu binafsi! Sio kundi; mtu binafsi! Kuzimu yote inaupinga.

⁴⁹⁶ Lakini siri Yake imefunuliwa tu kwa Bibi-arusi Wake mpendwa. Huyu ndiye pekee angeweza kuiona.

⁴⁹⁷ Alisema, “Isaya alisema vyema juu yenu, enyi wanafiki, enyi nyoka nyasini. Mnatoka hapa nje na kusema, ‘Loo, manabii wakuu watakatifu! Tunaweka alama makaburi yao. Tunayang’arisha.’” Akasema, “Ninyi ndinyi mliowaweka humo.” Je, alisema hivyo?

⁴⁹⁸ Jambo lile lile angeyaambia makanisa ya Katoliki katika siku zao, walipotumiwa manabii wa nini la Kale—Agano la Kale kabla hawajawa na Nikea, Rumi kule juu, na wateule. Hao manabii wa kale walitoka kule, wakila funza na kadhalika kutoka ardhini, wakiwa hata hawana nguo, huku wamejizungushia ngozi ya kondoo, na kujaribu kuitetea Kweli hiyo ya Biblia. Lakini kanisa Katoliki lilitaka wazo lao la kiakili. Kisha wakatoa... Wakaja Mtakatifu Ireneo, Polycarp, Martin, wengine wote. Nao walifanya nini? Wakawaweka kaburini, Joan wa Arc, Mtakatifu Patrick, na wengineo. Wakawaweka mle ndani, sasa wanarudi na kupaka kuta chokaa kama walivyomfanyia Joan wa Arc. Walifanya nini? Wakawaweka humo ndani!

⁴⁹⁹ Basi nasema, kama vile Roho Wake anavyowaita, “Kuta zilizopakwa chokaa! Enyi wanafiki, mkijiita kitu fulani, mnapochukua dhana ya kiakili ya mwanadamu, na kuliacha Neno. Badala ya kuja mmetiwa mimba kwa Mbegu ya Mungu, Neno ndani yenu, mmechukua kila chotara.” Si ajabu aliketi kama “kahaba,” kwa sababu yeye “anafanya uasherati wa kiroho,” kuwafundisha watu mambo ya mwanadamu wala si mambo ya Mungu.

⁵⁰⁰ Lakini Yeye alisema, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi Ufalme.” Hiyo ni kweli. Hakika. Hapo tunayo.

⁵⁰¹ Biblia, katika Ufunuo, ilisema, “Mji huu mkubwa ulitawala juu ya wafalme wote wa dunia.” Alisema alikuwa “kahaba.” Hiyo ni nini? Mwanamke anayedai kuwa ni mama wa heshima huku anafanya uasherati. “Alikuwa na kikombe mkononi mwake,” cha kuwatakia heri, walimwengu, “cha... kilichojaa uchafu wa machukizo ya uasherati wake.” Naye alikuwa na binti, makanisa ya Kiprotestanti, kwamba kila moja lilitoka kwake na mafundisho yale yale yake ya uongo, ubatizo ule ule, na kwa kupeana mikono, badala ya ubatizo wa Roho Mtakatifu; na mafundisho yao ya uwongo ya “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” na hayo yote, badala ya kuchukua Jina la Bibi-arusi... Bwana arusi, na kadhalika.

Unasema, “Haileti tofauti yoyote.” Inaleta.

⁵⁰² Nikiandika jina langu kwenye hundi, na kusema, “kasisi,” kwa “mhudumu,” ama kadhalika, hiyo haitatoa pesa zozote. Hiyo ni kweli. Inakataliwa kwenye benki. Uh-huh. Angalieni. Vema.

⁵⁰³ Lakini siri hii yote imefunuliwa tu, kama alivyoahidi, kwa Bibi-arusi Wake. Kuzimu iko kinyume na Ukweli huu, wa ufunuo wa siri hii. Lakini Bibi-arusi amesimama juu yake. Huo ndio msimamo Wake.

⁵⁰⁴ Kwa nini mnaona njaa, Kanisa, kwa nini mnaona kiu? Ni Baba akijaribu kuwafunulia siri hii iliyofichwa. Lakini mnaruhusu mambo mengi yaiondoe ndani yenu. Unaruhusu kazi yako, unamruhusu mke wako, unamruhusu mume wako, unawaruhusu watoto wako, unaruhusu mahangaiko ya ulimwengu, unamruhusu mchungaji fulani, unamruhusu mtu mwingine atoe hiyo kutoka kwako, huku unajua kwamba ndani kabisa moyoni mwako una kiu, una njaa. Ni Mungu akijaribu kukufunulia hilo, unaona, ufunuo. Siku ya mwisho imefika. Angalieni sasa.

⁵⁰⁵ Hebu tuangalie nyuma tena. Siwezi kuyakwepa haya yote. Mnaona? Ninawatakeni tu mtazame hapa kwa dakika moja tu sasa, nasi tutafunga katika dakika chache. Utakuwa... Nipeni tu usikivu wenu mkamilifu kwa dakika moja.

⁵⁰⁶ Angalieni, Wakolosai, kifungu cha 18 hapa. Katika Kitabu cha Wakolosai, kifungu cha 18.

Sasa yeye ndiye kichwa cha kanisa, mwili: naye ni mwanzo, mzaliwa wa kwanza katika wafu; ili katika—ili kwamba awe mtangulizi wa mambo yote.

⁵⁰⁷ “Yeye ndiye Kichwa cha Kanisa, ambalo ni Mwili Wake, Naye anataka utangulizi.” Sikilizeni sasa, sikilizeni kwa makini tunapoenda. Ati nini? Yeye anapaswa kuwa Kichwa cha Mwili, Mwili wa Bibi-arusi Wake, ambaye ametwaliwa kutoka Kwake; mwili na mfupa, kama vile katika Adamu, mnaona, Bibi-arusi.

⁵⁰⁸ “Aliyezaliwa kutoka kwa wafu,” mnaona, hiyo ni, aliyezaliwa kutoka kwa wafu, dhambi ya kutokuamini.

⁵⁰⁹ Hawa aliuawa na nini? Kutokuamini. Hiyo ni kweli? Kutokuamini kwao katika nini? Kwa, kwa wasio... kutokumwamini Mungu? La. Alimwamini Mungu. Hakika. Je, alisema, “Hakuna Mungu”? La, bwana. Hakuwa kafiri. “Vema,” alisema, “unajua, siamini Neno Lake hata kidogo”? La, hapana. Aliamini yote isipokuwa jambo moja dogo. Mnaona?

⁵¹⁰ Sasa je, Biblia haikusema, katika Kitabu cha Ufunuo, Yesu alisema Mwenyewe, “Mimi—Mimi Yesu nime mtuma malaika Wangu kuwashuhudia ninyi mambo haya”? “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake.” Na kama huzuni hizi zote na masikitiko ilibidi zije kwa sababu mwanamke mmoja alitilia shaka Neno

moja la Mungu, je, Yeye atakurudisha ukutilia shaka Neno moja? Angekuwa asiye haki. Uh-huh. Mnaona? Mnaona, hiyo haingekuwa haki. Imehukumiwa . . .

⁵¹¹ Huyu hapa mtu mmoja amesimama, naye alisababisha huzuni hizi zote kwa sababu ya neno moja lililotiliwa shaka; kisha anasonga mbele na kuchukua ujuzi wa miaka na kila kitu, na Biblia na kadhalika, na wengine ambao wametoa uhai wao kwa ajili yake; kisha kusema, “Loo, unaweza kwenda mbele na kula. Hiyo ni sawa, nitakuruhusu urudi, kwa vyovyote vile”? Loo! Mungu hana upendeleo, lakini . . . ? . . . Mnaona? Mnaona? Mungu hana upendeleo. Sasa angalieni.

⁵¹² Angalieni sasa. “Yeye ndiye Kichwa cha Mwili” aliyezaliwa kutoka katika dhambi, ya kutokuliamini Neno la Mungu. Hiyo ina . . . hiyo inaliachilia kila dhehebu, kila kanuni ya imani, mnaona. Kutokuamini Neno; ambalo ni Yeye mwenyewe, Neno la Uzima. Mnaona? Neno, pekee, lina Uzima. Neno lingine lolote ni chotara. Haidhuru linafanana Nalo kiasi gani, si Neno.

⁵¹³ Neno hutoa Uhai Wake Lenyewe, ambao Hawa aliubadilisha kwa maarifa ya kibinafsi. Mnaona jinsi kanisa limefanya, siku hizi? Kupitia ufahamu wa mtu fulani. Musa alikuwa na ufahamu mkubwa wa Mungu mpaka alipokutana na kichaka kilichowaka moto, ndipo akaona kupungukiwa kwake. Kile kichaka kilichowaka moto kilikuwa na yale Musa alipungukiwa. Neno lina yale ambayo madhehebu yamepungukiwa.

“Yeye, Kichwa, ndiye malimbuko ya ufufuo.”

⁵¹⁴ Tutauacha huu, “ufunuo”; kitambo kidogo tu zaidi, mkisema hivyo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Vema, sawa, kidogo tu sasa.

⁵¹⁵ “Yeye ndiye malimbuko ya ufufuo.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tazama. Basi, Yeye ni nani? “Yeye ndiye Kichwa cha Mwili, ambao ni Kanisa Lake, Bibi-arusi.” Uh-huh.

⁵¹⁶ Basi, Mwili wa Bibi-arusi lazima ukifuate Kichwa, kwa maana ni sehemu ya kufufuka Kwake na ni sehemu ya ile siri. Haiwezekani kwake kutoenda. Loo, jamani! Ni sehemu ya siri ya Mungu, jinsi Mungu alivyojifunua Mwenyewe hapa na kuuinua kwa Neno, kwa hiyo Yeye hulifunua Kanisa Lake na kuliinua kwa Neno lile lile. Ni sehemu ya siri Yake yenye sehemu tatu.

⁵¹⁷ Kama vile Kichwa kilivyochukuliwa kutoka kaburini, vivyo hivyo na Mwili hauna budi kumfuata kurudi Edeni. Ambapo, Kichwa cha familia, Mwanamume, Bwana Arusi; Bibi-arusi akiwa ni Mwili wa Bwana-arusi, hana budi kumfuata, Bibi-arusi, kwa maana huyo ndiye Kichwa. Nacho Kichwa kinafunuliwa, na kurudi na Uzima wa Milele; nao Mwili lazima ukifuate, kwa sababu ni Mume na Mke tena. Amina! Na maadamu umetiwa mimba ya Neno lile lile, ambalo ni

Mwili Wake; umeuchukua Mwili Wake, ukawa ndani Yake, ulipolichukua Neno. Si kanuni ya imani; Neno! Loo, jamani!

⁵¹⁸ Je, hilo si lingefanya somo kwa ajili ya alasiri hii, kuendelea nalo? Huh? Jamani, hilo si lingekuwa ni ajabu? Unaona? Hebu wazia jambo hilo sasa, kile lilicho.

⁵¹⁹ Kwa hiyo, Mwili hauwezi kutambua . . . Msilikose hili. Mwili, basi, hauwezi kutambua uongozi mwingine wowote ila Neno. Maana, Ki—Kichwa kimeunganishwa na Mwili, nacho Kichwa ni Neno, na ni Neno lile lile, Uongozi mmoja! Kwa hiyo, madhehebu, na baba watakatifu, na kila kitu kingine, ni samadi iliyokufa. Kuna Uongozi mmoja, huo ni Kristo. Mwili hutambua kitu kimoja tu, Neno!

⁵²⁰ Sasa nionyeshe ambapo mtu fulani alibatizwa, katika Mwili, katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”? Nawe unatambua nini? Unaona, ninatambua ninazungumza na maelfu, kwenye kanda, mwajua, nasi tuna huduma ya kanda kote ulimwenguni. Umebatizwa kwa jina gani? “Kwa maana hapana jina jingine walilopewa chini ya Mbingu,” lilisema Neno, “ambapo mwanadamu anaweza kuokolewa.” Kama umebatizwa, kuonyesha imani yako katika Kristo, na kisha uchukue jina la kanuni ya imani, basi wewe ni chotara. Ikiwa wewe si kama kanisa hilo hasa na unayapenda mafundisho yao hasa . . .

⁵²¹ Halafu, ninyi Wakatoliki, mnaona, mnawezaje kuwa chini ya mamlaka ya papa sasa, mkisema kwamba yeye ndiye mrithi kwa urithi wa kimitume, kutoka kwa Kris- . . . kutoka kwa Petro, na papa huyu na kanisa hili hufundisha kinyume sana na Neno hili la kwanza ambalo Mungu alilitambua, kwa ishara na maajabu, kuwa ndilo Kanisa Lake? Na kuona Neno lile lile likiletwa siku hizi katika usafi Wake, likionyesha ufufuo ule ule aliokuwa nao kule, Mungu akiishi miongoni mwa watu Wake, akifanya mambo yale yale, halafu ati unaweza kutambua uongozi katika Rumi?

⁵²² Uongozi wetu uko Mbinguni. Mimi siendi Rumi; ninaenda Mbinguni nitakapokufa. Mnaona? Mnaona? Uongozi uko Mbinguni.

⁵²³ Nao Mwili hauna budi kukifuata Kichwa, kama vile mke anavyomfuata mume. Kwa kuwa Adamu hakudanganywa, alitoka pamoja na Hawa. Hawa alidanganywa, alikuwa makosani, la sivyo ufufuo mzima wa Mwili wote ungetokea katika ile siku ya Bwana Yesu alipotoka kaburini. Lakini ilimbidi kumkomboa, ambaye ni Mwili Wake. Yeye hana budi kukombolewa apate kuja Kwake. Mnaliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo jamani! Mnaona, haungetukia wakati huo. Ukombozi unaendelea.

⁵²⁴ Sasa mnaiona ile Mihuri? Anapokuwa katika kazi Yake ya upatanisho kule nyuma, akikomboa, lakini siku moja atakuja na kukichukua Kitabu hiki alichokikomboa. Na wote walio katika

Kitabu hiki watakuwa ni Yeye, kwa kuwa huyo ni mwaminio, hayo maneno katika hicho Kitabu, nalo Neno ni Yeye. Na wote walio ndani ya hicho, Yeye alikuja kwa ajili ya Kitabu hiki cha Ukombozi, ambao majina yao yameandikwa katika hicho Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alipochinjwa kama Mwana-Kondoo.

525 Naye huyu hapa leo, katika Neno Lake, akidhihirisha jambo lile lile alilofanya kule. Hawezi kutambua uongozi mwingine. La, bwana. Hakuna askofu, hakuna chochote. Anatambua Uongozi mmoja, huo ni Kristo, naye Kristo ni Neno. Loo, jamani! Whiu! Napenda hilo. Uh! Naam, bwana.

526 Kama vile Kichwa kilivyotolewa kaburini, vivyo hivyo na Mwili Wake hauna budi kumfuata mpaka Edeni. Kwa hiyo, Mwili hauwezi kutambua uongozi mwingine wowote, ila Uongozi wa Neno.

527 Hakuna dhehebu linaloweza kuweka chochote Kwake. “Kwa maana mtu yeyote atakayeondoa Neno moja Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake, liliondoa Kwake.” Umekufa, chotara, papo hapo. Amerudi hapa, ushuhuda huu mikononi mwake, “uchafu wa uasherati wake, akifanya uzinzi wa kiroho,” dhidi ya Neno lile lile analodai kuamini. Mnaona?

528 Kwa hiyo, ni Neno, ama si chochote. Hiyo ni kweli. Yeye, Neno! Unajuaje kuwa ni sawa? Yeye, Neno, amethibitishwa. Unaona? Yeye, Neno, linapothibitishwa ipasavyo, ndiye Uongozi, Kichwa cha Kanisa. Yeye ni Neno, Uongozi. Yeye anatambulishwa ipasavyo, ametambulishwa, amethibitishwa, na Roho Wake Mwenyewe akiwa ndani ya Kanisa Lenyewe, huyo mtu. Akijidhihirisha Mwenyewe, katika uthibitisho, ndio uthibitisho wa moja kwa moja kwa huo Mwili mzima. Huhitaji kanuni za imani, basi. Madhehebu yameangamia. Lakini Uongozi Wenyewe, unatambulika katika Mwili kwa vitambulisho vya kibinafsi, unaona, akijitambulisha Mwenyewe, unathibitisha Uongozi kwa Mwili. Basi, tumeunganishwa chini ya Uongozi Mmoja uliothibitishwa, yaani, Kristo, Neno la Mungu [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] si chini ya kanisa lolote.

529 Basi, Uongozi wetu ni Ufalme. “Ufalme wa Mungu uko ndani yenu,” ilisema Biblia, Yesu. Ufalme! Sisi si dhehebu. Sisi ni raia wa Ufalme, nao huo Ufalme ni Neno la Mungu lililofanyika Roho na Uzima katika maisha yetu wenyewe, likitimiza kila ahadi katika siku hii, kama ilivyokuwa katika siku ile wakati Neno na Mungu walikuwa Mmoja. Nalo Neno na Mungu ni kitu kimoja katika Kanisa Lake siku hizi, likiufanya Ukuu wa Mwili uliokombolewa, kuleta Ujumbe katika siku ya mwisho; na kufufuka katika wafu, katika ufufuo, kurudi na kurejesha tena, kama vile Adamu na Hawa, hapo mwanzo katika bustani

ya Edeni. Siri ya Mungu yenye sehemu tatu, Mwili Wake! Loo, jamani!

Angalieni kwa makini sasa, kama katika mifano, Israeli wa kale. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁵³⁰ Je, ninachukua muda mwingi juu yake? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Msiniache, msiniache niingie sana kwenye. . . Sasa sikilizeni. Sasa hatuna ila kurasa kama ishirini zaidi. Mnaona? Mnaona? Lakini sasa mimi. . . Kidogo tu sasa, na kisha—kisha nitawaacha nyote mwende mpaka kiangazi kijacho, ama wakati fulani, Bwana akipenda. Mnaona?

⁵³¹ Sasa angalieni. Angalieni sasa, wameunganishwa pamoja chini ya Uongozi mmoja, kwa namna ile ile, mfano wa Israeli wa kale. Sasa mnalipata? Kama Israeli wa kale; Mungu mmoja, aliyethibitishwa kwa Nguzo ya Moto, na kujifunua Mwenyewe kupitia nabii, kuwa Neno. Mungu yeye yule, Nguzo ile ile ya Moto, kwa njia ile ile; hawezi kubadili njia Yake. Hilo ni. . . Kamili tu kama iwezavyo kuwa. Sivyo? Mnaona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁵³² Mungu mmoja! Israeli walikuwa na Miungu wangapi? [Kusanyiko linasema, “Mmoja.”—Mh.] Bibi-arusi ana wangapi? [“Mmoja.”] Je, kutakuwa na wangapi? [“Mmoja.”] Hakika. Hakika.

⁵³³ Mnaona, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa ni Nguzo ya Moto katika siku za Musa, yule nabii mkuu. Aliongozwa na Nguzo ya Moto. Je, hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Wakienda kwenye nchi ya ahadi.

⁵³⁴ Na katika wakati wa Kikristo, kulikuwa na Mungu mmoja ambaye alionekana katika umbo la Nguzo ya Moto, kwa nabii aitwaye Paulo, aliyetumwa kwa Mataifa, kuwatoa watu kwa ajili ya Jina Lake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁵³⁵ Na katika siku za mwisho, ameshuka kwa namna iyo hiyo, akijithibitisha Mwenyewe, mnaona, katika ishara ile ile, ajabu ile ile, Nguzo ile ile ya Moto, Injili ile ile, Neno lile lile, dhihirisho lile lile.

⁵³⁶ Mwili Wake utafanya kazi alizoahidi, kama katika Marko 16, na kadhalika. Mwili Wake haukuzuiliwa kaburini, bali ulitambulishwa pamoja Naye katika ufufuo. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, Mwili wa watoto Wake waaminio hautazuiliwa kaburini atakapokuja, bali utatambulishwa pamoja Naye, kwa sababu alikufa kwa kusudi la kumfufua Bibi-arusi Wake, ule Mwili. Unatambulika, kwa sababu ni Mwili Wake, kwa sababu ni Neno. Umetolewa kabisa kutoka kwa mambo ya madhehebu, kwenda Kwake, Naye ni Neno. Mnaona? Na unatambulishwa pamoja Naye kwa sababu sasa tuna limbuko la ufufuo wetu, kwa kujua ya

kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, tumekuwa wafungwa Wake. Naye Mungu, akituthibitishia kwa Ukuu Wake binafsi ya kwamba Yeye ni yeye yule jana na hata milele, kwa kufanya mambo yale yale kupitia Kanisa aliyofanya wakati huo, “Yeye ndani yangu, nami ndani Yake, ndani yenu,” mnajua, kadhalika. Hiyo ni kweli.

⁵³⁷ Mwili Wake haukuzuiliwa kaburini. Ukitambuliwa pamoja Naye katika ufufuo, sawa sawa na alivyo sasa, sikilizeni, ambayo ina maana hii: Neno Lake, ambalo ni Yeye, limeanza kufufuka. Neno, ambalo huko chini katika wakati wa Luther, Wesley, mnaona, limeanza kuinuka kwa nguvu Zake; hapo likianza kusogea, kisha likasogea zaidi, sasa limefikia kwenye utambulisho. Mnaona? Tazama. Sasa, kuhusu Uhai ndani ya Mwili, ni thibitisho la kukaribia kwa Unyakuo. Mtakapoona Uongozi na Mwili vikifanyika Mmoja, na utimilifu wa kipimo cha udhihirisho Wake, inaonyesha kwamba Mwili uko karibu kupokelewa Uongozini.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka.

⁵³⁸ Mnaona ninachomaanisha? Ameanza kutoa Uhai kwa Mwili Wake, (kwa nini?) Ule ambao ameukombo. Kazi ya upatanishi imefanywa, Yeye analeta Uhai Wake kwenye huo Mwili, katika uthibitisho wa Unyakuo. Kumbukeni, sasa, katika siku ya mwisho...

⁵³⁹ Mimi—mimi, kama mtaniruhusu, mtanivumilia tu juu ya hili kidogo, sasa—sasa, itakuwa ni sawa. Sitaki mlikose. Mimi—mimi, na sina budi—sina budi kuchukua kanda hii sasa, kwa kuwa nilianza umbali huu. Tamshi moja kubwa zaidi ninalotaka kutoa, ikinibidi kulisogea kidogo.

⁵⁴⁰ Sasa angalieni. Sikilizeni hili. Sasa ni jambo kubwa. Sasa ndipo tunapotaka kuangalia. Kumbukeni, katika siku za mwisho, zitarudi nyuma kabisa na kuthibitisha siku ya kwanza; mnaona, Adamu na Hawa, mume na mke, hawana dhambi, Uzima; kisha kuanguka. Angalieni, angalieni kwa makini.

Kumnyonganyonga. Uh-huh.

⁵⁴¹ Angalieni. Ni nini kilicholisababisha? Lusifa! Lusifa anafanya sasa kama alivyofanya mara ya kwanza.

⁵⁴² Kama vile ufalme wa mataifa ulivyoingizwa, pamoja na mfalme Nebukadreza, ukaithibitisha jamii ya Mataifa kwa nabii ambaye angeweza kufasiri lugha zisizojulikana, maono, ndoto. Na imeshuka kupitia kwa Mataifa, bila chochote, ni Wamedi-Waajemi tu, na chuma na kadhalika, na katika miguu unatoka kwa njia ile ile tena, ufalme wa Mataifa.

⁵⁴³ Mwangalieni Lusifa, katika siku za mwisho, anafanya kama alivyofanya hapo kwanza. Lusifa alifanya nini? Jambo la kwanza ambalo Lusifa alifanya ili kutenganisha ushirika wa Mungu na wanadamu, alitaka kujijengea ufalme wenye umoja, fahari

kubwa na unaoonekana umestaarabika zaidi, ufalme mkuu kuliko Mikaeli, Kristo aliokuwa nao.

544 Mmelipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, sasa kama ukilikosa, inua tu mkono wako, nitalisema tena, unaona. Unaona?

545 Lusifa, hapo mwanzo, kusudi lake moyoni lilikuwa kufikia jambo zuri na kubwa zaidi Mbinguni kuliko Kristo alivyokuwa nalo. Je, hiyo ni kweli? Kwa kilichoonekana chenye ustaarabu zaidi, kizuri zaidi, chenye fahari zaidi kuliko Ufalme wa Kristo. Mnafikiri tutakuwa na magari katika ule Utawala wa Miaka Elf, na ndege? Mnaona? Mnaona anachofanya Lusifa?

546 Sasa, yale madhehebu makubwa ya kielimu ya kifahari yanafanya jambo lile lile, kukusanyika pamoja kufanya jambo lile lile. Mnaona? Wanajikusanya na kujiundia madhehebu, kila mmoja akijaribu kumshinda mwenzake. Na sasa wana fahari nyingi sana, hawajui la kufanya ila kuliunganisha na kanisa Katoliki. Mnaona? Lusifa tena akijenga ufalme mkubwa zaidi, kuwasukuma nje watu wasioamini katika madhehebu; na hata kuchukua majengo ya kanisa lao na kutengeneza maghala, na wachungaji wa hayo hawana haki hata kidogo.

547 Na mtu ambaye ni mtu aliyetumwa na Mungu kamwe hatakaa katika dhehebu baada ya kusikia Hili ama kuliona, ikiwa—ikiwa anayo ya kutosha kwenda na kulitazama. Bila shaka. Mnaona? Sisemi hivyo kwa kukosoa; ninasema hivyo kwa kweli, mnaona, kuona hilo likifunuliwa.

548 Angalieni, katika siku hizi za mwisho, Lusifa anafanya jambo lile lile. Je, mnaweza kuliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ibilisi akifanya jambo lile lile, akijenga kanisa la kichotara, la kichotara kwa wafuasi chotara, chotara kwa maarifa badala ya Neno, na watu wenye akili badala ya watu waliozaliwa mara ya pili, akijenga ufalme wa kielimu ambao utanawiri kushinda kundi dogo la Kristo. Unaona? Ni nini kilichofanya hivyo? Malaika walioanguka.

549 Biblia ilisema ilikuwa ni malaika walioanguka waliomsikiliza Lusifa badala ya Kristo, Yule ambaye hapo awali walikuwa Wake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

550 Sasa sikilizeni kwa makini, “malaika walioanguka.” Malaika wa aina gani? Luther, Wesley, Katoliki, Wapentekoste, ambao hawakulinda enzi yao ya kwanza kama Malaika walivyofanya, nao wakatumbukia katika madhehebu, kama ile ngome kuu ya Lusifa huko Nikea. Nao wamefanya nini? Wameunda shirika kuu la ekumeni la wahudumu, kufanya “sanamu ya mnyama,” kama Biblia ilivyosema. Na kujenga uchumi wa Kikristo ambao utafunga milango ya kanisa hili na mengine kama hili. Mnamwona Lusifa akifanya kazi?

551 Ninajaribu kuwaletea ufunuo wenye sehemu tatu, ama siri ya Mungu.

552 Walifanya nini? Wakajiuza kwa hoja za hekima na elimu, kama Hawa alivyofanya, malaika walioanguka walivyofanya. Wesley alikuwa mtu wa Mungu; lakini ni nini kilichomfuata? Malaika walioanguka waliingia humo. Hao malaika walikuwa nini, kwanza? Viumbe umbaji wa Mungu, lakini waliangushwa na hekima ya Lusifa, waliangushwa na Lusifa—hekima ya Lusifa. Nanyi mnaona wanachokuwa? Malaika walioanguka. Na madhehebu, kutoka kwa watu wa Mungu waliotoka wakaenda kuziimarisha Kweli duniani; kabla hiyo Kweli haijaendelea na kutangazwa na kuingia kwenye ufunuo halisi wa Kristo, malaika walioanguka waliingia na kuiteka na kuiundia madhehebu.

553 Hiyo ndiyo sababu ufunuo wa ile siri ya Mihuri Saba ilibidi ufunuliwe.

554 Sasa mnaona? Yale waliyoacha, kama Luther angaliendelea, ingalikuwa hapa. Kama Wesley angaliendelea, kama Pentekoste ingaliendelea, wangepanya nini?

555 Sasa kuna jambo moja tu linaloweza kutokea. Inabidi kuwe na Ujumbe katika wakati wa mwisho, wakati hakuna kitu kingine kinachoweza kuufuata. Na sasa ulimwengu wa kiekumeni umeanzisha milki ya namna hiyo kwamba hapawezi kuwa na madhehebu wala hakuna kitu kingine kitakachofuata; ama uko ndani yake au huko ndani yake. Tunda liko juu ya mti, na Nuru inamulikia lile tunda lililokusudiwa tangu zamani. Nalo linaiva liwe tunda linalofanana na Kristo, likileta ubivu na utamu ule ule, na Roho yeye yule aliyekuwa naye ndani Yake. Natumai mnalionna! Mnaona?

556 Mimi hu—hujaribu kushindilia mengi sana katika siku moja. Ninawachosha. [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.]

557 Kwa hiyo, angalieni, walijiuzwa kwa hoja, wakajiuza kwa hoja za madhehebu. “Laiti ningalikuwa mfuasi wa *hili*! Me—meya anahudhuria kanisa hili.” Mnaona? “Laiti ningekuwa Mmethodisti, ama Mpresbiteri.” Angalia tu walikokwenda. Sasa, nimeeleza hivi punde, matawi hayo yamepogolewa. Wamekufa. Hawajaunganishwa na Kristo tena; wangukuwa wanaleta Uzima ule ule. Hawajaunganishwa Naye.

558 Lakini wao—wao ni kama tunda aina ya chungwa. Tunda lolote aina ya chungwa litaishi kwenye mchungwa, lakini litazaa tunda lake lenyewe. Ukiweka mbalungi katika—katika mchungwa, utaishi kwa mchungwa, bali utazaa balungi. Ukiweka mlimau mle ndani, ni tunda aina ya chungwa, utazaa maskini limau kali, bali linaishi kwa uhai mwingine. Na hivyo ndivyo madhehebu yanafanya, chini ya jina la kanisa.

559 Bibi-arusi ndiye Mti wa asili, Roho wa asili. Ufunuo unatoka kwa Kristo, si dhehebu. Kristo! Angalieni.

⁵⁶⁰ Je, dhehebu linajaribu kufanya nini? Kujitukuza, kama Lusifa. Wanajiita wenyewe “Kanisa, Bibi-arusi.” Ambapo, ndivyo walivyo katika Ufunuo 17, kama ilivyonenwa, yule bibi-arusi wa uongo. Juu ya kundi dogo la Kristo, Bibi-arusi; Lusifa anafikiri na kujiinua juu ya Neno nyenyekevu la Kweli la Mungu kwa maarifa ya ufunuo, na amejiweka kwa elimu ya seminari na theolojia mpaka wamejiinua. Na kama wewe si wa kundi lao, basi wewe ni mtu asiye na faida.

⁵⁶¹ Kama vile Lusifa alivyofanya hapo mwanzo, akiwaambia watu vile vile hasa Lusifa alivyomwambia Hawa, “Hakika Mungu atatupokea! Tunawalisha maskini.” Hilo ni jema. “Hakika atatupokea. Sisi ni dhehebu kubwa. Sisi ni kanisa la kupendeza. Mbona, tazama majengo yetu makuu! Angalia uanachama wetu mkuu. Tumefika mamilioni. Hakika Mungu hatalikataa kundi hilo.”

⁵⁶² Jambo lile lile alilofanya Kaini, akaleta matunda mazuri kutoka kwenye ardhi aliyolima, akajitahidi, na kufanya kazi, na kuleta matunda, na kukataa damu nyenyekevu ya mwana-kondoo.

⁵⁶³ Mungu na aturehemu, ili wanaume na wanawake wasifikiri ninasema hivi ili kuinua kitu, au ufunuo fulani wa kibinafsi au kitu fulani. Ninawaambia tu Ukweli. Hivi hamwezi kuona wanachofanya? Mnaona? Ninazungumza kwa sauti kubwa na kwa ukali, lakini huna budi kuupigilia msumari mpaka ushike, kama utafanya jambo lolote jema, mnaona, mpaka mtaliona. Mnaona?

⁵⁶⁴ Sasa, akiwaambia watu, “Hakika! Unataka kuniambia ya kwamba, kanisa letu kuu la Kikatoliki, lililosimama wakati huu wote, Methodisti yetu kuu, na yote? Angalieni mababu zetu!” Mnaona? Lakini walivunja Neno la Bwana. Naye Hawa alikuwa ni wa Mungu, mmoja wa walio Wake, naye...yeye alitokana na Adamu; na kwa sababu alitilia shaka Neno moja la Neno la Mungu, ikawa hivyo.

⁵⁶⁵ Naye huyu hapa Lusifa kazini mwake tena, leo hii. Na, kumbukeni, mpinga-Kristo si ukomunisti. Mpinga-Kristo yuko karibu sana kama kitu halisi, hata, “Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini,” Yesu alisema, Mathayo 24, “Wateule kama yamkini.” Lusifa, tena, Lusifa tena anavunja umoja wa Mungu ndani ya mwanadamu, kwa kuwekea—kuwekea Neno la Mungu mipaka kwa hoja zake. Kile anachofikiri kwamba ni sawa, na kile anachofikiri, yeye huvunja Neno la Mungu.

⁵⁶⁶ Na jambo lilo hilo alilifanya katika siku za Yesu. Naye Yesu akasema, “Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmelitangua Neno la Mungu.”

⁵⁶⁷ Nayo madhehebu, kwa hoja zao za kiakili zilizopangwa, yamelitangua Neno la Mungu kwa watu. Hiyo ni kweli. Hawawezi kabisa kuliona. Kisha wanasema, “Yuko wapi Mungu

wa Biblia?” Yuko papa hapa. Yeye ni Biblia, hivyo ndivyo Yeye alivyo.

⁵⁶⁸ Angalia, sasa, Lusifa anakuja katika ujanja, na kuvunja umoja wa Mungu kwa mwanadamu, kama tu alivyofanya katika Edeni, kwa majaribu makubwa ya ahadi za uwezo wa kibinafsi na kuinuliwa. “Mbona, unaweza kuwa askofu ikiwa tu utakaa nasi. Unaweza kuwa msimamizi wa wilaya. Kwa nini uende kwenye kitu kama Hicho?” Unaona, hao ni Wapentekoste, Wakatoliki, na kadhalika; mnaona, ahadi kuu ya uongo, kwa wanadamu, kupokea nguvu nje ya Neno na ahadi ya Mungu. Unapokea Nguvu wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yako, si wakati unapokuwa askofu, au shemasi, ama chochote alichokuwa. Unaona? Lakini Lusifa yuko kazini mwake tena.

⁵⁶⁹ Je, kanisa hili linaelewa hilo? Inua mkono wako ili nione hilo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, sitakaa nalo tena, basi.

Kujitenga, mbali na Neno la Mungu! Mnaona?

⁵⁷⁰ Alifanya vivyo hivyo huko Nikea, Rumi. Mnajua Konstantino aliwapa nini? Mlipitia Nyakati za Kanisa. Aliwapa... Hawakuwa na kitu, ila Kristo tu. Nao waliketi katika majengo madogo ya kale popote walipoweza, kwenye sakafu ya mwamba mgumu. Mnajua hilo, kama ukichukua *Baraza la Nikea*, na *Baraza Lililotangulia Nikea*, na *Wazee wa Nikea*, na kadhalika, na historia ya kanisa. Hawakuwa na kitu. Lakini walipokuwa na baraza hili na kuingiza baadhi ya upagani wa Kirumi katika Ukristo, na kuwaweka watu watakatifu na maaskofu, na kadhalika, na mapapa, na upuuzi wote wa namna hii, Konstantino aliwapa nini? Ninamwomba mwanatheolojia yeyote aniambie. Aliwapa mali. Aliwapa uhuru na kila walichotaka.

⁵⁷¹ Na wakabadilisha Neno la Mungu kwa hekima na utamaduni wa mwanadamu! Na hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Lusifa wakati huo, alilofanya katika bustani ya Edeni, nao wakafa papo hapo. Kanisa la Kipentekoste lilifia pale Nikea, Rumi, bali kufufuliwa katika ule Mti wa Bibi-arusi katika siku za mwisho.

⁵⁷² Angalieni, Lusifa anaingia, kwa hila, kama alivyofanya wakati huo, na kwa majaribu na ahadi za uongo, za nguvu nje, mbali na Neno la Mungu. Alifanya vivyo hivyo huko Nikea, Rumi. Anafanya vivyo hivyo leo kwenye Baraza la Makanisa ya Kiekumeni Ulimwenguni.

⁵⁷³ “Tuungane sote pamoja,” papa anasema. “Nataka ndugu zangu wote wa ekumeni huko nje waungane pamoja nami. Sisi ni kitu kimoja.” Hiyo ni kweli, katika madhehebu ninyi ni mmoja. Lakini hiyo haina uhusiano wowote na Bibi-arusi wa Kristo; hata kidogo, ndugu. Kamwe hutamuosha katika kitu kama hicho.

⁵⁷⁴ Sasa imeahidiwa, katika siku za mwisho, kwamba Imani ya asili katika uo huo . . . kurejeshewa watoto wa Mungu wakati wa Mti wa Bibi-arusi. Malaki 4, Mungu alisema, “Kabla ulimwengu haujateketea kwa moto, tazama, nawapelekea Eliya nabii, naye atairezsha Imani ya watoto.” Sasa, huyo hakuwa Eliya wa kwanza aliyekuja. La, la.

⁵⁷⁵ Sasa, hatufundishi hapa joho la Eliya na mablanketi ya Eliya, na mambo hayo yote namna hiyo. Tunafundisha tu Neno la Mungu. Mnaona? Hivyo ndivyo alivyosema. Mnaona, tuna kila namna ya Eliya *huyu* na *Eliya* yule, ambalo ni upuuzi. Hiyo ni—hiyo ni . . . Tunajua hilo. Hiyo ni . . . Sizungumzii hilo, na ninyi wenye nia ya kiroho mnaelewa. Unaona, kwa vile kuchelewa, saa inazidi kuchelewa, na siwezi kuweka yote kwenye kanda hii, hakika.

Sasa, ahadi katika siku za mwisho. Sasa kama . . .

⁵⁷⁶ Yesu alisema, katika—katika Mathayo, naamini, mlango wa 11 ama mlango wa 6, na ninii cha 11 . . . La, ni mlango wa 11 na yapata kifungu cha 6. Wakati Yohana alipowatuma wanafunzi wake kule kuona kama Yeye Ndiye kweli, Yesu alisema, “Mlitoka kwenda kumwona nani? U—u—upepo . . . unyasi unaotikiswa na upepo? Je, mlitoka kwenda kuona *fulani-fulani*?” Akasema, “Au mlienda kumwona nabii?” Akasema, “Aliye mkuu kuliko nabii.” Yohana alikuwa zaidi ya nabii; alikuwa mjumbe wa Agano. Naye akasema, “Ikiwa mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa na manabii, ‘Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.’”

⁵⁷⁷ Sasa, hiyo ni katika Malaki 3, si Malaki 4. Maana, Elisha ambaye angekuja katika Malaki 4, dunia ilipaswa kuteketezwa kwa moto mkali, na wenye haki walipaswa kutembea katika Utawala wa Miaka Elfu Moja juu ya majivu ya waovu. Mnaona? Kwa hivyo si huyo. Mnaona?

⁵⁷⁸ Sasa tunaona ahadi ikitimizwa. Kristo, Uongozi wa kweli akiingia, akiya katika Bibi-arusi Wake, akifanya kazi zile zile alizofanya hapo mwanzo, na kutayarisha na kulitimiza Neno Lake kama alivyofanya, hapo kwanza, katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Basi, Kichwa na Mwili vinakuwa Mmoja, katika matendo na ishara na katika Uzima, imethibitishwa na Mungu Mwenyewe kupitia Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya siku za mwisho. Aliahidi hili katika siku za mwisho. Sasa, kama ninyi ni wa kiroho, mtalipata.

⁵⁷⁹ Halafu, tunaweza kuona kwamba Karamu ya Arusi imekaribia. Sasa, kama sitawaona tena, kumbukeni, Karamu ya Arusi imekaribia. Halafu basi Ufalme kulingana na ahadi uko tayari kuanza, ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu, kunyakuliwa kwa Kanisa, na kuangamizwa kwa waovu. Nao ulimwengu, chini ya Muhuri wa Sita, kutakaswa kwa volkeno, kuchukua

uozo na dhambi zote za ulimwengu na kuufinyanga tena, na kuuleta ule Utawala wa Miaka Elfu kwa ajili ya wakati ujao.

⁵⁸⁰ Wakati, tunapona haya yote, ufunuo mkuu wenye sehemu tatu: Mungu ndani ya Kristo; Kristo ndani ya Kanisa; Ufalme unakuja. Adamu na Hawa wamekombolewa kurudi kwenye bustani ya Edeni, katika uwakilishi wa Kristo na Bibi-arusi Wake, na kisha Ufalme utarudishwa kulingana na ahadi Yake. Mungu asifiwe! Sasa, kwa huo ufunuo wa ile siri yenye sehemu tatu, ile siri, na kwa Neno lililothibitishwa kibinafsi na Ukuu Wake wa asili!

⁵⁸¹ Usiseme, “Vema, utukufu kwa Mungu, tunapaza sauti; haleluya, tunaimba.” Hilo, hilo silo. Mimi ni mmishenari. Nimekuwa mara saba, kwa kweli, duniani kote. Mnaona? Nimewaona wapagani, mashetani, na chochote kile, wakicheza na kupaza sauti. Nimeona kila namna ya madhihirisho ya kimwili. Hayo ni ya kimwili.

⁵⁸² Lakini ninazungumza juu ya Uongozi wa Kristo. Angalia, tukitambulishwa kibinafsi na Uongozi asilia, tuna jibu la swali la ibilisi. Amina! Utukufu! Tuna jibu la swali la ibilisi. Yeye, Kristo, amefufuka na amelipa gharama, na kukifufua Kichwa... au Mwili.

⁵⁸³ Ibilisi hawezi kulistahimili. Hiyo ndiyo sababu falme hizi za kiekumeni zinaanzishwa. Hiyo ndiyo sababu wote wanaingia kwenye kile wanachofanya sasa. Ibilisi, hiyo ndiyo sababu analia kwa sauti kuu jinsi anavyofanya. Uovu wake umekuwa... mbinu zake zimefichuliwa na Kristo aliyeinuliwa, aliyefufuka, aliyefanyika hai katika Ukuu juu ya Mwili Wake. Utukufu!

⁵⁸⁴ Mnafikiri nimerukwa na akili? Sijarukwa na akili. Tuna jibu la ibilisi. “Si mimi ninayeishi, bali Kristo Neno anayeishi ndani yangu.” Sio wazo langu; ni Nguvu Zake. Si wazo langu; ni Neno Lake. Aliahidi hilo; hili hapa. Alisema litakuwa hapa, na hili hapa. Tunalo jibu lake.

⁵⁸⁵ Kristo amefufuka na amelipa gharama ya ukombozi wetu. Kile ambacho Mungu katika Kristo alidhihirisha, aliutoa huo mwili, huo na Damu; ili katika hiyo Damu uje Uzima, ndipo mwili upate kukombolewa, ili—ili Mungu katika mwili huu uliokombolewa aweze kulidhihirisha Neno Lake kwa ajili ya siku hizi kama alivyofanya katika siku hiyo. Whiu! Utukufu!

⁵⁸⁶ Mnaliona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Ninaweza kumalizia lini? Liangalieni. [“Endelea!”]

⁵⁸⁷ Ndipo, tunasimama tumehesabiwa haki Mbele za Mungu. Kama tone la wino linaloanguka kwenye be—be—beseni iliyojaa dawa ya kuondoa madoa, hutawahi kupata hilo doa la wino tena. Lilienda mahali fulani. Kamwe halitarudi tena. Basi mwanadamu anapokombolewa kweli, hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani inaliona na kulikubali, dhambi zake zinaangamizwa. Zimekwisha. Zimetenganishwa.

Zimetupwa kwenye wino wa—wa Damu ya Yesu Kristo, wala hazitakumbukwa tena. Mungu huzisahau. Naye husimama kama mwana na binti wa Mungu, Mbele za Mungu. Amina na amina! “Sasa sisi ni wana wa Mungu.” Si *tutakuwa*; ndivyo tulivyo! Sasa tumekombolewa.

⁵⁸⁸ Tuna jibu la Shetani. Mungu amejithibitisha Mwenyewe. Mungu amejithibitisha Mwenyewe, kwa ahadi Yake katika siku hii. Haleluya! Uongozi uko hapa. Amina! Kristo, Bwana aliyefufuka, yuko hapa katika Nguvu zile zile za kufufuka Kwake alizowahi kuwa, akijidhihirisha Mwenyewe. Hilo hapo jibu la ibilisi.

⁵⁸⁹ Hiyo ndiyo sababu wakati mtu huyu aliyeketi hapa, alipoanguka na kufa hivi majuzi, aliyeketi hapa, tungeweza kusema, “Rudi, uhai!” Maana, Roho Mtakatifu alisema hivyo.

⁵⁹⁰ Hiyo ndiyo sababu ingeweza kumsaidia mtoto huyo mdogo kule Mexico, aliyekuwa amekufa kwa yapata saa kumi na tano, wakati ono lilipokuja na kusema, “Mwite kutoka mau- . . . apate kuishi.” Kisha kasema, “Acha mtoto huyo mdogo aishi.” Ndipo mtoto ambaye madaktari waliandika taarifa, alikufa saa tatu asubuhi hiyo, na saa tano usiku huo akarudia uhai; yu hai leo.

⁵⁹¹ Ni kitu gani? Si hao watu. Uongozi na Mwili vimekuwa kitu kimoja. Ni Mungu akidhihirishwa katika watu Wake. Hiyo ndiyo sababu mume na mke si wawili tena; wao ni mmoja. Mungu na Kanisa Lake ni mmoja, “Kristo ndani yako,” Ufunuo mkuu wa Mungu. Utukufu kwa Mungu! Hata kubeba Jina Lake; Jina Lake ni Yesu, Mtiwa Mafuta. Sababu ya kuitwa Yesu, Yeye ni Mtiwa Mafuta. Ni Mwili wa Kristo uliotiwa mafuta, ukithibitisha, umemdhahirisha Mungu kama mwili Huo ulivyofanya. Nao mwili Huo ulikomboza kila mmoja wa hii, miili hii, na kupitia hapo Mungu anafanya udhihirisho Wake wenye sehemu tatu, akienda kwenye Ufalme. Amefufuka, amelipa gharama! Tumekombolewa. Mungu amelithibitisha, amelithibitisha hilo. Mnaona?

⁵⁹² Nasi tunasimama tumehesabiwa haki katika Kristo, mbele Zake. Kwa sababu, Yeye hawezi kutoa hukumu, kwa maana tayari amehukumu Mwili huo, ambao mimi ni sehemu yake. Je, mimi ni sehemu yake vipi? Hili *hapa*; Yuko ndani yangu. “Ikiwa ninii Yangu. . . mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, basi yale msemayo. . . Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, litatimizwa, kwa sababu liko hapo.” Kuhesabiwa haki! Utukufu kwa Mungu!

⁵⁹³ Loo, laiti ningaliweza kuufanya ulimwengu kuona hilo! Kwa nini? Haya basi. Huo hapo Mwili wa Kristo unaoishi, umesimama umekombolewa. Umekombolewa! Loo, jamani!

⁵⁹⁴ Umehesabiwa haki machoni Pake! Kwa nini tunahesabiwa haki? Sisi ndio ushindi Wake. Kanisa ndilo ushindi Wake. Tunatokea katika siku hizi za mwisho na Injili hii tukufu,

tukionyesha ushindi Wake. Alikufa kwa kusudi hili, nasi ni thibitisho la ushindi Wake. Amina! Tunapomwona akishuka na kuishi miongoni mwa Kanisa, huo ni ushindi Wake. Inaonyesha kwamba hangeweza kumweka kaburini, wala hawawezi kutuweka. Hiyo ni kweli. Tumefungwa vema. Nasi tayari, kwa uwezekano, tumefufuka, kwa sababu tumefufuka katika wafu, kutokuliamini Neno Lake, kutoka katika kanuni za imani za madhehebu, hadi kwenye Neno la Milele la Mungu wa Milele; ambalo ni Yeye, Mwenyewe, akitenda kazi kupitia sisi, akijidhihirisha Mwenyewe ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁵⁹⁵ Ndipo basi Neno linashuka chini kuingia kwenye Mwili, kutoka Kichwani. Ni nini? Neno lili hili. Hakuna kinachoweza kuongezwa au kuondolewa Kwake. Kwa hiyo Neno lilo hilo linatoka Kichwani, kadiri ile Siku inavyokaribia, kuingia Mwili, chini kuingia kwenye Mwili, ikithibitisha ya kwamba wao ni Mmoja. Wao ni Mume na Mke. Wao ni nyama ya nyama Yake, Neno la Neno Lake; Uhai wa Uhai Wake, Roho wa Roho Wake. Mnaona? Amina! Unajua? Huzaa taarifa ile ile, tunda lile lile, Neno lile lile. Mnaona? Humdhihirisha Kristo; Uhai ule ule, Mungu yule yule, Roho yule yule, Neno lile lile, Kitabu kile kile! Amina! Ishara zile zile, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Loo, haleluya! Jamani!

⁵⁹⁶ Angalieni, Neno lililothibitishwa katika Mwili Wake ndilo ushindi Wake hasa na sababu ya kifo Chake. Mnaona, mauti, si katika Roho; alipokufa, alikufa tu katika mwili. Roho Yake ilikwenda kuzimuni na kuwahubiria nafsi zilizokuwa kifungoni. Hiyo ni kweli? Mwili Wake, pekee, ndio uliokufa, kisha akaufufua tena na kuuhuisha. *Kuhuisha* linamaanisha “kufanywa hai,” mwili Wake, ambao ulikuwa ni mwili Wake. Na hilo ni Neno. Limekuwa katika hali ya kufa kwa miaka mingi, lakini polepole likianza kuja katika yale matengenezo, na sasa limesimama kwa miguu Yake!

⁵⁹⁷ Loo, laiti ninge kuwa na wakati wa kurudi katika Ezekieli, na kuitoa nje “mifupa mikavu,” na kuwaonyesha. Alisema, “Je, mifupa hii inaweza kuishi tena?”

Akasema, “Tabiri!”

⁵⁹⁸ Unabii unawezaje kuja? Kwa njia ya nabii pekee. Ni Neno la Bwana. “Sikieni, enyi mifupa mikavu, Neno la Bwana!” Na mishipa, ngozi ikawajia, nao wakasimama jeshi kuu, na kuanza kutembea kuelekea Sayuni. Utukufu kwa Mungu! Huyu ni Yeye. Huyu ni Yeye, ushindi.

Waliokombolewa wa Bwana watakuja Sayuni
basi kwa furaha,
Milima Yake yote mitakatifu hakuna kitu
kitakachodhuru wala kuharibu. (Huh.)

599 Yeye huthibitisha Uzima Wake wa ufufuo basi kadiri anavyojithibitisha Mwenyewe. Yeye, Bibi-arusi, yuko huru na wengine wote. Yeye ni Mwanamke huru, Ndege mkubwa mwenye madoadoa ambaye ni tofauti na wengine wote. Mnakumbuka Biblia juu ya hilo, “Ndege mkubwa mwenye madoadoa.” Lakini, alikuwa na Jina Lake, Mke alikuwa na Uzima Wake. Kwa ajili ya...

600 Walimtiaje madoadoa huyo ndege? Wote wawili walikuwa weupe, ndipo wakaking’oa kichwa cha ndege mmoja na kuimimina hiyo damu juu ya huyo ndege mwingine. Ndipo basi huyo ndege mwingine akawa na madoadoa ya damu nyekundu, naye akapigapiga mabawa yake namna *hii*, ndipo hiyo damu ikalia, “mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” huku ikiilowesha ardhi.

601 Kwa hiyo Kristo, Mwenzi aliyekufa, aliweka Damu Yake, Damu Yake kutoka kwa Uhai Wake, ndani yetu; nyunyuni... akiibeba Damu Yake, akilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana!” Ni ndege mwenye sura iliyo ya kipekee. Hakika, ndivyo. Lakini Yeye, Bibi-arusi, a—ametambulishwa Naye, naye ni huru na wengine wote. “Umlinde yeye pekee maadamu nyote wawili mngali hai. Kaa tu Naye, yule Neno,” hakuna, hakuna uzinzi, hakuna ishara moja ya madhehebu, hakuna dalili moja ya kanuni za imani, hakuna uzinzi hata kidogo. Neno, na Yeye pekee!

602 “Juu ya Kristo mwamba wenye imara nasimama, sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,” alisema Eddie Perronet. Uh-huh.

603 Ndivyo hivyo, Kristo, Neno! Yeye alikuwa Neno; Yeye ni Neno. Nalo Kanisa linakuwa Neno, kwa Yeye kumfanya kuwa sehemu Yake, na hilo ni Neno tena. Limetambulishwa binafsi Naye, mali Yake peke yake! Mali yake peke yake! Limekombolewa Naye, kupitia Kwake, kwa ajili Yake, na kwa ajili Yake pekee. Hiyo ni kweli. Halafu, kile ibilisi anacholilia, kwamba kinafunuliwa.

604 Tuko katika wakati wa hatari. Kumbukeni, Maandiko yanasema, mambo haya yatakapoanza kutukia, “wakati haupo tena.” Anafifia, tutakapoona yale madhihirisho.

605 “Matetemeko ya ardhi.” Mliwaona elfu waliouawa hivi majuzi? “Matetemeko ya ardhi mahali mahali.”

606 Kasema, “Vitu vya kutisha angani, vitu kama nguzo za moto,” vikielea kama visahani virukavyo. Hawajui ni nini. Mnaona? Hawana fununu yoyote.

607 Je, mliwaona wale Malaika walioshuka chini, waliochunguza Sodoma kabla ya Sodoma kuangamizwa? Mnakumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kulikuwa na kundi la Hao lililoshuka, watatu Wao. Mmoja Wao alibaki na Ibrahimu. Mnakumbuka hilo? [“Amina.”] Wao walikuwa ni Nuru kutoka

Mbinguni, zilizoshuka katika hukumu ya kuchunguza. Mmoja ni...

608 Angalia mahali wote wanapopatikana. Karibu na Pentagoni, na kadhalika, wanawapata. Hiyo ndiyo hukumu ya ulimwengu, Sodoma. Na kuna Mmoja anayewakilishwa, atakayewakilishwa miongoni mwa makanisa, atakuwa ni Kristo Mwenyewe, akijithibitisha Mwenyewe. Mnaona? “Kuona mambo... mbinguni juu, na ishara katika nchi chini.” Hakika.

609 Kutambulishwa! Loo, ibilisi anapiga mayowe juu ya jambo hili: Kweli iliyodhihirishwa ya ahadi ya Neno ndani Yake pekee.

610 Hawana jibu. Yesu alipokuja, kwa nini hao Mafarisayo hawakuja? Alisema, “Ikiwa natoa pepo kwa kidole cha Mungu, ninyi mnawatoa kwa kitu gani?” Mnaona? Alisimama peke yake.

611 Nalo Kanisa Lake linasimama peke yake. Yeye hajafungwa na chochote. Bali Yeye alitambulishwa na Mungu, akiwa ni mwili ambao Mungu aliishi ndani yake; na Kanisa linatambulishwa na Mwili Wake, likifanya jambo lile lile. Yeye ni Mwili Wake, Kweli iliyodhihirishwa ya Neno Lake lililoahidiwa kwa siku za mwisho. Naye, na Yeye pekee, anasimama Nalo. Hiyo ndiyo sababu ibilisi anapiga mayowe, madhehebu haya makuu, kuanzisha kitu fulani apate kumfungia. Hawatafanya hivyo kamwe. Atatwaliwa juu, sio kufungiwa. Sasa amefufuka, na kwa nguvu za Neno lililothibitishwa aliloahidiwa. Amina!

612 Jinsi Bibi-arusi anavyoshikilia ahadi hiyo! “Aliniambia atarudi kunichukua. Nitaamini hilo.” Uh-huh. Unaona? Naam, bwana. Kukutana na Uongozi Wake, Mkombozi Wake, Mumewe, Mfalme Wake, Bwana Wake, Mpenzi Wake, Mwokozi Wake, katika mahali palipoandaliwa pa kukutania!

613 Ana mahali pa kukutana nao. Mwajua, Yeye—Yeye... Bwana arusi haachi chochote. Anayo pete, ule utambulisho. Analoo joho ambalo Mkewe anavaa, mavazi Yake. Mnaona? Naye ana mahali palipoandaliwa kukutana Naye, huko ni hewani. Kila kitu kimeandaliwa kabisa. Ameshaandaa Karamu ya Arusi; tayari wageni wamealikwa, tayari wamechaguliwa. Malaika wote wamesimama karibu, watumishi Wake, miguu sawa. Loo, loo, loo, loo, loo!

Loo, kutakuwa na mkutano hewani,
Katika utamu huo, utamu hivi karibuni;
Nitakutana nawe, nitakutana nawe Huko
Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
Uimbaji mzuri sana uliopata kusikika,
kusikika na masikio ya mwanadamu,
Itakuwa adhimu, ninatangaza!
Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, atakuwa
Ndiye anayeongoza, (dhihirisho kamili la
Mungu.)
Katika mkutano huo hewani. (Loo, jamani!)

614 Tazama uthibitisho Wake sasa.

Umesikia—umesikia hadithi ikisimuliwa
 kuhusu Musa kichakani,
 Umesikia juu ya shujaa Daudi na kombeo lake;
 Umesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu
 mwota ndoto,
 Ya Danieli na simba tunaimba mara kwa mara.
 Loo, kuna wengi, wengine wengi
 waliothibitishwa katika Biblia,
 Jinsi ninavyotamani kukutana nao wote,
 natangaza!
 Pole pole Bwana atatujalia kukutana nao,
 Katika mkutano huo hewani.

Kwa maana kutakuwa na mkutano angani,
 Katika utamu huo, utamu baadaye;
 Nami nitakutana nawe, nikusalimu Huko
 Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
 Uimbaji mzuri sana uliowahi kusikika,
 umesikika na masikio ya mwanadamu,
 Itakuwa adhimu, natangaza!
 Na Mwana wa Mungu Mwenyewe atakuwa
 Ndiye anayeongoza
 Katika mkutano huo hewani. (Loo, jamani!)

615 Je, hamuupendi huo? Sasa kusudi lenye sehemu tatu la siri
 Yake kuu ya ufunuo limefunuliwa. Yeye ndiye Mkuu. Huyu
 Ndiye. Loo, jamani! Hebu tuuimbe. Kamwe siwezi kuhubiri
 tena. Najisikia vizuri sana, mnaona.

Loo, kutakuwa na mkutano angani,
 Katika utamu huo, utamu hivi karibuni;
 Nami nitakutana nawe, nikusalimu Huko
 Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
 Uimbaji mzuri sana uliowahi kusikika,
 umesikiwa na sikio la mwanadamu,
 Itakuwa adhimu, ninatangaza!
 Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, Yeye
 atakuwa Ndiye anayeongoza
 Katika mkutano huo hewani.

616 Je, unaenda? Amina! Kwa neema ya Mungu, kwa neema ya
 Mungu! Unaona? Loo, jamani!

Mmesikia habari za maskini Musa kichakani,
 Mmesikia habari za Daudi asiyeogopa na
 kombeo lake; (Wao ni vivuli.)
 Mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu
 mwota ndoto,
 Na ya Danieli na simba tunaimba mara kwa
 mara.

Loo, kuna wengine wengi sana katika Biblia,
 (Ambao ni Yeye)
 Na ninatamani kukutana nao wote, natangaza!
 Karibuni Bwana atatujalia kukutana nao
 Katika mkutano huo katika . . .

617 Lakini kuna Mmoja mkuu!

Loo, kutakuwa na mkutano hewani,
 Katika utamu huo, utamu hivi karibuni;
 Nitakutana nawe, nikusalimu Huko
 Katika makazi hayo ng'ambo ya anga;
 Uimbaji mzuri sana uliowahi kusikika,
 umesikika na masikio ya mwanadamu,
 Itakuwa adhimu, ninatangaza!
 Naye Mwana wa Mungu Mwenyewe, atakuwa
 Ndiye anayeongoza
 Katika mkutano huo hewani.

618 Sasa, tutakutana sisi kwa sisi Kule. Hebu sote,
 Wamethodisti, na Wabaptisti, na chochote ulicho, ambao
 wamezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, tupeane mikono
 sisi kwa sisi tunapouimba.

Loo, kutakuwa na mkutano angani,
 Katika utamu huo, utamu hivi karibuni;
 Nitakutana nawe, na kukusalimia Huko
 Katika Makazi hayo ng'ambo ya anga;
 Uimbaji mzuri sana uliopata kusikika,
 umesikika kwa masikio ya mwanadamu,
 Itakuwa adhimu, ninatangaza!
 Kwa maana Mwana wa Mungu Mwenyewe
 Ndiye atakuwa anaongoza
 Katika mkutano huo hewani.

619 Loo, loo, loo! Loo, hilo ni ajabu, angalieni, angalieni
 atakavyokuwa. Sasa tazameni.

620 Inabidi tu tufunge, marafiki. Ni karibu saa nane, mnaona,
 na tuta—tutakuwa hapa kwenye chakula cha jioni. Bado nina
 ukurasa baada ya ukurasa wa jambo hili, mnaona, kwa hiyo
 itatubidi tu kufungia kwenye hili. Hakuna mwisho wake.

621 Ni ufunuo. Ni wa Milele kama vile Neno la Mungu lilivyo
 la Milele. Tazama, lakini kusudi lenye sehemu tatu la siri
 kuu ya Mungu limefunuliwa! Mungu akidhihirishwa katika
 Kristo; Kristo akidhihirika katika Kanisa; ili kumkomboa Hawa
 aliyepotea arudi kwenye hali ya awali katika bustani ya Edeni.
 Loo, jamani!

622 Loo, kutakuwa na nyakati nzuri sana kwenye Siku hiyo!
 Naam. Ni sasa hivi. Tunaamini. Je, hamuamini hilo? Ninauwazia
 tu wimbo huo kila ninapoliwazia.

⁶²³ Alijithibitisha Mwenyewe katika Danieli, na katika Musa, na katika Yeremia. Walikuwa nini? Manabii ambao Neno liliwajia, mnaona, hao watu mashuhuri. Mnaona, mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu aliyeota ndoto, mnaona, na Danieli katika tundu la simba, na hawa wengine wote, mwajua. Hao, ambao, walikuwa nini? Manabii. Mnaona? Lakini aliye Mkuu. . . Mungu alikuwa tu, kwa muda, akiainisha ndani yao.

⁶²⁴ Alijifananisha Mwenyewe katika Adamu, akijua lililo sahihi, bali akatoka kwenda kumkomboa mke wake, kwa maana alikuwa amekosea. Haikumlazimu Kristo kuwa dhambi, bali alitoka nje na kuitwaa dhambi, ili kumkomboa mtoto Wake aliyepotea. Mnaona? Mnaona? Alijifananisha Mwenyewe.

. . . na Musa kichakani,
Na mmesikia habari za shujaa Daudi na
kombeo lake;
Mmesikia hadithi ikisimuliwa ya Yusufu
mwota ndoto, (Nabii.)
Na ya Danieli na simba tunaimba mara kwa
mara.
Loo, kuna wengi, wengi sana katika Biblia,
Na mimi. . .

⁶²⁵ Wao, wao ni Biblia.

Na mimi. . .

Wote walidhihirishwa ndani Yake, hata hivyo. Mnaona? Bila Yeye, wote wamepotea. Mnaona? Nami sina budi kuwa sehemu ya Hilo, niwe Yeye. Amina! Mnaona?

Na ninatamani kukutana nao wote, natangaza.
(Hiyo ni kweli.)
Lakini Mwana wa Mungu Mwenyewe, Yeye
atakuwa Ndiye anayeongoza
Katika mkutano hewani.

⁶²⁶ Waebrania 11, ilisema, “Hawangeweza kuwa wakamilifu bila sisi.” Mikono na miguu haiwezi kuwa mikamilifu bila akili, maarifa, kichwa, na kadhalika. Mnaona? Na sisi sote tunakamilishwa ndani yake, “Kwa hiyo kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja,” huru na Hukumu; tumepita kutoka dhambini, kuingia mautini. . . Amina! “Mwana wa Mungu Mwenyewe atakuwa Ndiye anayeongoza kwenye mkutano huo hewani.” Mnampenda?

Nampenda, nampenda
Kwani. . .

⁶²⁷ Bwana Yesu, upako wa Roho Mtakatifu uje juu ya lesi hizi, Bwana, na uwaponye wagonjwa. Na iwe hivyo, kama walivyoiweka juu yake. Ninaomba ya kwamba utafanya hivyo, katika Jina la Yesu. Amina.

. . . mtini Kalvari.

628 Hebu wazieni, “Kristo, akifunuliwa,” moja kwa moja ndani yetu sasa, sasa hivi ndani yetu. Jinsi gani, alifunuliwaje? Kwani alinipenda kwanza. Alifanya nini?

Na kununua wokovu wangu
Juu. . .

629 Utukufu! Yule Malaika mkuu wa Agano, Yule aliyekuwa pamoja na Musa nyikani, Yule aliyemjia Paulo akienda zake Dameski, Yeye yule aliyeruhusu picha Yake ipigwe pamoja nasi; Yule yule aliyekuwa kwenye ile picha kwenye gazeti la *Life* hivi majuzi; Neno lile lile, kwa Mungu yule yule, kupitia njia zile zile, kwa mapito yale yale, kwa ahadi ile ile! “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nipo hapo miongoni mwao.” Basi Yeye yuko hapa. “Malaika wa Mungu wamefanya kituo kuwazunguka wamchao,” wanaotegemea Neno Lake tu. Hakuna mtu anayeweza kuliheshimu Neno hilo bila kumcha Mungu. Unaona? Basi, Yeye yuko hapa ndani asubuhi ya leo, pamoja nasi, tunapomwabudu katika Roho.

630 Loo, tukiwa na Ujumbe mgumu kama huu, nafikiri inatupasa tu kumwabudu kidogo katika Roho. Unaona, funga tu macho yako na tumwimbie Yeye tena, “Nampenda, nampenda,” huku mki—mkiinua tu mikono yenu, hivyo, Kwake.

Nampenda, nampenda
Kwani. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Loo, jamani, jinsi tunavyompenda!

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, hawa watatu ni
Mmoja;
Pepo watatetemeka, na wenye dhambi
wataamka;
Imani katika Yehova hufanya chochote
kitikisike.

631 Amina! Utukufu kwa Mungu! Jinsi tunavyompenda! Mwabuduni tu moyoni mwenu sasa, mwabudu Yeye tu, wa—wazia tu jinsi alivyofanya vizuri. Angalia kile Yeye ametufanyia. Miaka yote hii ya maono, hakuna hata moja lililowahi kushindwa. Kila kitu alichosema kingetimia, kilitimia tu kama vile Yeye alivyosema.

632 Nawapenda. Msisahau amri za Mungu kwenu, watoto wadogo, “Pendaneni.” Mpende kila mtu. Awe sahihi ama makosani, mwenye dhambi ama mtakatifu, wapende, kwa vyovyote vile. Kama huwapendi, basi mwombe Mungu akusaidie, maana Mungu alimpenda mwenye dhambi. Na asili ya Mungu iko ndani yako. Kama mtu yuko makosani, mpende, hata hivyo. Usishiriki dhambi zake. Unaona? Usishiriki dhambi zake. Lakini kwa utamu, si kwa uchungu na kukemea, kwa

utamu mwambie juu ya tumaini la Uzima lililo ndani yako, kwa njia ya Yesu Kristo akifunuliwa kwako na Roho Mtakatifu.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na wa majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Loo, lipeleke (Usisahau sasa.) kokote uendako.
Loo, thamani . . . (Jina hilo!) . . . O . . .

633 Tunalo Jina Lake. Tunaitwa kwa Jina Lake.

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

634 Sasa nitawapa siri ndogo, mpaka nitakapokutana nanyi tena, kumbukeni hili, tunaposimama, kumbukeni hili:

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvika taji,
(Tutamvika taji!)
Safari yetu itakapokamilika.
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) (Loo jinsi lilivyo tamu!)
Matumaini ya . . .

635 Ati nini? Ufunuo wenye sehemu tatu! Tumaini na furaha ya Mbinguni, iliyofunuliwa ndani Yake.

Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya . . .

636 Ati nini? Tumaini la dunia na furaha ya Mbinguni, kila kitu kinadhihirika katika Kristo. Mungu, Kanisa, kila kitu kingine chochote, kimedhihirishwa katika Kristo. Biblia ni Kristo. Biblia ni Neno lililoandikwa. Ambapo, Yeye ni Neno. Kudhihirishwa Kwake ni thibitisho la Uhai ukija katika mwili wa Neno, kulidhihirisha. Loo, si ni ajabu!

Peleka Jina la Yesu pamoja . . .

Sasa sikilizeni kwa makini sasa.

Kama Ngao . . . (Usisahau hilo sasa.) . . . kila mtego;
Wakati majaribu yakikuzunguka, (Unapaswa kufanya nini?)
Litamke tu Jina hilo Takatifu katika maombi.
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu! (Loo jinsi lilivyo tamu!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

⁶³⁷ Bila kujua...Bila shaka, ukiwa wa kiroho, unatazama mambo ya kiroho. Bila kujua hili; Mungu anajua. Lakini kama utageuka na kuangalia saa ya ukutani, iko kwenye nukta, saa nane kamili, mwisho wa Mvuto wa Pili. Mvuto wa Tatu umekaribia! Mnaona?

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa
wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.
Jina la thamani...

Mvuto wa Pili umedhihirika!

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

⁶³⁸ Je, mmeona Roho akichukua wimbo ule ule na kuuinua juu oktava moja zaidi namna hiyo? Mvuto unaofuata umekaribia! Amina! Uh-huh.

Peleka Jina la Yesu,
Imechelewa kuliko unavyofikiria!
...huzuni na wa mashaka;
Litakupa furaha na faraja,
Loo, peleka uendako.
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi
lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha...

Sasa majaribu yakija, unafanya nini?

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Wakati majaribu...(Kitu cha kukufanya
usiamini sasa)...yakikusanyika,
Kumbuka tu, tamka hilo Jina Takatifu katika
maombi.
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi
lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

⁶³⁹ Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kila mtu, kwa kicho. Tazama sasa.

Tukilisujudia Jina la Yesu...

⁶⁴⁰ [Lugha na tafsiri zinatolewa—Mh.] Sasa kama mnaelewa, Roho wa Bwana alishuka katika mkutano, juu ya lugha

zisizojulikana, akizungumza na mtu asiyejua; kutafsiri kwa mtu mwingine bila kujua. Neno la Bwana! Mnakumbuka wakati adui alipokuwa anakuja na hawakujua wangepanya nini? Roho wa Bwana alishuka juu ya mtu, na kufunua kile ambacho kilikuwa kinaenda kufanyika. Loo, jamani!

⁶⁴¹ Tuinamishe tu vichwa vyetu sasa, kwa unyenyekevu. Mungu awabariki.

Hata twonane! Hata twonane!
Mpaka tukutane miguuni pa Yesu;
Hata twonane!

Vema, mchungaji. 

63-0728 Kristo Ni Siri Ya Mungu Iliyofunuliwa
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org